ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Tatu – Tarehe 30 Julai, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HATI YA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani, Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Marina Joel Thomas: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Kilimo na Maliasili

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na tunakusudia mjadala huu wa hotuba ya bajeti hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, umalizike mnamo saa 5:00 za asubuhi hii. Hii inatokana na ufinyu wa muda tuliokuwanao, na baada ya hapo tumuombe Mhe. Waziri baada ya Naibu Waziri kuanza kufanya majumuisho. Hali hairuhusu kabisa kuendelea na mjadala, kabisa kabisa hairuhusu.

Sasa tutaona utaratibu tutakaouweka baadae ambao kama nilivyoomba jana kama mara mbili. Kwa hivyo, nitawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuje tukubaliane na hayo mawazo ambayo nitayatoa, ili tuweze kumaliza shughuli zetu mapema. Hivyo, itabidi tuwe na utaratibu wa kuwataja Waheshimiwa Wajumbe ambao watapata nafasi kwa huo muda wa saa kama mbili hivi mpaka hapo tutakapofunga mjadala wetu.

Watakaopata nafasi ni pamoja na Mhe. Subeit Khamis Faki. Ikitokea mmoja hayupo wakati huo basi nachupia kwa mwengine, kwa wakati ule hatutokuwa tunamngoja mtu, mwengine ni Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Asha Abdu Haji na hii inakwenda kwa mujibu wa aliyewahi kuomba, aliyeomba mwisho huko tena ndio itakuwa naomba radhi. Mwengine ni Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Mussa Ali Hassan na inaelekea tutaishia kwa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baada ya hapo tumuombe Mhe. Naibu Waziri aanze kumsaidia Mhe. Waziri kwa kutoa majumuisho na hatimaye Mhe. Waziri amalizie.

Waheshimiwa Wajumbe, hiyo naomba mniwie radhi sana na niwaombeni radhi sana. Hali halisi ndio hiyo, ndio mambo yalivyo. Kwa hivyo, wengine watakaofuata baada ya hapo ambao hadi sasa majina niliyonayo ni pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Abdalla Moh'd Ali, Mhe. Ashura Sharif Ali na Wajumbe wengine walioleta sasa hivi ni pamoja na Mheshimiwa wangu sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Hawa waanze kujitayarisha kumpelekea maandishi Mhe. Waziri mapema sana, ili apate namna ya kuweza kutafuta majibu kwa kuwapa wale watendaji kazi wake wamsaidie. Waheshimiwa Wajumbe naomba radhi sana hali halisi ndio hiyo.

Majadiliano yanaendelea, sasa naomba nimuite Mhe. Subeit Khamis Faki. Nikuombe Mhe. Subeit utumie dakika 15 tu kutokana na hali hiyo, ukipunguza nitakufurahia sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa asubuhi hii ya leo na mimi kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, hii ni wizara ambayo pia ni muhimu, kwa sababu ina mambo muhimu ya uti wa mgongo wa nchi yetu, kwa sababu Wizara ya Kilimo na Maliasili ni wizara muhimu sana. Mhe. Spika, kwa makusudi baada ya Baraza hili la mwanzo Mhe. Rais alipokuja kutuhutubia hapa alitangaza kwa makusudi kama sasa hivi tunaingia kwenye Mapinduzi ya kilimo, na kwa bahati nzuri wizara hii ina wataalamu wengi sana.

Lakini Mhe. Spika, mimi kidogo nina masikitiko kuhusu hayo Mapinduzi ya kilimo, ambayo mimi naona bado hayajafanikiwa, na hasa ukizingatia kwamba Mapinduzi ya kilimo yameelekezwa kwenye kilimo cha mpunga tu, kumbe kilimo sio kilimo cha mpunga tu. Kuna vilimo ambavyo kuwa ni sehemu za ardhi ya mawe, lakini bado serikali haijajikita kwa makini ili

kuangalia kama kuna haja ya kuboresha na kuona wananchi wetu wanalima vilimo vya kujipunguzia umaskini na kujiongezea kipato.

Mhe. Spika, suala la mikarafuu ni kilimo ambacho kilikuwa kinatuendesha katika nchi yetu, pamoja na kuwa sasa hivi tunasema kwamba utalii ndio biashara ambayo inachukua nambari moja, lakini bado mimi nasema mikarafuu ni kilimo ambacho kinaongezea mapato ya nchi yetu na ni kilimo ambacho tunategemea katika nchi yetu. Lakini sasa hivi pamoja na kuwa Kilimo kuna wataalamu wengi, lakini bado mikarafuu inakufa kwa wingi na hawajatueleza katika utafiti wao kwamba hii inasababishwa na kitu gani, na kuendelea kuona kama mikarafuu ni kilimo ambacho kinahitaji kuongezewa nguvu zaidi.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aone bado kuna haja ya kuhuisha mikarafuu, katika huo uwekezaji wa miche basi wakaona kuwa kuna haja ya kuipa nguvu mikarafuu ili iendelee kuhuishwa mikarafuu.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala la minazi. Minazi Zanzibar imekatwa mingi na hakuna hata uhamasishaji wa kupanda minazi mingine. Zamani ilikuwa minazi inahamasishwa sana kupandwa, lakini sasa hivi naona kama imesahauliwa kabisa kama kuna kilimo cha minazi, na wakati minazi ilikuwa nayo inasaidia kukuza uchumi na kusafirisha biashara ya mbata ambazo zilikuwa zinasaidia serikali mapato, lakini sasa hivi minazi inakatwa na hakuna uhamasishaji wa kupanda mingine.

Mhe. Spika, zamani ilikuwa serikali inapanda mashamba, inahimiza watu kufanya kazi ya kupanda minazi, lakini sasa hivi hakuna. Mhe. Spika, pamoja na wataalamu wengi na mabwana shamba wengi waliopo, lakini bado mabwana shamba wamekaa kitako hawapiti mashamba kuwaelekeza watu na kuwahamasisha kulima vilimo na kwa wakati unaotakiwa. Mabwana shamba wamekaa kitako na utaalamu wao.

Mhe. Spika, juzi nilipigiwa simu nikaitwa Makunduchi, kwa bahati nzuri mimi na Mhe. Hija tulikuwa na safari ya kwenda Makunduchi, tuliitwa na wakulima. Tulipofika Makunduchi Mhe. Spika, wakatupeleka katika eneo moja la Makunduchi ambalo linaitwa Kajengwa, lakini huko Makunduchi tulipelekwa mpaka mashamba tukaona hali ilivyo.

Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha sana, na ni aibu sana kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, inasikitisha na inahuzunisha. Tumewahamasisha wakulima, wameitikia wito wa serikali, wamelima vilimo ambavyo ni vya biashara, wamepanda michungwa mingi ya biashara na yanazaliwa mengi

mno, lakini machungwa hayo yameingiwa na wadudu yanapuputika, ukifika chini ni kama zilizomwagwa chini kwa makusudi.

Mhe. Spika, utatamani kulia kabisa, mtu anakwambia mimi hapa nilikuwa nategemea kupata shilingi milioni 2, lakini sasa hivi hata shilingi 200,000 siwezi kuzipata. Mhe. Spika, hakuna bwana shamba anayepita, hakuna mtu wa kilimo anayepita, hakuna utaratibu wowote unaoandaliwa wala hakuna fikra zozote wanazopewa wale wakulima, ilimradi ni masikitiko makubwa wanahuzunisha kwa kweli.

Mhe. Spika, mimi naomba sana atakapokuja Waziri anieleze na nitakuwa mkaidi sana katika kifungu hiki cha Idara ya Sera na Utafiti kwa sababu hawa ndio mambo yao. Kwa hivyo, nitakuwa mkaidi kweli kweli mpaka anieleze kwamba watu wale serikali itachukua hatua ya kuwasaidia kama ni dawa au kama ni kuwapa utaratibu wowote, lakini wahakikishe kama yale machungwa yanapatikana.

Mhe. Spika, kwa upande wa pili kuna sehemu za Jimbo la Mhe. Jaku Hashim Ayoub tumekwenda na kule kuna ndimu zinapukutika, hapana pa kuuzwa ndimu, kuna ndimu zimejaliana lakini hakuna pa kuuza. Sasa sisi tunawahimiza watu wanaitikia, kwa nini serikali isiwatafutie soko watu. Kwanza kama hizi ndimu ukawatafutia soko wakawa wanauza ndimu zao na kujipatia kipato, na hayo machungwa kwa nini wadudu wale ambao wanaitwaa, hapana Mhe. Spika, jina lao limenipita basi nitaendelea hivyo hivyo.

Mhe. Spika, kwa kweli hawa wadudu, wataalamu wao wanawajua zaidi. Kwa kweli serikali inatakiwa iwasimamie vizuri wananchi wake. Kwa hivyo, atakapokuja Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili hapa anieleze na mpaka atakaponipa maelezo mazuri kwamba watu hawa watashughulikiwa ili kile kilimo chao wanachokilima kiweze kuwafaidisha, kuliko vile tunavyofanya. Kwa sababu wao wanasikitika na wanahuzunisha. Utakwenda utawaona wazee wengine wanahuzunisha. Kuna mzee mmoja ana mguu mmoja kidogo ni mzito, lakini hayo mashamba yake aliyotuonesha anayolima kwa kujikaza kabisa, lakini ukija kutizama havuni.

Mhe. Spika, hiyo ardhi yenyewe kule ukiiangalia kuna migomba inayomwagiliwa maji, watu wanachukua maji wakimwagilia kwa ndoo, ndizi zinazopatikana ni nzito kweli kweli, kwa ukanda wa kule Makunduchi pamoja na Micheweni. Lakini kwa nini serikali isifanye utaratibu ikawa wanamwagilia na wale watu wa maweni kule sehemu za mawe, lakini leo tunaelekeza kwenye mpunga tu, kumbe hatuli wali tu, kuna ndizi zinatakikana kama mwezi huu wa Ramadhani huwezi kula wali tu, unataka ndizi, unataka

mihogo, ardhi zinakubali za maweni. Lakini leo serikali haiandai utaratibu wa kumwagilia, bahati nzuri mimi kila siku nalizungumza suala hili kama Micheweni kule, alikuja Rais, akaja Makamu wa Pili wa Rais, akaja Makamu wa Kwanza wa Rais wakazunguka pale na wakakagua eneo, wakasema hili eneo litakuwa ni la kilimo cha mfano wa kumwagilia maji. Patachimbwa kisima halafu watu wamwagilie ili ipatikane migomba kwa njia ya kumwagilia, lakini ghafla suala lile naona lilififia moja kwa moja halitajwi na wala halipo tena kabisa, kwa nini? Kwa hivyo, kama tuna Mapinduzi ya kilimo, mimi naomba tusiseme kwenye vitabu tu, tuseme lakini na vitendo vionekane kama tunafanya. Halafu na hawa wananchi wakishalima vilimo vyao basi serikali isimamie.

Kwanza wale wananchi wanaoharibikiwa machungwa, basi aje aniambie Waziri kama watawasaidia vipi wananchi wale. Wao kwa sababu wameshapata hasara na kilimo chao walichokuwa wakitegemea ni machungwa, na machungwa yameshaingiwa na wadudu yameshapuputika yote.

Je, watawasaidia vipi kuona kwamba wanawaendeleza ili waweze kujiendeleza zaidi. Kwa sababu chupa moja ya dawa ni shilingi 8,000, na bahati mbaya mno wanatuambia kwamba walikuwa wanachukua hizo chupa za dawa, wakaweka katika vituo, lakini haikuua kitu chochote. Kwa hivyo, je serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia watu hawa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la haya mambo ya mali asili yetu, ambapo katika kipindi kilichopita nilizungumza na mpaka sasa nazungumza. Sasa nataka Waziri aje aniambie, kwa sababu tumeshazungumza, wenzetu mali asili zao zinawasaidia katika utalii na nilizungumza kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, tulikwenda China kule tukawaona wenzetu wanavyowaghushi wale panda na wanavyoingiza pesa katika Utalii. Sasa na hapa kwetu tunao wale Kimapunju, tuna Popo ambao hawapatikani katika nchi yoyote ile ila hapa Zanzibar tu. Sasa Mhe. Waziri aje aniambie kama wameandaa utaratibu upi na ni fedha zipi zinazoingia kwa hizi mali asili zetu tulizonazo katika misitu yetu. Mhe. Spika, kule Micheweni wako Popo wengi sana katika msitu wa Micheweni, na wapo katika maeneo mengine na watalii wanahitaji. Sasa ule utaratibu, lakini je ni utaratibu upi tunaowawekea, ili kuona kama hizi mali asili zetu zinasaidia kuingiza pesa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu wenzetu, yule komba wa kawaida basi anaingiza pesa katika utalii, kwa sababu watu wana utaratibu maalum wa kujua kama eneo hili wanapatikana komba, basi wanapelekwa watalii wanawaangalia

komba fedha zinaingia katika nchi, lakini sisi tupo tupo tu. Vitu vya kupatia fedha vipo, lakini kuvijengea utaratibu tukapata fedha hamna.

Mhe. Spika: Unazo dakika tatu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Baada ya mchangio wangu huo mfupi na baada ya kupata maelezo ya kina kutokana na walimaji wale wa michungwa wanaoathirika, akinipa jawabu nzuri Mhe. Waziri basi nitaunga mkono, lakini kama hajanipa jawabu nzuri, basi kifungu hiki cha Sera na Utafiti nitakuwa mkaidi kweli Mhe. Spika.

Baada ya hayo Mhe. Spika, ninakushukuru sana, nitaunga mkono baada ya kupata majibu mazuri, ahsante nakushukuru.

Mhe. Spika: Mhe. Subeit Khamis, nakushukuru sana maana umeniokolea muda. Tumkaribishe basi Mhe. Panya Ali Abdalla na baadae Mhe. Asaa Othman Hamad.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi hii kutujaalia kufika hapa. Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii. Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba yao hii.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 28 kwenye Idara ya Misitu na Maliasili Zisizojesheka. Mhe. Spika, idara hii inashughulika sana na uoteshaji wa miche, mimi nilikuwa nataka nizungumze hasa miche hii ya mikarafuu ambayo hili ni zao kuu la biashara.

Mhe. Spika, mimi niseme miche inayooteshwa bado ni kidogo, wakulima hatuenei maana yake bado kuna mapungufu. Lakini pia nilitaka niiombe serikali kwa kuwa hili ni zao kuu la biashara, basi wale pia watakaopatiwa ile miche serikali iweze kuwafuatilia na wakulima wale wapewe utaalamu ili waweze kuilea vyema miche ile na iweze kukua, hali ikiwa tuna matumaini tumeongeza katika upandaji wa miche. Lakini tukiitoa tu ile miche halafu tukiacha kufuatilia, maana yake inaonekana miche mingi inakufa na inayopona ni kidogo, pengine ni kwa kukosa utaalamu wa kuilea ile miche pale tunapoipanda. Kwa hivyo, mimi ombi langu lilikuwa hilo.

Mhe. Spika, pia katika idara hii kuna uzalishaji wa mpira. Mimi naiomba serikali au Waziri atakapokuja atueleze, mimi bado sijaiona ile faida kubwa inayopatikana katika zao lile, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutuelezea ni kiasi gani serikali inafaidika na mradi ule wa mpira na kama

hakuna faida basi hayo maeneo tungewapatia wakulima wetu ili wakafaidika na kilimo.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 22 kwenye taasisi ya utafiti wa kilimo. Mhe. Spika, kwa kweli bado tuna tatizo kubwa, na tatizo letu ni wakulima ambao tunakosa wataalamu. Bado wale mabwana na mabibi shamba hawatufikii wakulima, na sisi bado tunaendelea kulima kile kilimo ambacho tumekizoea, na siku zote tunashauriwa tusilime kilimo ambacho tumezoea tulime kilimo cha kitaalamu. Sasa mimi ombi langu ni kwamba wataalamu hawa bado wangeshuka mabondeni kwa wakulima, na ikiwa hawana nafasi ya kumfikia mkulima mmoja mmoja basi angalau wangekuwa wanatuita wakulima tukaweza kukaa kikundi na wakaweza kutupatia elimu hiyo ya kilimo.

Mhe. Spika, bado wakulima tuna matatizo, wadudu wanashambulia katika mashamba, lakini hatuna wa kutusaidia maarifa. Utakuta mipunga inaingiliwa na viwavi jeshi, tangu mpunga unaanza kushambuliwa, lakini kwa kuwa unakosa mshauri wa kukupa ushauri basi mpaka shamba lile litamaliza kuliwa.

Pia tuna tatizo la kunguni nunda na utumiaji wa mbolea. Kwa sasa mbolea tunaishukuru serikali imepanga utaratibu mzuri tunapata mbolea, lakini bado utakuta hatuna ile elimu ya kuitumia ile mbolea, tunaweza hata tukaharibu hayo mazao yetu ambayo tumeyapata. Mhe. Spika, niwaombe sana wataalamu hawa washuke na kutupatia elimu hii ili kilimo hiki kiweze kutusaidia sisi wakulima.

Mhe. Spika, niende katika hii idara ya uhakika wa lishe. Kwa kweli Wizara hii ilipotuletea mswada ule, mimi nilisema kwa hakika tumeshapiga hatua moja kubwa. Lakini inaonekana serikali bado haijajipanga vizuri. Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja hapa aweze kuniambia juu ya suala hii, kwa sababu suala hili ni muhimu kuwa na uhakika wa chakula ni suala muhimu sana, na ukizingatia miaka hii tunayokwenda, kuna tatizo la mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi aniambie ni vipi amewahamasisha wakulima juu ya kupanda mbegu zile ambazo zinastahamili ukame, ili tuweze kuwa na uhakika wa kupata chakula hicho kwa kupanda mbegu zile ambazo zinavumilia ukame.

Pia Mhe. Waziri amewahamasisha vipi wakulima juu ya kutunza au kujiwekea akiba, ili wakati wowote tutakapopata tatizo tuwe na akiba ya chakula. Mhe. Spika, mimi hii ni mara ya pili nasema kuhusu hili. Wakati ule tulipokuwa tunaupitisha huu mswada nilisema sana kwenye huu uhakika wa lishe. Hivi sasa nimeona kuna utaratibu mahindi tunayavuna mabichi na

tunayachoma kwa wingi bila ya kuyaweka, na tungeyaanika mahindi halafu tukayakausha basi tungekuwa na chakula cha kutosha. Lakini mahindi yale yanavunwa mabichi na imekuwa ni biashara kubwa hatimaye wewe huwezi kula muhindi wa kuchoma ukasema tayari umerudi nyumbani labda unashiba, lakini muhindi ule ule ungeanikwa halafu ukasagwa unga ukapikiwa ugali basi ungeweza kusema kwamba tayari wewe una chakula. Mimi naomba sana serikali iangalie juu ya huu uhakika wa chakula, ni lazima tuweze kuwa na uhakika wa chakula kweli, vyenginevyo tutakuja kuadhirika.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni mdogo, nilitaka tu niungane na wenzangu katika kuchangia hotuba hii. Mhe. Spika, mimi binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100, lakini pamoja na uungwaji wa mkono huo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi aweze kunipatia haya majawabu ambayo nimemuuliza, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujaalia asubuhi hii kukutana tena kuendelea na shughuli zetu za wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jitihada kubwa wanayoiendeleza siku hadi siku ya kuendeleza mbele sekta hii ya kilimo kwa faida na maslahi ya nchi hii.

Mhe. Spika, jitihada hizi za watendaji wala hazitotuondoa tulipo, kama kwa makusudi serikali haijaamua sekta hii iwe na tija kwa wananchi wake. Mhe Spika, tukubali kwamba Zanzibar kama visiwa kuna haja kwa makusudi ya kuvitizama visiwa vyenyewe na ongezeko la watu, mahitaji ya ardhi na mahitaji yake, baada ya kuyaona hayo tuamue sasa, *kupanga ni kuchagua*, vyenginevyo tutaendelea kupitisha bajeti mwaka hadi mwaka, na siku moja vizazi vya nchi hii vitakuja kutusuta, ardhi hii kwa matumizi ya kilimo itakuwa ni tabu kubwa.

Mhe. Spika, rasilimali moja kubwa ya kilimo ni ardhi na halafu kuwe na rasilimali watu wakiwemo wataalamu, na humo tena yatazalika mengine mengi ya kukiendelezea hicho kilimo.

Mhe. Spika, nimpongeze pia Mhe. Waziri kwenye suala la makusanyo waliojiwekea mwaka uliopita wameweza kupindukia lengo. Lakini tunaposema Mhe. Spika, kwamba bado tunalo tatizo ni upande mzima wa fedha za maendeleo, yaani haya yanayozungumzwa ndani ya kitabu hichi. Kwa kweli kama fedha za maendeleo hazipo ama zinatolewa chini ya mataratjio basi zitabaki humu kwenye kitabu. Kwa mfano, mwaka uliopita

serikali imechangia asilimia 22 na waliotuchangia wametupa asilimia 30 na jibu tutalipata hapa.

Vile vile katika suala zima la kilimo Mhe. Spika tunahitaji utafiti. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, anieleze kule Pemba Kituo cha Utafiti wizara yake imekusudia ni mwaka gani kutakuwa na jina sahihi la kituo hicho. Kwa kweli kituo kitakachojulikanwa na kuonekanwa kwamba kweli sasa kuna Kituo cha Utafiti Kisiwani Pemba, na tukiacha jina lile tulilolizoea la Matangatuani kuna majengo, lakini ukweli wenyewe ni kufunika kombe mwanaharamu apite. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, ndani ya takwimu jana tulikuwa tunakusikia Mhe. Spika mwenyewe unakiri kwamba kuna mambo ndani ya Taasisi za Mifugo na Kilimo zimefanya vizuri zaidi Kisiwani Pemba, lakini kwa nini wizara hii ikadharau kiasi chote hicho hadi leo na kesho tuna miaka 50 Pemba hakuna Kituo cha Utafiti.

Jengine Mhe. Spika, niwapongeze watu wa Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa kazi nzuri wanayoifanya, wanatuzalishia vijana wazuri. Lakini uzuri huu wa vijana wanaotoka Chuo cha Kizimbani kuna haja sasa Serikali ya Mapinduzi Mhe. Spika, samahani kidogo ndani ya mchango wangu.

Sisi Wajumbe wako Mhe. Spika, huwa tunasema tunapokuwa na kazi hii hapa ndani basi ni vyema wale Viongozi Wakuu wa Shughuli za Serikali tuwe nao humu ndani, maana yake tunatoa ushauri na ukitupa macho kwenye viti hawapo wenyewe wala wanaowasaidia. Lakini baya zaidi wenzetu huwa tunawasikia kwamba shughuli zile leo atakuwa nazo mtu fulani na anatajwa Mhe. Waziri mmoja katika mawaziri, sasa angalau tuwe tunajua hili jasho tunalolitoa halipotei bure na Mhe. Spika, nakuomba sana katika hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, chuo hichi kinatoa vijana wenye taaluma ya kilimo lakini wakishatoka mategemeo ni ajira, sasa leo serikali ajira tayari kumeshajaa. Kwa hivyo, ni juu ya serikali sasa kutafuta ni namna gani vjana hawa watapata uwezo wa kujitegemea kutokana na taaluma waliyoipata kwenye chuo kile na hilo ni la serikali. Sasa kama tunasema serikali haipo tunamwambia nani?

Nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye Idara ya Misitu. Hawa wenzetu wanafanya kazi kubwa, tena nzuri lakini bado tatizo lipo. Tatizo ni namna gani mazingira yanavyochafuliwa na kuvurugwa. Mhe. Spika, tuna tatizo na hasara kubwa ambayo imetukabili na jambo hili serikali sijui

wanalichukulia vipi, lakini kizazi cha miaka 50 ijayo tukishashereheka sisi kesho hao ndio watakaokuja kutuuliza maswali na kushindwa kujibu.

Mhe. Spika, miche inayopandwa kwa mwaka hivi Mhe. Waziri hebu atuambie kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba idadi hii ya mwaka inayopandwa mwaka jana na mwaka juzi ni mingapi? Leo tunayo ambayo iko ardhini tena ni hai, maana isiwe ni kazi tu, kwamba idadi milioni moja miche ya mikarafuu, milioni tatu michenza na tunataka tujue iko mingapi leo ipo. Kwa hivyo, kama huu upandaji ni sambamba na uhai, basi tutie matumaini kwamba tunafanya kazi yenye malipo.

Sasa nije kwenye Idara ya Uhakika wa Chakula. Mhe. Spika Kauli Mbiu ni '*Kujitegemea kwa Uzalishaji wa Chakula'*. Lakini kuna kile kipindi kwenye *television* ambacho kinauliza Je, tutafika? Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba Idara hii ya Uhakika wa Chakula je, tutafika?

Mhe. Spika, nauliza swali hili bahati nzuri ni Waziri huyo anayekaimu wizara hii ndiye Waziri anayeshughulika na masuala ya maji. Kwa kweli alivyotuambia humu ndani kwamba hivi sasa tuna tishio kubwa la suala la maji ardhini. Sasa Idara hapa inatuonesha maeneo ya uchimbaji wa visima kwa ajili ya umwagiliaji. Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya leo ya tabia nchi na mengineyo na balaa za walimwengu hapa duniani ndio zinazoleta huo tabia nchi na mabadiliko yake.

Kwa hivyo, bila ya kuwa na umwagiliaji hatuna kilimo tusijidanganye Mhe. Spika, bila ya kuwa na misitu endelevu ya siku hadi siku hatuna kilimo, bila ya kuhifadhi mazingira kwa nguvu zetu zote hatuna kilimo. Sasa ni jitihada na mikakati ipi ya muda mfupi, wa kati na mferu wa serikali kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi? *(Makofi)*

Mhe. Spika, haya atujibu Mhe. Waziri mikakati ya serikali katika nyanja hizo tatu na tatizo lipo. Nadhani ni vyema tuwatumie masheha katika suala hili, na tukiacha zile shughuli zao za serikali walizozoea na hili kwa sababu wao ndio wako karibu na wananchi mbona mengine wanayaweza kuhusu kwenye misitu na uvurugaji wa mazingira isiwezekane kwa nini?

Vile vile kulikuwa na suala la kuvuna maji ya mvua. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aje atuambie sasa kwamba hili limefikia wapi na lipi limepangwa na serikali au limekwama huko serikali hadi leo kwamba hii naona hata kwenye kitabu halimo mwaka huu.

Kwa kweli maji ya mvua Mhe. Spika yamezua majanga makubwa mwaka huu, lakini yote baadaye yameishia baharini na Mhe. Waziri kwa sababu

analijua hili kwamba kuna maji mengi lakini yako chini ya ardhi, na bado hayajatusaidia hayo na kupata matumizi ya maji hayo ni kazi kubwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tatu.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nimekuona dakika zangu tano za mwisho.

Changamoto, Mhe. Spika hebu tufike mahala watu wazima wakisema wasikilizane na kukubaliana, ili kila siku kitabu hichi kinaandikwa uvamizi wa maeneo. Mhe. Spika, ukienda kuyatizama maeneo yanayovamiwa ni miongoni mwetu humu ndani na walioko maofisini hivi sasa na wala sio wale walala hoi na wale tunaokwenda kuwapiga magongo Darajani wale hawako huku. Kwa hivyo, hivi sasa tunamwambia nani maneno haya.

Kutokana na hali hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho kwamba maneno haya amekusudiwa nani. Hivi ni kweli Mhe. Spika anavamia mtu eneo halistahiki serikali haina uwezo wa kumwambia ondoka, ndipo pale tunasema kwamba mumeigeuza serikali ni shamba la bibi sasa kwa wenye madaraka yao na wanyonge wao aa! Hawana haki na wala haiwezekani Mhe. Spika.

Kwa kweli eneo tunalolitegemea kwa maisha ya watu akienda mtu tu akafanya anavyotaka na serikali ipo na haiwezekani, tunawaambia nini ambao hawana uwezo huo. Hali hii inaonesha kwamba tunajenga matabaka ya mabwana na wasiokuwa mabwana, na hii ni dhambi kubwa wanyonge na wenye nacho, ndicho kinachoendelea hivi sasa. Vile vile maeneo tunayoyategemea kwa ajili ya vyanzo vya maji ndio yanayoharibiwa, na serikali ipo Mhe. Spika, sasa kesho na kesho kutwa tutasema nini.

Mhe. Spika, la mwisho nakuomba nimeona ukarabati wa maghala.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umemalizika.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nakubali, isipokuwa nataka yalikuwa mangapi na hivi sasa tunayo hakiba kiasi gani. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante. Sasa nimuombe Mhe. Asha Abdu Haji na baadaye Mhe. Asha Bakari Makame.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa asubuhi hii na kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema asubuhi hii.

Vile vile napenda kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea hotuba hii.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwenye ukulima wa mpunga. Kwa kuwa wakulima wa mpunga wengi walilalamika kwa mbegu waliyopewa haikufumbua. Kwa hivyo, Mhe. Spika naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wale ambao hawakufaidika na mavuno yao, na wala hawakufikia malengo ya kupata chochote na kuweza kujikwamua na umasikini.

Mhe. Spika, naiomba wizara hii inapowapelekea mbegu wananchi au wakulima, basi kwanza lazima iifanyie utafiti ndipo wawapelekee wananchi au wakulima, kwa ajili ya kupanga. *(Makofi)*

Hata hivyo, mabwana shamba hawapiti kwa wakulima na kuwapa elimu yoyote. Kutokana na hali hiyo, ndipo pale wakulima wanapoharibikiwa na kutopata mavuno ya aina yoyote. *(Makofi)*

Kwa kuwa wameelimishwa wakulima 1,500 idadi hii kwa upande wa wakulima naona ni ndogo sana kutokana na kwamba wazanzibari wote ni wakulima. Je, idadi hii ya wakulima waliopatiwa mafunzo, ambapo ni 1,500 wa Pemba ni wangapi na Unguja ni wangapi? *(Makofi)*

Mhe. Spika, ufugaji wa nyuki wazanzibari wameitikia sana na hususan Wilaya ya Kusini. Kwa kweli kuhusu ufugaji wa nyuki ningeiomba serikali kupitia wizara iwaelimishe sana wanawake kuwapa elimu, ili na wao wajikwamue kimaisha na ufugaji wa nyuki.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu misitu. Mhe. Spika, serikali ilitushajihisha sana juu ya hifadhi ya misitu. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hifadhi ya misitu Wilaya ya Kusini Unguja sehemu ya Kajengwa wamejishajihisha sana na kuweka hifadhi ya misitu.

Jambo la kusikitisha hivi sasa hifadhi ile wako wenye nguvu ambao wanaitaka hifadhi ile kwa ajili ya kujenga Chuo cha Polisi na wanataka lazima wakijenge pale kwenye hifadhi ya misitu na wenyewe hawataki, wanawaambia kwamba watawapa sehemu mbadala. Lakini sasa wao kwa vile wana nguvu Afisi Talawa Wilaya ya Kusini anasema lazima tupate pale,

sababu gani inayopelekea lazima wapate pale na tayari wameshaambiwa kwamba hapa musijenge tutakupeni sehemu mbadala. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi anipe sababu ya kwamba lazima wapate eneo lile na wenyewe ambalo wameshaliweka ni Hifadhi ya Misitu. *(Makofi)*

Sasa nizungumzie kuhusu ukulima wa michungwa. Mhe. Spika, ukulima wa michungwa ni zao kubwa ambalo tumeliitikia hususan kwa wazanzibari. Kwa mfano, Kitogani, Makunduchi, Chwaka, Ndijani. Lakini zao lile halina soko na hata wadudu waharibifu ni wengi na ukienda wizarani watakwambia tumetoa mitego, lakini mitego ile haitoshi. Mhe. Spika, naiomba wizara ifanye kila jitihada iieneze mitego ile, ili waharibifu wale tuwatokomeze.

Mhe. Spika, ukulima wa ndimu Dongwe Wilaya ya Kusini Unguja. Kwa kweli Dongwe kuna ndimu ambazo hazina kiasi na ndimu zile bado hazina soko, hivi je serikali ina mpango gani wa kuwashajihisha tena wakulima wale na kuwapatia soko, pamoja na angalau usindikaji wa ndimu zile, kwa ajili ya kujikwamua na maisha yale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu maeneo kwa kusema kweli kuna maeneo ambayo yanahitajika kwa kilimo na mengine kwa ajili ya ujenzi. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba eneo lile ambalo linahitajika kwa kulima, basi serikali isijenge majumba na badala yake liwe kwa ajili ya kilimo tu na eneo ambalo halifai kwa kilimo basi serikali itoe eneo lile kwa kuruhusu kujenga. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naunga mkono hoja iwapo Mhe. Waziri atanijibu maswali yangu. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mchango wa Mhe. Mjumbe ni mzuri, isipokuwa alikuwa akisoma kinyume na utaratibu. Sasa kwa siku za usoni najua atajitahidi awe anachukua *point* anaielezea ndivyo inavyotakiwa. *(Makofi)*

Vile vile namshukuru kwa kutuokolea muda na sasa naomba nimkaribishe Mhe. Asha Bakari Makame na baadaye Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika hali ya afya njema pamoja na mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atufikishe tule Sikukuu kwa salama.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri …

Mhe. Spika: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, nakuomba tuwe pamoja kwenye kikao hichi.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote pamoja na watendaji mbali mbali ya wizara hii kwa jinsi walivyomsaidia Mhe. Waziri kwa hotuba hii. Vile vile nichukue fursa hii nimuombe Mwenyezi Mungu kwamba amjaalie Mhe. Waziri apate afya njema, ili ajumuike nasi katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwa sababu wenzangu wengi wamegusia mambo tofauti.

Hata hivyo, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa dhamira yake ya kugawa wizara hii, kwa sababu wizara hii ilikuwa ni wizara kubwa, ambapo ilikuwa inaitwa Wizara ya Kilimo, Uvuvi, Mazingira pamoja na mambo mengine, ambayo yanakubaliana kuwa pamoja.

Lakini Mhe. Rais aliona kuna haja ya kugawa wizara hizi mbili na kuzifanya wizara mbili; na moja ni Wizara Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Dhamira yake Mhe. Spika, ni kwamba kilimo tunaelewe kwamba ni uti wa mgongo, na Mhe. Rais alionesha dhamira nzuri sana na tunaona kwenye *television* namna mbegu za mipunga na tukaona Kizimbani kule Chuo cha Utafiti, dhamira yake kubwa Mhe. Rais ni kuona kwamba kweli wizara hii ni wizara muhimu katika lishe ya wananchi wa taifa hili.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla kupitia kwako Mhe. Spika, kwa dhamira hiyo kwa nini wizara hii haikupewa kipaumbele cha hali ya juu, ili kuona kwamba ni kweli kilimo ni uti wa mgongo, na kilimo ni moja wapo ambalo suala la kusaidia watu wa sehemu mbali mbali, kuona kwamba tunajitosheleza kwa kilimo chetu sisi wenyewe hapa Zanzibar.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, sasa nije kwenye ukurasa wa 38 wa kitabu hichi, na hapa kwenye ukurasa huu naona mambo yako shaghala baghala. Mhe. Spika, hivi kweli tunavyoelewa visiwa hivi viwili, yaani Kisiwa cha Unguja na Kisiwa cha Pemba, kwamba visiwa vyote viwili ni *fertile Islands*.

Sasa kweli tunashindwa na niunge mkono suala alilolisema Mhe. Asaa Othman Hamad, kwamba kulikuwa na dhamira serikali ijenge Kituo cha Utafiti Pemba, leo tunafikia miaka 49 kituo hichi namuomba Mhe. Waziri

kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba aje anieleze kimefikia wapi? Mhe. Spika, kama sikupata jawabu nzuri basi mimi nitakuwa bado sijakubaliana na kuiunga mkono hoja hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. *(Makofi)*

Vile vile ninasikitishwa kwamba hivi kweli kitabu chote hichi kiandike kurasa mbili na nusu tu Ofisi Kuu Pemba, wakati na kule ni kisiwa ambacho kina ardhi nzuri ya ukulima. Kwa kweli mazao mengi Mhe. Spika tukitaka tusitake yanatoka Pemba ndio yanayotuhifadhia sisi huku kama vile viazi, mihogo na ukija ndizi ndio barabara, embe, mabungo na leo tunaandika kurasa mbili na nusu katika bajeti nimesikitishwa Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anieleze ilikuwaje mpaka tukaandika kurasa mbili na nusu tu kwa ajili ya Kisiwa cha Pemba, wakati ni kisiwa kinachozalisha mazao mengi sana katika ukulima. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu niingie katika suala zima. Mhe. Spika, Kizimbani ni kituo cha mfano, lakini niiombe sana wizara hii kwamba wale wanafunzi ambao wanasoma wakati mwengine huwa kuna matatizo, na binadamu analipa yeye mwenyewe kwa kutaka kujua kuisaidia nchi yake.

Lakini binadamu yule akikosa kulipa zile fedha za ada basi anaambiwa asifanye mtihani na wala hili si jambo la busara, kwa sababu mtu ameshatimiza masharti yote, amelipa kidogo na kama hajamaliza anaambiwa hana ruhusa ya kufanya mtihani na yule ni masikini anajitafutia masomo, ili baadaye aje kuisaidia nchi yake.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kuwe na utaratibu maalum ambao utawawezesha wanafunzi hawa kuweza kupata masomo yao kwa uhakika.

Mhe. Spika, kubwa zaidi wale wanafunzi wanaosomeshwa na wale walimu wanaosomesha wanafunzi, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho, kwamba kuna vitu gani ambavyo vinawalinda wao katika maisha yao kutokana na kutumia *chemicals* zile ambazo wanafundishia kwenye Chuo chetu hichi cha Kizimbani.

Kwa kweli huko nyuma tulipata malalamiko, na sasa sijui mara hii wamewafanya vipi mpaka wakaweza kuwasaidia, ili kuhakikisha kwamba na wao hawafikwi na madhara makubwa yanayotokana na *chemicals* zile bila ya kupewa vifaa vya kuvaa, ili kuweza kuwanusuru na afya yao.

Mwisho Mhe. Spika, niseme tu niwaombe sana Wizara hii ya Kilimo na Maliasili kwamba warudi wakafanye utafiti upya, kwa sababu hii wizara

ilikuwa imechanganyishwa na mambo mengi, ili mwakani Mwenyezi Mungu akitujaalia akitupa uhai na uzima tukija hapa basi tujue kwamba kweli kilimo ni uti wa mgongo.

Mhe. Spika, uvamizi wenzangu wameshazungumza na nchi yetu ni ndogo tutakuja kujikuta hapa hata ile sehemu ya kukaa sisi wenyewe hakuna na pa kulima hatuna, isipokuwa tutabakia tunasongamana bila ya sababu yoyote.

Baada ya kusema hayo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kwamba suala la kuotesha maua hapa Zanzibar. Mhe. Spika, nadhani kipindi kilichopita tulilizungumza sana suala hili, hebu aje atueleze suala hili limefikia wapi na kuna utaratibu gani ambao tutautumia.

Sasa baada ya kusema hayo Mhe. Spika mimi mpaka aje anieleze Mhe. Waziri kuhusu habari ya Chuo cha Utafiti Pemba limefikia wapi suala hili kwa sababu hivi sasa ni miaka 49, na wakati Pemba inazalisha mazao mengine sana ambayo yanasaidia wananchi kwa jumla, basi hapo ndipo nitaweza kuipitisha bajeti hii.

Baada ya kusema hayo ninakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na wewe pia umetuokolea muda tunakushukuru sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Salim Abdalla Hamad na baadaye Mhe. Mussa Ali Hassan.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii fupi ya kuchangia kidogo katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa umuhimu wa wizara hii tumuombe Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili afya njema na amuondolee matatizo, na *inshaallah* katika siku zinazofuata kwa sababu ya ubingwa wake aweze kuwasilisha mwenyewe shughuli zake hapa. *(Makofi)*

Pili Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo ni muhimu sana na ni moja kati ya wizara muhimu kabisa katika wizara tulizonazo, kwa sababu inagusa viumbe na maisha yao moja kwa moja.

Kwa kweli wizara hii Mhe. Spika, ningeomba kutoa tanbihi hasa kwa sababu ni yenye wataalamu wengi sana. Wizara hii ya Zanzibar ni kama tunavyoona ni wizara ya hali ya joto ya kiasi na kadhalika. Zanzibar kwa bahati nzuri imebarikiwa miti ya aina inaota, miti mikubwa na miti midogo. Kama kweli kungekuwa na tahadhari ya aina yake katika umiliki wa ardhi na uendeshaji

wa kilimo katika hali hasa inayotakiwa, naamini Zanzibar hii leo tungekuwa matajiri wa kilimo kinachokidhi mahitaji yetu ya lazima na vile vile cha ziada kwa kuuza nchi za nje na kuweka hakiba.

Lakini kwa sababu *Zanzibar ni njema kila atakaye aje*, nchi imeingiliwa na watu wengi, ardhi ya kilimo ndiyo inayohamiwa, ndiyo inayojengwa na kila siku zikiendelea idadi ya watu inaongezeka, ardhi ya kilimo inapungua. Kwa hivyo wizara hii kwa wakati huu ilionao, ina umuhimu wa kutumia utaalamu wake wa mwisho kuona kuwa hiyo ardhi ndogo inayobakia inasarifiwa vilivyo, ili wananchi wapate chakula cha kujiendeshea maisha na kuinusuru nchi hii kuagizishia chakula na mambo mengine yanayohusiana na hayo kutoka nchi za nje ili uchumi wetu uweze kukua.

Pia kwa sababu tumeona na tumeshuhudia wamekuja wenzetu wawekezaji na wamehamia katika sehemu za mawe, na kila walipohamia na kuweka hoteli yao wamepafanya pamekuwa pana rutba na miti ya aina kwa aina inaota. Lakini sisi sehemu yote ile tunaiacha kama ilivyo tukisingizia tunaendeleza ufugaji wa paa.

Naishauri Wizara kwa sababu tuna eneo kubwa Makaani hatulitumii na kipo kilimo kinaota vizuri Makaani, kwa hivyo waanze mkakati mpya wa wizara kuweza kutumia maeneo yale ili kuweza kuzalisha chakula kwa wingi badala ya kutegemea kijisehemu hichi kidogo ambacho kila mtu ndio anachohamia.

Jengine kabla sijaja kwenye kitabu vile vile naomba kuieleza wizara kuwa kuna matatizo ya tabia nchi. Tabia nchi imesababisha matatizo makubwa sana katika nchi zote duniani, kutokana na shughuli za maendeleo zinazofanywa na nchi zinazoendelea. Kwa sababu ya tabia nchi kunakuwa na ongezeko la joto katika nchi zote. Hili linasababisha mfumo mzima wa maisha ya miti ya asili iliyopo na ile inayofanyiwa utafiti katika nchi. Kwa sababu ya athari ya tabia nchi hakuna mvua za uhakika. Yaani hali ya mvua haina miongo maalum, haitabiriki kama zamani kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi, bahari yetu imepanda juu na baadhi ya sehemu ya ardhi hii tayari imeshachukuliwa na bahari. Kwa sababu tabia nchi kuna ongezeko kubwa sana la hewa mpaka *carbon dioxide* ambalo linaleta matatizo katika mazingira.

Hivyo basi yote haya pia yanachangia kupambana na juhudi kubwa ya Wizara katika kuimarisha kilimo. Ushauri wangu kwa sababu Wizara hii ni yenye wataalamu waone kuwa kuna tabia nchi hii ambayo inaleta matatizo kama hayo, waweze kusoma na kujua pakitokea haya kwa hivyo huku tunapata athari, ili hayo mazao wenyewe waliokuwa wanavumbua ambayo ni yenye tija pia wayaingize katika mpango huo ili yaweze kukua, kumea na kuweza

kustawi na kadhalika kutokana na hali ya mabadiliko ya hali ya hewa inavyokwenda.

Pia kwa vile najua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa makusudi kwa kuona athari ya tabia nchi wamewasiliana na nchi kadhaa kuna misaada imetolewa, kuna ushauri umetolewa katika kupambana na hali hii, na moja katika ushauri ni kupanda miti kwa wingi.

Mhe. Spika, kwa sababu ya umasikini wetu wananchi wanajiendeshea maisha kwa kukata miti ovyo, ambayo ni athari kubwa sana. Anakata miti lakini anasababisha joto kuongezeka, anakata miti anasababisha mvua kukimbia, anasababisha upepo kuongezeka, na hata ardhi kukauka. Ardhi yote inayolimwa kwa *irrigation* ardhi kavu, matokeo yake huwa haizalishi kabisa na mabadiliko tunayaona. Kwa hivyo wizara itumie taaluma yake kwa kupambana na haya ili tuweze kufika huko tunakokwenda.

Huo hi ushauri wangu, niliposema kupanda miti kwa wingi ninazungumza kitu kinaitwa hewa ukaa, tujue kwamba miti inavyofanya chakula chake, tofauti na sisi. Miti inafanya chakula chake wenyewe, inatumia hewa hii ukaa pamoja na maji yanayovutwa kwenye ardhi. Muangaza wa jua unasababisha kupatikana chakula kinachoenea katika nchi ambacho huwa ni chakula chetu na kadhalika. Kwa hivyo miti inapunguza hii hewa ukaa kwa wingi, kwa hivyo kuipanda ni kuleta rutba ya mazingira na kufanya mambo haya kwenda vizuri kama yanavyotakiwa.

La mwisho katika hili ni kuwa Mwenyezi Mungu alivyoumba ardhi hii aliumba na mazingira yake na akaiumba miti, akawaumba wanyama, yote inazaana lakini ni michache inayomea. Hii kuna sheria inaitwa *natural selection* ambayo aliitoa kama ingelikuwa watu wote wanaozaliwa wanapona, samaki wote wanapona na miti yote inapona ingelikuwa hakuna pa kukaa na nchi yetu ingelikuwa ni msitu. Lakini ni michache inayobakia kwa sababu ndiyo inayokuwa na sifa za kuweza kustahamili. Sasa wenzetu wanafanya utafiti wa kuweka mbegu bora, tunajua kuwa Mwenyezi Mungu keshaweka mambo ya asili hapa, tusije tukaweka mbegu bora ikaja ikawa haikuwa endelevu, sababu yake tukaja tukafikwa na hasara kubwa sana.

Naomba utafiti wenu wataalamu wajue kuwa kuna hiyo *natural selection*, na hayo ni mambo ambayo kayaweka mwenyewe Mwenyezi Mungu ndio tukaona kuna miti mpaka leo inaendelea na kuna mingine haiwezi kuendelea.

Halafu tukija katika kitabu Mhe. Spika, kwa haraka haraka nikianza kifungu Nam. 1.11 ukurasa wa 3 kinasema kuwa "Sekta ya kilimo na Maliasili bado inaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi Zanzibar". Hilo nakubaliana

nalo na sekta hizi zinatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha kwa kuwa na uhakika wa chakula na lishe kwa walio wengi wa mijini na vijijini. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 sekta hii ilichangia asilimia 30.2 ya pato la taifa. Nawapongeza kwa hilo na pia inakadiriwa kuwa zaidi ya silimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hii kwa mapato na ajira.

Mhe. Spika, kitabu kinasema katika mwaka huu wa fedha 2012/2013, ukuaji wa sekta hii ya kilimo umepungua kwa asilimia 1.3 yaani kutoka asilimia 2.7 katika mwaka uliopita nyuma. Hali hii inatokana na ukame na kupungua kwa maeneo yaliyokuwa ya kilimo kwa baadhi ya maeneo makuu ya chakula ukiwemo muhogo, ndizi pamoja na mahindi. Alivyoeleza mapungufu ni kama haya yafuatayo.

Mhe. Spika, katika mazao hayo tukianza na muhogo mwaka wa 2011/2012 ilikuwa ni tani 273342 na mwaka 2012/2013 ni tani 81270, yaani kiwango kilicholimwa ni asilimia 70.3 na mapungufu ni asilimia 29.7 hii ni hali mbaya sana.

Tukija kwa ndizi nyuma ilikuwa ni tani 1, 10250. Mwaka 2012/2013 ilikuwa ni tani 97934.5. Kwa hivyo kilimo hichi kililimwa kwa asilimia 88.83 na kulikuwa na upungufu wa asilimia 11.17.

Tukija kwenye mpunga ni tani 23702 na mwaka huu 2012/2013 ilikuwa ni tani 6372.1. Hali ya ukulima ilikuwa na tija asilimia 26.89 ni hali mbaya, na mapungufu yalikuwa ni 73.11. Sasa asilimia 11.17 na mpunga ambao ndio nataka niuzungumze vyengine naviwacha kwa sababu ya wakati, ulilimwa tani 23702 mwaka 2011/2012 lakini kulilimwa tani 6572.21 katika mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika: Unazo dakika 2 kumaliza hotuba yako.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Haya, ni asilimia 26.89 ni mapungufu makubwa sana. Lakini katika hichi kitabu Mhe. Spika, ameeleza kuwa taarifa za hali ya hewa katika kipindi cha miaka 2012/2013 inaweza kutia moyo hasa kwa kilimo cha mpunga wa kutegema mvua. Takwimu zinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la mvua za masika mwaka 2011/2012, zimenyesha zaidi ya wastani wa kila mwaka.

Hali hii imeimarisha kwa kiasi kikubwa ukulima wa mpunga kwa kutegemea mvua ambapo, sehemu kubwa ya kilimo hicho kimeimarika vizuri na kuleta matumaini ya kupata mavuno mazuri. Kutokana na hali hiyo kwa msimu wa 2012/2013 mavuno yamekadiriwa kufikia zaidi ya tani 30,000. Sasa huku

wamesema kilimo kimekuwa, lakini huku wamesema kilimo kimepungua sana. Kwa hivyo hapa naomba maelezo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati niseme kuwa Wizara hii ni muhimu. Lakini pia kuna jambo ambalo hakulizungumza wenzetu wa Wizara ya Mifugo wanajitahidi kufanya *selecting breeding* kutafuta mbegu mpya ambazo zitatusaidia, lakini humu haikutiwa. Sikuona sababu kwa nini hawakuhimiza mambo yale ya *reproduction* ili kupata mbegu mpya na kupata kizazi kipya.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa nakushukuru.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mheshimiwa na mimi nakushukuru japo kuwa sijamaliza.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kuchangia bajeti hii pamoja na kumshukuru Waziri wa wizara hii kwa shughuli zake nzuri anazozishughulikia pamoja na watendaji wake.

Kwanza kwa leo sina mengi sana ya kuchangia na nianze kwa kuzungumzia sehemu zetu za kilimo zinazokuwa hazifiki trekta kwa wakati. Mhe. Spika, hivi sasa tuna matatizo makubwa katika mabonde yetu ya mpunga kutokana na hali ya kilimo kwamba hatulimi kwa wakati. Sina budi kumsisitiza Mhe. Waziri ili kumpa mawazo ya shughuli zake za kazi, ili aweze kushughulikia wakulima wa matrekta ili waweze kuwahudumia wananchi wetu kwa wakati, ili kuweza kupata mazao kwa wakati unaotakiwa.

Hivi sasa tuna matatizo katika mabonde yetu ya mpunga hasa Cheju na upande wa Mwera katika Jimbo langu la Koani. Matrekta hayafiki kwa wakati hivyo uzalishaji wetu unakuwa ni mdogo sana, hasa katika kilimo cha mpunga. Ningeshauri kwamba matrekta yaweze kuchekiwa ili wakati wa kilimo yaweze kulima kwa wakati.

Wakati mwingi Mhe. Waziri anapigwa changa la macho kuambiwa tuna trekta 50 kumbe trekta pale zipo tano tu. Namshauri Mhe. Waziri aweze kufika mabondeni kuweza kuchunguza kweli yale matrekta 50 yapo na tarehe ya kilimo ikifika Mhe. Waziri ahakikishe matrekta yale yanalima kwa wakati. Utakuta mabonde mengi wakati tayari kulima lakini utakuta matrekta yale hayafiki, na sehemu nyingi mabondeni utakuta watu wanalima kwa majembe ya mkono ambayo yameshapitwa na wakati kwa kulima sehemu hizo. Mhe.

Waziri angelijitahidi sana kusisitiza sehemu zake ili matrekta yafike kwa wakati.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nachangia ukurasa wa 4 kuhusu hali ya ushukaji wa uzalishaji katika sehemu zetu za kilimo. Kwa kweli uzalishaji hivi sasa kama nilivyosema katika ukurasa huu mwaka huu wa kilimo mambo mengi yameshuka hasa kilimo cha muhogo, viazi, pamoja na migomba. Nisemee zaidi katika Jimbo langu la Koani. Hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa vitu kama hivyo na wakati hatukuzoea sisi kununua katika masoko vitu hivi, mara nyingi huwa tunapata mashambani kwetu. Ukweli vitu hivi vimepungua hasa kutokana na wanyama waharibifu ambao kima na wengine, hao ni waharibifu zaidi, lakini tumeshawapatia zana zao za kuwashambulia, tunawashambulia kwa magobore tunawaweza.

Kuna matatizo ya wanyama waharibifu lakini sio waharibifu ni wanyama ambao tunawafuga, kama ng'ombe na mbuzi kwa kweli ndio wanaotutatiza katika majimbo yetu. Hivi sasa Mhe. Spika, ni bora Mhe. Waziri ahakikishwe kwamba wanyama hawa wamewekewa sheria maalum ili wakulima wetu waweze kulima kwa wakati na waweze kupata mazao. Utakuja katika jimbo langu ng'ombe na mbuzi wanaharibu sana vipando vya wananchi, utakuta kwamba wanyama hawa hajapangiwa sheria yoyote ili kupata adhabu kuanzia mnyama mwenyewe kama ng'ombe au mbuzi au mwenyewe mfugaji; ambaye anafuga wanyama hawa ambao anawaachia ovyo kuharibu mazao ya wananchi.

Nimshauri Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze kwamba ni lini ataweza kuweka sheria ya ng'ombe na mbuzi wanapoharibu mazao ya wananchi wakaweza kuchukuliwa hatua. Mhe. Waziri utakapofika hapa kwamba hukuweza kunipa tarehe, mwezi au mwaka wa kuweza kuweka sheria hii, kwa kweli mimi nitaondoa shilingi yangu katika bajeti yako.

Mhe. Spika, hivi sasa utaona mazao mengi tumefanikiwa kulima hasa katika jimbo langu la Koani kama ulivyoona. Mananasi yameweza kuzidi kutoka elfu 3300 mpaka 12.5 ambapo ukulima huu umezidi kutokana na kwamba sheria nzuri ingeliwekwa kwa kila Jimbo ingeweza kuzalisha mazao ambayo wanaweza kuyalima. Namshauri Mhe. Waziri afanye kwa makusudi au achague kila Mkoa aweze kuupa nafasi ya kilimo kinatoa zaidi ili kunufaisha katika nchi yetu. Mkoa wangu wa Kusini kama Mhe. Waziri akiweza kunisaidia kwamba Mkoa wa Kusini mzima akaweza kuupa nafasi ya kulima chooko na mbaazi au mtama na mawele, mimi nafikiri Zanzibar tunaweza tukailisha kwa vitu hivyo bila ya kununua nchi za nje. Jimbo la Koani akatoa nafasi ya kulima mananasi pamoja na shokishoki ambazo zinatoka kwa wingi, mimi sifikirii kama tutaagiza katika mji mwengine kuweza kupata vitu hivyo.

Namshauri Waziri ajitahidi kwa wazi kwamba wananchi aweze kuwapangia bajeti kwamba atanunua mbaazi bei gani, atanunua mtama bei gani, kama vile alivyoweza kuweka katika mazao ya karafuu kuweza kuwatajia wananchi pesa za kuweza kununua mazao hayo, wananchi wanaweza kufanya bidii kuyalima mazao ambayo yanatoka katika mkoa wao. Kwa kweli Mhe. Spika, nisiwe na mengi sana na wakati mwingi kuupoteza. Hayo naomba Mhe. Waziri atakapokuja aweze kunisaidia ni lini wananchi ataweza kuwapa bajeti ya kuweza kununua mbaazi bei gani, mtama pamoja na vitu vyengine ambavyo vinaweza kuwekeka na vinakauka kama karafuu ili wananchi wetu wakahamasika kuweza kulima mazao hayo.

Ahsante sana Mhe. Waziri na Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii, sina mengi zaidi isipokuwa nitaunga mkono bajeti hii pindi Mhe. Waziri atakaponijibu masuala hayo. Ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, nianze kwenye kilimo.

Mhe. Spika, ukiangalia asilimia kubwa ya Wazanzibari, ni wakulima ambao hutumia nguvu zao kwa ajili ya kilimo, ambapo wafanyakazi wa serikali na wafanyakazi wengine hutegemea sana kilimo hicho au hutegemea mazao hayo ya wakulima kuwafikia wao. Lakini je, nimuulize Mhe. Waziri, serikali kwa nini bado haijajipanga kuwasaidia wakulima.

Kwa mfano kuwapatia zana za kulimia ili kupungua kulima kwa mikono na kutumia nguvu za kifua, ili kuwapatia zana za kilimo kama vile mbegu za kutosha na kuwapatia mbolea wananchi hawa au wakulima hawa ni jambo ambalo litawasaidia wananchi wetu. Pia, nimuombe Mhe. Waziri au niwaombe wakulima na Mhe. Waziri alitilie sana mkazo suala hili la wakulima wetu, wasiache kutumia mbegu zao za asili kama vile ringa, kinazini, sotea, mvivu kwa nongwa, kinuke na kadhalika. Ukiangalia mbegu hizi Mhe. Spika, ni mbegu ambazo zinazaa sana na zinaleta tija kwa wakulima wetu.

Vile vile Mhe. Spika, niwaombe wakulima wetu wasiache kuzitumia mbegu za muhogo kama vile ndege, mbopwe, majoka, mwari, Jumakali, na kadhalika, mbegu hizi Mhe. Spika, ni mbegu ambazo zinazaa sana na muhogo wake huwa ni mtamu zaidi. Naomba na hili Mhe. Waziri alitilie mkazo zaidi kwa wakulima wetu.

Mhe. Spika, nije katika Chuo cha Kizimbani, ukurasa wa 26 kifungu cha 7(3) kinasema kwamba

"Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo kimetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Mafunzo yalitolewa kwa wanafunzi 210 kwa upande wa ngazi ya Diploma ni wanafunzi 40, wanaume wakiwa ni 21 na wanawake wakiwa ni 28."

Kwanza hapa Mhe. Spika, nikipongeze Chuo kwa kuzingatia jinsia. Mhe. Spika, pamoja na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 49 kwa ngazi ya diploma ya kilimo Mhe. Spika, bado haijapewa umuhimu diploma kama inavyopewa umuhimu diploma nyengine. Ipo haja kuiboresha diploma ili wananchi wa Bara na Zanzibar waweze kulingana kitaaluma.

Mhe. Spika, vile vile kuna tatizo la kutowaajiri wanafunzi pale wanapohitimu mafunzo yao na kukaa bila ya kupata ajira. Je, Mhe. Waziri hili huoni kama linawarejesha nyuma wanafunzi hawa na pia linaweza kufanya Chuo kupoteza hadhi yake?

Mhe. Spika, nije katika tatizo la kuwaajiri wafanyakazi yaani mabwana shamba na mabibi shamba. Mabibi shamba hupelekwa Pemba na mabwana shamba ni tatizo kubwa sana. Wakaazi wa Unguja wanapofika Pemba huwa wanafanya kazi zao kwa muda na baadaye hurejea Unguja. Hili Mhe. Waziri alione hatimaye huiacha Pemba kukosa mabwana shamba na mabibi shamba. Namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie ili alipe kipaumbele kwa Pemba awapeleke mabibi shamba ambao watakuwepo kule na kufanya kazi zao kule.

Mhe. Spika, nije katika Chuo hicho hicho. Chuo kina ukosefu wa Ofisi yake ya kilimo ndani ya Wilaya ya Micheweni, ambapo wafanyakazi wa kilimo hufanya kazi zao ndani ya kituo cha Mifugo. Je, Mhe. Waziri unalielewa hilo? Kama unalielewa kwa nini iwe hivyo. Pia Chuo hicho hicho kuna tatizo la maji. Wanafunzi huwa wanapata tabu sana pale, hutumia maji ambayo yana athari kwa afya zao. Wengi pale hutokewa na matumbo ya kuharisha, hutokewa na matatizo mengine. Naomba Mhe. Waziri naomba hili ulielewe.

Vile vile kuna tatizo la ukosefu wa usafiri. Mhe. Spika, kipindi kimoja pale nilikwenda baada ya kupita pale njiani tukamkuta mfanyakazi yaani mlinzi kaanguka pale na tulikuwa mimi na Mhe. Abdalla wa Mkoani. Kwa bahati yule alikuwa tayari siku yake imeshafika na ahadi imeshafika hilo siwezi nikalitilia nguvu kwamba ni ahadi yake. Lakini tatizo la gari lilikuwa ni kubwa, kwa bahati wakaniomba nimchukue nimpeleke, lakini kwa bahati tunaye mtaalamu pale kumkamata mtu yule tayari ameshafariki. Namuomba Mhe. Waziri tatizo la gari katika Chuo cha Kizimbani aliangalie sana kwa sababu kuna watoto wetu, kuna wafanyakazi wetu, na kuna watu wengine ambao hukaa pale.

Mhe. Spika, jengine hili la wafanyakazi wana mizunguko ya *field*, hili ni moja kati ya somo la vitendo. Lakini baadhi yao hupangiwa sehemu mbali kwa mfano kama Kisiwa cha Pemba au wengine kisiwa cha Unguja. Watoto wale huwa hawasaidiwi wala huwa hawalipwi na wengine huwa ni masikini. Mhe. Spika, hili aliangalie kwa sababu usafiri huwa ni mgumu na hawana usafiri wa kusafiri na wala nauli huwa hawana. Je, Mhe. Waziri wizara yako imejipanga vipi kuhusu suala hili?

Mhe. Spika, mwisho nije katika Idara ya Misitu, hili linanihusu zaidi na mimi kunipa taarifa zao wananchi wangu ambao walikuwepo Kangani Kuu watu hao ni kikundi ambacho kimekaa cha uatikaji wa miche ya mikarafuu. Lakini kwa bahati ilikwenda Wizara ya Kilimo au Idara ya Kilimo kwenda pale kutaka mikarafuu, watu wale wakawekewa mikarafuu kwa ajili ya kununuliwa, haki hii leo Mhe. Spika, idara ile haijapita kuwalipa wala haijawapelekea salamu zozote. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili, kwa sababu wale ni watu waliojiajiri na ambao wanategemea ajira zao zitoke katika mazao yao.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili alione kwamba kuwachukulia miche yao watu kama wale serikali haioni aibu na pia kuwa haiwalipi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri alitambue hilo ili awalipe pesa zao zile mara moja kama iwezekanavyo. Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi katika wakati wa majeruhi. Kwa kweli nilikuwa nimeanza kutoa mchango wangu kwa njia nyengine, lakini kwa sababu nimepata nafasi itabidi nichangie katika njia hii ya kawaida.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi hii kusimama mbele ya Baraza hili kutoa mawazo yangu mafupi, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Kwa kweli nilikuwa nimeshakata tamaa, jana sikupata, leo nilikuwa nimeshakosa, lakini kwa sababu wenzangu wamekwenda vizuri nimepata nafasi.

Mhe. Spika, nimpongeze Waziri na watendaji wake jinsi walivyojiandaa katika bajeti yao hii, ingawaje vitabu vyetu vingi huwa vinajirudia. Cha mwaka jana na cha mwaka huu, hakuna tofauti yoyote kubwa, takriban mambo yao huwa ndio yale yale.

Mhe. Spika, nianze na hili waliotuonesha kuwa upungufu wa chakula katika mwaka huu wa 2012/2013 ukilinganisha na 2011/2012. Na wizara imetoa sababu zake kadhaa ikiwemo ukame na mambo mengi mbali mbali. Lakini pia pamoja na sababu hizo, sababu nyengine ni upungufu au uchache wa

mabwana na mabibi shamba katika maeneo yetu mbali mbali kutoa elimu kwa wakulima.

Mhe. Spika, bado wakulima wetu tunalima vile alivyokuwa akilima babu na bibi huko zamani, kilimo chetu bado hakijabadilika tunatumia jembe la mkono. Ukulima wa namna hii kwa kweli hatutofika popote, tunasema huu ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Sasa kama tutaendelea kuwa tujitegemee kwa chakula kwa kutumia ukulima wetu tulionao kwa kweli tutachelewa kidogo kama tutafika, ingebidi tubadilike tutumie ukulima wa kisasa ili tuondoke hapa tulipo twende mbele.

Mhe. Spika, kwa upande wa wakulima wa mpunga bila ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji, bila ya sehemu kubwa kutumia matrekta, kwa kweli hatutokwamuka. Mwanaadamu amevumbua mashine kufanyia kazi katika sehemu mbali mbali ili kumrahisishia kazi zake. Kwenye kilimo trekta ni mojawapo ambalo linamsaidia mwanaadamu kufanya kazi kubwa kwa muda mdogo, lakini lengo la kutuwezesha sote wakulima kufanya hivyo halijafikiwa. Kwa hivyo serikali ingejipinda kuhakikisha kuwa tunafika hapo ili wakulima wetu wakwamuke na hiki kijembe kongoroka.

Na kwa kuwa mpaka leo sehemu kubwa ya kilimo chao mpunga tunategemea mvua ambazo miongo ya nchi hii imebadilika. Wakati wa nyuma kidogo kipindi cha hivi sasa cha Juni, Julai, Agosti ingekuwa mvua ndogo ndogo za mchoo lakini leo hazipo. Mvua za vuli zimepungua halkadhalika na mvua za mwaka, kwa hivyo kulima kwa kutegemea mvua tutachelewa mno. Kwa hivyo ili tuendelee kwenye kilimo ni vyema yale mabonde ambayo yanaweza kufanywa miundombinu ya umwagiliaji, yatafanyiwa ili tuweze kupata mpunga kwa wingi.

Mhe. Spika, mimi katika Jimbo langu la Mtambile liko bonde moja Mtambile ambalo wanaliita bonde la Mtungi, wengine wanaliita Makigini hili limetayarishwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Miundombinu yote imekamilika, kisima kimechimbwa, maji yamo ya kutosha kwenye kumwagilia, lakini jambo lililobakia la Wizara ya Kilimo ni kisima kile kukipatia mashine kikatiwa umeme ili bonde liweze kutumika. Ningemuomba Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na kwa kuwa yeye ni Kaimu na pia ni Waziri anayehusika na mambo ya Umeme, aunganishe kilimo chake anavyokaimu na uwaziri wake wa mambo ya umeme ili bonde langu hili alipatie huu umeme mwaka huu ili bonde liweze kutumika. Mwaka jana watu wanatoka na majembe kwenda kuipekua ile misingi yote kuwa hawataki tena serikali inawadanganya. Kwa bahati kuna watu waliotumia busara wakazuia ndio mpaka leo wamekaa midomo wazi wanangojea ni lini serikali itakamilisha kuwapatia umeme pale ili lile bonde liweze kutumika.

Mhe. Spika, pesa nyingi zilitumika za TASAF nadhani kipindi hiki kilichopita imeingiza kama milioni 44 kwa matayarisho ya lile bonde, sasa pesa hizi zisipotee bure zilete tija, lile bonde kukaa vile hizi pesa hazina tija yoyote. Ningeomba kwa hivyo Mhe. Waziri alione hili na avae buti, afunge mkaja ahakikishe kuwa hili bonde linapata umeme liweze kutumika.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanaadamu anatumia mashine ili kufanya kazi kubwa kwa muda mdogo. Zamani sisi wakati wa mavuno tulikuwa tunatumia kinu na mchi kutwanga, leo watu wamevumbua mashine za kukobolea, watu hawatwangi tena kwa mchi na kinu, wanakoboa kwa mashine. Kwa hivyo muda mfupi anatwanga pishi chungunzima kutumia mkono kutia mpunga kwenye kinu akatwanga hivi anachukua muda mrefu. Kwa hivyo lengo la mashine ni kumrahisishia mwananchi au mwanaadamu kufanya kazi kubwa kwa muda mfupi na kwa ufanisi zaidi. Hasa hapa kuna tatizo kubwa juu ya uharibifu wa mazingira linalotokana na hii misumeno inayoitwa misumeno ya moto.

Sasa misumeno ya moto ni moja katika mashine ninasikia mkata mbao hukata miti mingi kwa muda mfupi na kutoa mbao nyingi, lakini matokeo yake anaharibu mazingira, lakini bado tunataka mazingira yawepo lakini halikadhalika kwa sababu tunajenga tunahitaji milango na madirisha na mambo mengineyo yatokanayo na miti. Sasa hawa wenye misumeno ya moto wanafanya kazi hii kwa muda mfupi lakini wanaharibu mazingira. Mimi ningeshauri kuwa labda wangesajili wachache wakapata leseni maalum, maana yake isiwe kila mtu anajikatia tujue kuwa wapo watu waliosajiliwa kwa kufanya kazi hii. Kwa sababu iwe vyovyote miti lazima itakatwa, ama kwa kutumia msumeno wa moto au kule Pemba kuna mwengine tunaita jambeni watu wawili wanavutiana hiyo hatimaye mti unaanguka. Kwa hivyo kwa njia yoyote ile miti itakatwa, kwa hivyo hawa wanaotumia msumeno huu wa moto tungeliwaorodhesha tukasajili wachache wakawa wana leseni maalum na ikawa wanalipa ada serikali.

Mhe. Spika, vile vile wizara hii ina programu nyingi mojawapo ni kuangamiza adui kunguru na mara hii imo katika programu hiyo ya kuangamiza, lakini kama kwanza ningejua katika programu hii mara hii wamekusudia kuangamiza wangapi. Kwa bahati nzuri programu hii inatekelezwa na Ofisi mbili tofauti, moja kakusudia awaangamize wote iwe hawapo tena sijui yeye huyu kakusudia kuangamiza wangapi. Lakini waharibifu si kunguru peke yao wa mambo mbali mbali, wachangiaji wengi wameonesha jinsi ya kuwa na wadudu waharibifu wa mazao yetu katika mashamba ya vipando vyetu tofauti kwenye machungwa, ndimu, mihogo na kadhalika. Je hakuna programu ya waharibifu hawa na wao kuangamizwa. Kwa sababu ni uharibifu wa mazao ya chakula. Chungwa likiingia mdudu

huyu haliliki tena, embe ikiingia funza hailiki tena. Zamani kulikuwa na funza mmoja tu katika kokwa ya embe lakini ilikuwa embe haiharibiki kwa sababu alikuwa yeye kajifunga ndani ya ile kokwa lakini mafunza ya leo yanaingia katika ile nyama ambayo tunataka tuile. Kwa hivyo lazima na hii na wao wangekuwa na programu ya kuangamizwa.

Mhe. Spika, kwa kuwa nilikuwa nishakata tamaa naomba nimalizie hapo. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii, nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa japo hizi dakika saba, mchango wangu utakuwa mfupi lakini utakuwa mzito sana kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni. Ninachokusudia kuzungumza hapa Mhe. Spika, nazungumza kwa nia njema kabisa ya kutetea maslahi ya Zanzibar na wananchi wake.

Mhe. Spika, Wajumbe wako hapa tupo tumechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, ya kuwatumikia wananchi kwa maslahi yao. Mhe. Spika, kuna kilio kikubwa hivi sasa cha wananchi wa Kitogani dhidi ya ndugu zao wa Ukongoroni kwa eneo la mipaka, na suala hili likiachiwa Mhe. Spika, litaleta athari sana na nitakuwa sijafanya haki wananchi wa Jimbo la Muyuni/Kitogani kuhusu mipaka yao. Kwa hivyo nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa twende tuangalie nani mwenye haki ya eneo lile kulitumia hivi sasa, ingawa ardhi yote ni mali ya serikali hilo halipingiki na watu wa Ukongoroni na watu wa Kitogani ndugu wasije wakatofautiana kama ilivyotokea Marumbi na Ukongoroni.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije katika wananchi wa Muyuni kuhusu kilimo cha mpunga. Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Muyuni wameitikia wito wa kilimo cha mpunga lakini bahati mbaya mwaka huu wameathirika sana, na sijui kama ndio tuseme tabia nchi au miundombinu yenyewe ya mvua zinavyonyesha. Wananchi wale hivi sasa wameshachoka na kilimo cha jembe na hivi sasa wanataka kuelekea katika kilimo cha kumwagilia mpunga ndio maendeleo yenyewe. Sasa nitamuomba hapa Mhe. Waziri ni lini wale wananchi wa Jimbo la Muyuni watakuwa na trekta la kuduma pale ili Mwakilishi wao na yeye apate kujibana ili kuwachangia suala la mafuta.

Nikitoka hapo nije katika suala la misitu haraka haraka tulikuwa tunaambiwa tuhifadhi misitu yetu lakini la kushangaza sana Mhe. Spika, hivi sasa katika Ofisi zetu za vitambulisho pana miti inafyekwa pale tunahifadhi kweli hii misitu yetu. Tukitoka hapo tuangalie njia ile ya Bwawani kuelekea kule kuna majumba ya Michenzani pale kuna miti yote imeondolewa kwa ajili ya suala la *parking*. Leo kweli tutabaki na miti, tuangalie msitu wetu uliopo Masingini

unavyopoteza hadhi yake hivi sasa, kwa kweli ni jambo la kusikitisha na la kuvunja moyo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi nitahitaji maelezo kuhusu eneo la Kiwandani kati ya wanachi wa Kitogani na Ukongoroni. Sitounga mkono hoja hii mpaka nitakapopata maelezo haya Mheshimiwa, kumekuwa na tatizo kubwa na jengine hapa wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kweli wanatia huruma sana tena nitakuletea picha hizo uzione, na kumbe Subeit alikwenda, kweli machungwa yao yanapukutika sana Kajengwa. Pana picha pana ushahidi hapa nitakuletea upate kuziona, sijui serikali inawasaidia nini wananchi hawa wa Kajengwa Makunduchi, machungwa yao naona humu, Mhe. Subeit yumo anaonekana kwenye picha nitaleta hapa upate kuziona upate kuangalia hali yenyewe hii ilivyo, sijui serikali imejipanga vipi kuwasaidia wananchi wa Kajengwa, machungwa mengi *alhamdulillahi* yamezaa lakini yote yanapukutika. Ningeiomba serikali hapa ikaangalia suala hili jinsi wanavyojituma wananchi hawa na serikali ipate kuwasaidia.

Vile vile nije kuhusu zao la embe za Muyuni, mwaka jana embe zile zimeharibika na sijui serikali imechukua hatua gani kuhusu mitego ile naomba nao wasaidiwe.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi sitaki kupoteza muda mwingi, sitounga mkono hoja hii mpaka nitakapopata maelezo ya Mhe. Waziri hasa eneo la Kiwandani.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kujaalia asubuhi hii tukawa wazima wa afya na tukaweza kuhudhuria katika Baraza hili tukaweza kutoa michango yetu katika hoja iliyo mbele yetu. Lakini pili nikushukuru na wewe kwamba tuko wengi tuloomba kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo, lakini kutokana na muda haitowezekana kuweza kutoa michango yao kwa maneno na umewaomba hapa watoe kwa maandishi. Kwa hivyo na wewe ukajaalia kunipatia nafasi hii na mimi nikatoa mawazo yangu machache kabisa.

Lakini Mhe. Spika, kabla sijatoa hoja yangu niseme kwamba mimi binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe tunaunga mkono hii hoja.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utaanza katika ukurasa wa 28 *paragraph* ya nane pale inazungumza Idara ya Misitu, Maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, kwa kweli Idara hii ya Misitu mimi nawapa pongezi mia fil mia, ninashukuru miaka miwili na nusu, ulinituma katika kufanya kazi katika Wizara hii ya Kilimo, kwa hivyo tulikuwa tunakwenda sana kwa ndugu zetu

hawa wa misitu tumeona jitihada zao, kwa kweli ni kubwa na ni za kupigiwa mfano. Wanajitahidi sana katika kuotesha miche hii mbali mbali ya misitu na miche ya mikarafuu. Pia nawapa pongezi nyengine kubwa kuwashajiisha wananchi wakaandaa vikundi vyao kwa kuotesha miche hii ya mikarafuu ya minazi na miti mengine mbali mbali.

Kwa kweli wananchi wameamka na wamefahamu na wao watu wa misitu wanaowatembelea mimi binafsi nilipokuwa katika kamati ya Fedha, Uchumi na Kilimo tulikuwa na ziara mbali mbali kufuatilia katika mambo haya ya uoteshaji wa vitalu. Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kweli wanahitaji hongera sana. Hapa Mhe. Spika, wamesema kwamba malengo ya mwaka huu ni kuotesha miche milioni moja ya mikarafuu pamoja na kufanya maotesho ya miche milioni moja ya matunda ya viungo na mambo mengine. Sasa Mhe. Spika, kutokana na changamoto yao moja waliyoiandika katika sehemu ya changamoto hali ya hewa na mvua zisizotabirika wameeleza katika kitabu chao kwamba huwa wanapanda hii miti wakati wa vuli na masika.

Sasa kutokana na hii hali ya hewa kwamba mvua sasa imekuwa adimu, mimi ningeliwashauri sana ndugu zetu wa misitu wasipande tena wakati wa mvua za vuli zinapoanza, kwa sababu mara nyingi mvua ya vuli inakuwa ndogo mno na ukishaipanda miti ikikosa mvua basi miti ile yote huenda ikafa. Kwa hivyo ningeliwashauri sana wapande mwisho kabisa karibu na kuingia mvua za mwaka, kwa sababu hapa mmea kama utapata kutunzwa vizuri utastahmili na kinyevu kilichopo ile ikifika mvua za mwaka miti ile tayari inaanza kumea inakuja haraka, na kipindi cha pili wakapanda mvua za masika ili kuhakikisha kwamba ile waliyopanda mwisho wa mvua za mwaka mwanzo mwanzo na wanaopanda kipindi cha masika itakuwa kiasi fulani miti ile inaweza kustahmili na ikaja juu.

Lakini kutokana na hali ya mvua tulizonazo na akawa anapanda wakati wa vuli, basi siku zote itakuwa tunaotesha miti mingi lakini tunayopata kuweza kustawi itakuwa kidogo mno. Kwa hivyo hali hii ya hewa ni vyema tukaiona na tukashirikiana ili kuhakikisha kila tunachokiotesha basi kinastawi vizuri. Lakini pia Mhe. Spika, wanasema kwamba kuna kupanda hekta 30 za eneo la mikoko na kilomita 50 maeneo ya barabarani. Mhe. Spika, suala la miti ya mikoko mimi binafsi Wizara hii na idara yake pale Wete nimeshaifuatilia sana kwamba tuna tatizo la hali ya ukame sehemu zetu hasa Jimbo langu la Tumbe, miti hii imepotea kwa wingi na wananchi tumewashajiisha wameshajaribu kupanda miti mbali mbali lakini ufuatiliaji umekuwa ni mdogo. Ningeliiomba sana Wizara wafuatilie sana hasa katika Jimbo letu la Tumbe kwa sababu wananchi sasa hawapati tena kulima, maji ya bahari yanachukua maeneo ya kilimo. Kwa hivyo naiomba sana Wizara katika hekta hizi 30 basi Jimbo la

Tumbe walione kwamba linahitaji kupata upandaji wa miti hii ya mikoko kwa sababu wananchi tayari wako tayari, inayobakia pale ni kuhamasishwa.

Lakini pia Mhe. Spika, eneo hili la barabarani mwaka 1992 baada ya kumalizika barabara ya *Cogefer* naishukuru sana Wizara ya Kilimo iliwahamasisha wananchi na Wizara yenyewe ikapanda miti hii kando kando ya barabara ya *Cogefer* ninashukuru sana. Wananchi walipata vivuli na wakapata kuni na mambo mengine, lakini Mhe. Spika, miti hii imewapatia faida kubwa sana wananchi iliyopandwa kando kando ya barabara. Lakini hivi sasa Mhe. Spika, imekuwa ni kinan'ganyiro miti ile hajulikani mwenyewe ni nani. Watu wa Ardhi wanasema ni yao, watu wa kilimo ni yao, misitu ni yao watu wanajivunia, tatizo panavunwa lakini hapapandwi mengine, sasa ningeliiomba sana Idara hii isimamie suala hili kila mmoja ni mkubwa, watu wote ni kambare kila mmoja ana ndevu kila mmoja ni mkubwa hajulikani nani mdogo nani mkubwa.

Kwa hivyo ili kuliondoshea tatizo hili ningeliomba sana hizi kilomita 50 basi naomba Wizara kupitia Idara hii basi eneo hili la Tumbe waweze kuja kuwapa taaluma shehia hizi zilizopitiwa na barabara, mikeshia ile imo katika maeneo mbegu zile zipo, waje wawape taaluma na tuweze kurejesha hali ile ya hewa ya barabara ili watu waweze kupata vivuli na hii miti itakapokuwa tena kama ilivyokuwa mara hiyo watu waweze kufaidika.

Mhe. Spika, huu mti wa mkeshia unazalisha vitanda na Mhe. Spika, ukikiona kitanda cha mkeshia utakinunua kwa bei yoyote, kwa hivyo unapata tija kubwa. Watu wanatoa madirisha, dirisha lake ni la mfano Mhe. Spika. Kwa hivyo hii miti ikikua ikawa mizuri na mikubwa na yenye faida kubwa kwa wananchi, lakini wakati wa kuvuna kila mmoja yeye ndiye muhusika. Kwa hivyo ningeliomba sana Idara isimamie suala hili ili ile iliyopo tujue ni nani anayehusika na ile miti, na ile miche iliyopo iweze kupandwa ili kurudisha ile hali ya hewa, na itakapofika wakati wa kuvuna wananchi pia na serikali iweze kufaidika.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika changamoto moja nimeshaisema kwamba wajaribu kubadilisha kupanda miti wakati ule wa vuli wapande katika kipindi kile.

Lakini changamoto chengine waliyonayo ndugu zetu wa kilimo ni uchache wa mabwana na mabibi shamba. Mheshimiwa hili nasema kwamba hatuna uchache wa hawa mabwana na mabibi kwa sababu tuna Chuo hiki Chuo kipo Kizimbani kinazalisha watu hawa. Hivi sasa wapo wengi wanazururа humo mabarabarani, hivi sasa ukienda hapo Juakali wamejaa mabwana na mabibi shamba tatizo ni nini? Tatizo ni kwamba serikali haijajipanga hawa watu

wapo wanahitaji ajira, sasa mimi ningeliomba sana Ofisi ya Rais Fedha na kupitia Ofisi ya Rais Utumishi hiki kilio cha ndugu zetu wa kilimo wakione. Kwa sababu mkulima bila ya kupata taaluma kwa kupitia bwana shamba au bibi shamba itakuwa Mhe. Spika, mara zote tunafeli kilimo, watu wetu hawafaidiki wala hakuna tija inayopatikana.

Mhe. Spika, ni machungu sana kulima ukakosa kupata taaluma na ukakosa kuvuna haya yanakatisha tamaa, kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara hizi mbili kwanza Wizara hii ya Fedha hii keki iongezwe. Kwa sababu kama hawa hawatoingiziwa mshahara Wizara itashindwa kuwaajiri mabwana shamba na mabibi shamba, kwa hivyo hii keki yao hii ijaribiwe kuongezwa zaidi ili waweze kuwaajiri hawa mabwana shamba na mabibi shamba ili wakulima wetu waweze kufaidika. Na ningeliomba sana Mhe. Spika, kama walivyosema wengine waajiriwe mabwana shamba na mabibi shamba katika maeneo yao.Kuna mtindo wa kuchukua mabwana shamba Mkoani wakaletwa Micheweni hakai miezi miwili mitatu anarudi kule kule Mkoani. Kwa hivyo wale wakulima wetu pale ile faida waliyokuwa wanaipata hawaipati tena. Hili naliomba sana Mhe. Spika.

Nimalizie Mhe. Spika, naujali sana muda wako kwa Idara ya Umwagiliaji Maji ukurasa wa 34 *paragraph* ya 10.0 Mheshimiwa nishukuru kwamba Idara inafanya kazi zake vya kutosha kabisha tumeitembelea tumeoneshwa maeneo ambayo tunahitaji kulima mpunga wa umwagiliaji maji Mhe. Spika, yanatukifu kabisa, tatizo serikali haijawa tayari kuwaboresha hawa watu wakalifanya hili suala. Tatizo tunaelekeza sana nguvu zetu kwa wahisani, mhisani ni hiari kukusaidia kile ambacho atakupa, na mara nyingi wahisani wetu hawa hawatufikishi katika yale malengo ambayo tunayoyahitaji, kwa hivyo ikabakia tunaimba tu umwagiliaji maji, umwagiliaji maji Mtwango, wapi, wapi, wapi lakini hatutofika na wananchi wanaanza kupoteza ule uhalisia wao na ile kauli aliyoitoa Rais ya kusema kwamba kilimo ni uti wa mgongo.

Sasa kama tutategemea wahisani Mhe. Spika, hili halitofika abadal abidina, lakini hebu serikali ikusudie kwamba kilimo asilimia ya wakulima wanaokwenda katika kilimo, hebu wajaalie sasa hii Idara ifanywe kwamba ni kipaumbele, ili tuweze kufikia katika yale malengo serikali iliyokusudia. Lakini pia Mhe. Spika, tunao wakulima hawa wa umwagiliaji hasa bonde la wananchi wangu pale Kinoo, hili bonde bwana watu wameshindwa kuvuna Kinyakuzi, hawakuvuna kabisa vuli hata mipunga mengine haikufumua kabisa. Hapa ningeliomba Mhe. Waziri hawa wakulima hawa wa Kinyakuzi na mabonde mengine utawasaidia nini?

Mhe. Spika, ninashukuru nishapongeza tokea mwanzo.

Mhe. Spika: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kunipa mashirikiano makubwa katika uchangiaji wa jumla, na sasa nimuombe basi Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili aanze kufanya majumuisho wakati Mhe. Naibu Waziri anaanza kufanya majumuisho, niwaombe Waheshimiwa walioko nje basi warudi ndani ili tuhakikishe kwamba kazi hii tunaimaliza pamoja. Naomba sana Waheshimiwa walioko nje warudi ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia na kujibu baadhi ya hoja za Wajumbe Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako tukufu kuhusu hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Wajumbe kwa kuichangia vizuri hotuba ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, napenda kuwahakikishia kuwa michango yao, maelekezo na ushauri wao tunaupokea na yote tutayafanyia kazi ipasavyo kadri ya uwezo utakavyoruhusu kwa utekelezaji wa majukumu ya kazi ya maendeleo ya Wizara.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wake wa Kamati ya Kudumu ya Fedha Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa michango yao na maelekezo katika utayarishaji wa bajeti hii, tunaahidi kwamba Wizara itayafanyia kazi maelekezo na ushauri walioutoa.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inakubaliana na hoja ya Kamati ya Biashara, Fedha na Kilimo kwamba fedha zilizotengwa katika bajeti ni ndogo kulingana na mahitaji ya Wizara, aidha tunakiri kwamba uingizwaji wa fedha kutoka serikalini hasa za maendeleo si mzuri. Hata hivyo wizara inafanya jitihada za mara kwa mara kuwasiliana na uongozi wa Wizara ya Fedha kwa lengo la kutatua changamoto hii.

Mhe. Spika, hoja ya kuongezeka kwa mapato ya Wizara, sababu zilizosababisha kuvuka kwa lengo la mapato ni pamoja na usimamizi na uratibu mzuri wa ukusanyaji wa mapato na kuongezeka kwa idadi ya miche ya misitu iliyozalishwa. Aidha kuhusiana na hoja ya kutokusanya mapato na mauzo ya miche kwa Pemba fedha zake zimeingizwa katika kifungu cha 142101 cha mauzo ya miche, ambapo jumla ya 4,400,780/= zilikusanywa kwa kipindi hichi sawa na asilimia mia nne ya lengo la kukusanya jumla ya 1,000,000/=.

Mhe. Spika, mazingira mabaya ya kazi yaliyokuwa kwa wafanyakazi wa Idara ya Kilimo ambao walikuwa wakitumia majengo ya maabara ya Kizimbani kuwa ni sehemu zao za kufanyia kazi, suala hili tayari limeshapatiwa ufumbuzi, na hivyo wafanyakazi hao kwa sasa wamewekwa katika majengo ya Wizara yaliyopo Mbweni Zanzibar.

Mhe. Spika, kuhusu kuhakiki mali za Serikali ikiwemo majengo na mashamba; suala hili linatekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kutokana na hali ya fedha inaporuhusu, kwani maeneo yanayohitaji kupimwa ni makubwa, na hivyo kufanya gharama zake kuwa kubwa. Hata hivyo Wizara imeanza na itaendelea na kazi hii kadiri hali itakavyoruhusu, kwa sasa maeneo yaliyokwishapimwa na kupatiwa hati miliki kwa mashamba ni Kizimbani, Bambi, Ndijani, Kijichi, Miwani, Selem, Makunduchi na Mwera na kwa upande wa majengo ya SST na SDPL, Marumbi, Mazizini, Mbweni na Saateni kwa Unguja, aidha Wizara imetenga fedha katika bajeti inayokuja kwa ajili ya kazi hii.

Mhe. Spika, Wizara inachukua juhudi za kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake kwa mujibu wa bajeti na hali ya fedha inaporuhusu. Suala hili linatekelezwa kwa pamoja kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2012/13. Wizara imeweza kupeleka jumla ya wafanyakazi 106 ikiwemo watafiti katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi na kwa ngazi tofauti.

Mhe. Spika, kuhusu suala la uhaba wa maji katika Chuo cha Kizimbani. Wizara ya Kilimo imeliona suala hili na hivyo Wizara imeshalipa fedha kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar ZAWA kwa ajili ya uchimbaji wa kisima ambapo kwa sasa uchimbaji wa kisima hicho unaendelea kwa lengo la kupatikana huduma ya maji kwa wanafunzi na Chuo kwa ujumla. Aidha kuhusu suala la gari linalotumika kwa huduma za wanafunzi kuwa ni mbovu, chuo hivi karibuni kimepata gari mpya yenye namba ya usajili SMZ 290A ambapo gari hiyo inakuwemo chuoni hapo kwa muda wa usiku kwa lengo la kutoa huduma pindi inapotokea wagonjwa wanaohitaji kupelekwa katika hospitali za mbali. Pia chuo kina basi ambalo hutumika kwa ajili ya usafiri kwa wafanyakazi na wanafunzi.

Mhe. Spika, suala la malipo ya ziada kwa madereva. Ni kweli kwamba madereva na mafundi hawakulipwa fedha zao za likizo na malipo ya ziada, aidha Wizara imetenga fedha za kuwalipa katika bajeti ya mwaka 2013/14 ambapo watendaji hawa watalipwa kama inavyostahiki.

Mhe. Spika, ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao unaendelea kwa kukamilisha utiaji wa milango, madirisha, sakafu na umeme. Mara baada ya

kukamilika kazi hiyo uhamishaji wa vifaa kutoka ghalani kwenda kituoni huko itafanyika. Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na juhudi za usimamizi wa mali asili kwa kuhamasisha wanajamii kusimamia mali asili zao. Aidha Wizara inaendelea na kazi za doria ili kupiga vita matumizi ya msumeno wa moto. Katika mwaka huu jumla ya misumeno 57 Unguja na Pemba ilikamatwa na kuangamizwa, ili kudhibiti suala hili, rasimu ya uzuiaji wa matumizi ya msumeno wa moto tayari imeshatayarishwa.

Mhe. Spika, uendelezaji wa kituo cha uzalishaji wa mbegu cha Bambi unaendelea kwa kupima na kutayarisha michoro ya umwagiliaji maji, na Wizara inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji.

Mhe. Spika, suala la ukosefu wa vitendea kazi katika kituo cha utafiti cha Matangatuani Pemba. Wizara inaendelea na ukarabati wa ujenzi wa Maabara zake za Unguja na Pemba, baada ya kukamilika kazi hii ununuzi wa vifaa na vitendea kazi utafanyika. Aidha utafiti wa mashambani unaendelea kwa mbegu za mazao na chakula kama tulivyoeleza katika kitabu chetu.

Mhe. Spika, napenda kujibu suali la Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Wawi kuhusu utafiti wa mbegu ya *nerika* katika ukanda wa mashariki ya Pemba. Namuhakikishia Mhe. Mwakilishi, Mheshimiwa Mkwe wangu kwamba utafiti umefanyika katika mabonde ya Tovuni, Ungoni, Jombe Ume, Mchangamdogo, Msubaha, Vitongoji na Chanjaani, na Chambani ambako matokeo ya utafiti huo yameonesha mafanikio mazuri.

Mhe. Spika, Wizara imekuwa ikiotesha miti ya mikarafuu na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo kwa kutumia matende na mabotea, uoteshaji huu umechangia katika kurudisha mashamba ya mikarafuu na kufanya maeneo hayo kuwa na mikarafuu mingi yenye umri mdogo. Kwa mwaka wa fedha 2013/14 lengo letu ni kuzalisha miche 1,000,000 na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo. Aidha suala la utafiti juu ya njia bora za uzalishaji wa karafuu linaendelea kwa lengo la kuongeza tija na kudumisha ubora wa karafuu zetu.

Mhe. Spika, suala la kupotea kwa misitu ni kubwa, kama tulivyoeleza katika changamoto za Wizara hii, kwa kuliona hilo Wizara imechukua hatua zifuatazo:

1. Kupitia na kurekebisha kanuni za msumeno wa moto ili kupiga marufuku kabisa matumizi ya msumeno huo.
2. Kusimamia maeneo yenye misitu ya asili kama vile Ngezi, Msikiti Mkuu Ras Kiuyu, Jozani, Kiwengwa na Masingini. Pia kuongeza maeneo mapya ya hifadhi kama vile Jambiani, Muyuni, Ufufuma na Kangani ili kuongeza makaazi ya ndege na wanyama wakiwemo Kwau.

3. Kushirikiana na jamii kuhifadhi misitu ya asili ya jamii ambako jumla ya mipango ya usimamizi ya jamii imeandaliwa na ipo kwa Mwanasheria Mkuu kwa hatua za kukamilika.

4. Kushajiisha matumizi ya nishati mbadala kwa kupikia ikiwemo gesi na matumizi ya majiko sanifu.

Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Ussi Jecha Simai, Mwakilishi wa Chaani kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na hatua za kufuatilia upatikanaji wa hati miliki ya shamba la Makurunge kwa ajili ya matumizi ya Chuo cha Kilimo Kizimbani. Hatua zilizochukuliwa ni hizi zifuatazo:-
Kufanya kikao cha pamoja kati ya Waziri wa Kilimo na Mali Asili wa Zanzibar na Waziri wa Ardhi na Mipango Miji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ambapo wenzetu walitoa pendekezo la kutoa eneo jengine lenye ukubwa sawa na eneo la Makurunge katika Mkoa wa Pwani au Lindi kwa hoja kwamba eneo lililobaki halifai kwa kazi za kilimo na ufugaji. Wazo hili liliwasilishwa katika kikao cha Baraza la Mapinduzi na halikukubaliwa, Baraza likaiagiza Wizara iendelee kudai hati miliki ya shamba lililopo katika eneo la Makurunge.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Mali Asili iliiandikia Wizara ya Ardhi na Mipango Miji na baadae Kamishna wa Ardhi wa Tanzania Bara aliiandikia Wizara yetu juu ya kukubali kupatiwa hati miliki ya eneo hilo, Wizara hivi sasa ipo katika hatua za kukamilisha taratibu za upatikanaji wa hati miliki.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Utumishi wa Umma na Utawala bora na Kamisheni ya Utalii ya umma imetoa maelezo kwa vyuo kutayarisha rasimu ya malipo ya mishahara kwa wafanyakazi kama ilivyoelekezwa na sheria nambari 2 ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, ni kweli ubalozi wa Norway umeonesha nia ya kusaidia ujenzi wa dakhalia ya wanawake yenye ghorofa nne, hatua za awali za uandaaji wa michoro na utayarishaji wa gharama na zabuni uko katika hatua za mwisho. Aidha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2013/14 imetenga shilingi 90,000,000/= kwa kuchangia ujenzi huo.

Mhe. Spika, kuhusiana na upungufu wa vitendea kazi katika Chuo cha Kilimo Kizimbani. Wizara imekuwa ikichukua hatua za kukiimarisha Chuo hicho kwa kutenga na kutoa fedha za ruzuku pamoja na kuwasiliana na washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, mfano mzuri ni uimarishaji wa Maktaba ya Chuo kwa kupatikana vitabu vya kufundishia na ujenzi wa dakhalia pamoja na vifaa vya kufundishia vikiwemo kompyuta, pia Chuo

kinategemea kupokea matrekta madogo manne hivi karibuni ili kuhakikisha vifaa vyote muhimu vinapatikana.

Mhe. Spika, kuhusu shamba la misitu liliopo Chaani. Shamba hili ni la hifadhi ya Serikali ambalo limetangazwa kwa kuwa msitu huu wa hifadhi mwaka 1987. Aidha wananchi walilipwa haki zao wakati Serikali ilipotangaza eneo hilo kuwa msitu huo wa hifadhi. Shamba hili lilikuwa limepandwa miti lote kama yalivyo mashamba mengine ya Serikali, lakini baada ya kuvunjwa wananchi waliingia na kuanza kulima mazao mbali mbali. Hata hivyo wakati wa kupanda tena miti maeneo hayo wananchi wamekuwa waking'oa miti kwa madai kuwa maeneo hayo ni mali yao. Katika kuimarisha shamba hili Wizara imechukua hatua zifuatazo:-

1. Kukutana na Uongozi wa Mkoa na Wilaya pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mikoa. 2. Kuwapaleka katika vyombo vya sheria wale wote wanaohujumu miti iliyo katika eneo hilo.
3. Kuendelea kutoa taaluma kwa wakulima na masheha kuhusu kuitunza na kuiendeleza miti iliyopandwa katika eneo hilo.

Aidha Wizara inamuomba Mhe. Mwakilishi, kuwahamasisha wananchi wake kuacha uharibifu wa miti iliyo katika maeneo hayo. Kuendelea kupanda miti katika maeneo yote yaliyovunwa ndani ya shamba. Kuingia mikataba na wakulima wanaolima katika eneo hilo.

Mhe. Spika, pia napenda kumwambia Mhe. Mwakilishi, kuwa uharibifu wa miti kwa makusudi katika shamba hilo ambayo ni mali ya Serikali ni kwenda kinyume na sheria ya nchi. Hivyo basi Wizara ingawa haipendi kuchukua sheria za kuwafungulia mashtaka pamoja na kuwaadhibu, lakini lisilobudi hutendwa.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea na juhudi za kurejeshea mashimo yaliyochimbwa ili yaweze kutumika upya. Kwa mwaka uliopita jumla ya hekta 18 zilifukiwa na kupandwa miti Unguja na Pemba, kazi hii itaendelea kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha kwa kuwa kanuni ya usimamizi wa mali asili zisizorejesheka imeshatoka, tutaendelea kusimamia kazi hii kwa kuwajazisha mikataba watu wanaochimba mali asili hizo kwa mujibu wa kanuni ikiwa ni pamoja na kuhakikisha jamii inachangia katika kurejesha maeneo hayo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe. Nakubaliana na hoja juu ya kuchelewa kuanzishwa kwa hifadhi ya chakula hapa nchini na ni dhahiri kwamba Wizara inahitaji kujipanga vizuri katika kulitekeleza jukumu hili. Hatua zilizochukuliwa na

Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kufanikisha uanzishwaji wa hifadhi hiyo ni uchambuzi yakinifu juu ya uanzishwaji wa hifadhi ya chakula, kazi hii imekamilika na imeshawasilishwa Serikalini. Utayarishaji wa miongozo na kusimamia na kuendeleza hifadhi ya chakula, miongozo hii tayari imekamilika kwa kutumiwa.

Mhe. Spika, uanzishwaji wa mfumo wa ukusanyaji wa uchambuzi wa taarifa za masoko na makundi ya watu wanaoishi katika mazingira ya hatari ya ukosefu wa chakula umekamilika na mafunzo kwa watumiaji yanaendelea kutolewa.

Mhe. Spika, uanzishwaji wa maghala ya akiba unahitaji kuwepo kwa mifumo na hatua tulizozitaja hapo juu, kutokana na kukamilika taratibu hizi Wizara itaendelea na taratibu za ukarabati wa maghala kama ilivyoainishwa katika hotuba ya bajeti hii.

Mhe. Spika, nakiri kwamba wakulima wote wa mabonde ya umwagiliaji maji ikiwemo Bumbwi Sudi wanatakiwa wachangie huduma za umeme katika vituo vya umwagiliaji ambavyo ni kati ya shilingi 20,000/= na 30,000/= kwa mkulima kwa msimu. Aidha kwa kuwa fedha hizo hazitoshi, kwa msimu uliopita Wizara imelipa gharama zilizobaki na gharama zote za madeni yaliyopita. Mhe. Spika, kwa upande wa Bumbwi Sudi tunaomba kumuarifu Mhe. Mwakilishi, kwamba kuna jumla ya vishamba 309 ambapo kila mkulima alichangia shilingi 20,000/= na jumla ya shilingi 6,018,000/= zilikusanywa na viongozi wa jumuiya ya kila bonde na sio maofisa wa Wizara ya Kilimo na Maliasili. Hata hivyo suala la Afisa wa Kilimo aliyetajwa ndugu Kadiri hukusanya fedha za wakulima hao sio sahihi na wala fedha zilizokusanywa sio 20,000,000/= kama ilivyoelezwa na Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, kuhusu fedha za miradi ya maendeleo kama zilivyoainishwa katika kifungu cha kitabu cha makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka 2013/14 fungu nambari 20 Wizara ya Kilimo na Mali asili ukurasa wa 458 mpaka 459, maelezo ya miradi hiyo yameainishwa wazi wazi katika kitabu chetu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 43 hadi 55 kiambatanisho nambari 2 hadi nambari 10.

Mhe. Spika, kuhusiana na hoja ya fedha za *basket fund* wanazopata Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Tanzania Bara fedha hizi hutolewa kutekeleza *program* ya SSDP ambayo ni makhsusi kwa Tanzania Bara pekee. Kwa upande wa Zanzibar washirika wa maendeleo wanachangia kupitia mfuko wa miradi ya *program* badala ya *basket fund.* Aidha kupitia mfumo huo wa miradi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2012/13 ilipangiwa kupata 900,417,016,000/=, kama ilivyoanishwa katika hotuba ya bajeti.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Salma Mohammed Ali, nafasi za wanawake. Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kilimo cha umwagiliaji maji kinapewa msukumo unaostahiki Unguja na Pemba. Mara baada ya kuandaliwa mpango mkuu wa umwagiliaji maji wa 2012 kwa upande wa Pemba mabonde ya Weni, Tibirinzi, Makombeni yameendelezwa. Aidha na mabonde ya Kinyakuzi na Machigini yamefanyiwa matengenezo, mabonde ya Mlemele, Pujini na Makwararani, Wingwi yameingizwa katika mpango wa kuendelezwa kwa kutumia fedha za Exim Bank ya Korea. Pia mabonde ya Dobi, Machigini yataendelezwa, na kwa upande wa visima kwa sasa tunavyo visima vinne vya umwagiliaji maji huko Pemba.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa Wilaya ya Chake Chake ina mabwana shamba 7 kwa sasa, hata hivyo idadi hiyo itaongezeka ndani ya mwezi ujao baada ya kupangiwa kazi mabwana shamba na mabibi shamba wapya walioajiriwa. Mabwana shamba na Mabibi shamba hao ni kidogo na hivyo kupelekea kushindwa kufikia wakulima wote kwa wakati. Hata hivyo baada ya kuliona hilo Wizara imeamua kuanzisha skuli za wakulima, na hivyo katika Wilaya ya Chake Chake kuna skuli za wakulima zisizopungua 133. Aidha kuhusu suala la wakulima wa Bonde la Dobi waliopelekewa mbegu mbovu. Napenda kuwapa taarifa waandishi wetu, ningeliwaomba wakati wanapoandika taarifa waandike taarifa ambapo washafanya uhakika.

Mhe. Spika, napenda nieleze kidogo tu "Mtume alipopita pahala akamkuta ng'ombe kaekewa kisu kwenye shingo yake, kufika usoni akaulizwa *yaa rasulah llah*, ulipopita hapo huyo ng'ombe keshachinjwa, basi alisema nimepita nimemuona ng'ombe kaekewa kisu, lakini kwa mimi ningelisema ng'ombe ameshachinjwa, pengine kile kisu kingeondolewa" Kwa hiyo hii ni taarifa ambayo ni vizuri ya kuitoa.

Mhe. Spika, wakulima wa Bonde la Dobi waliopewa mbegu, Mhe. Spika, wakulima hao hawakupewa mbegu mbovu, taarifa ya watu wa mawio mimi nimeisikia walisema wamepewa mbegu mbovu. Wakulima hao hawakupewa mbegu mbovu ila walipewa mbegu ambazo haziwezi kufumua wakati wa kipindi cha vuli, hao walipewa wakati mbegu hizo haziwezi kuchanua wakati wa vuli na hao wakulima ambao waliopata hasara walipewa fidia ya asilimia 100 ya maharibiko yaliyotokea, jumla ya 1,350,000/= zimelipwa kwa eneo la hekta 0.45 liliotarajiwa kuvunwa kilo elfu moja mia moja ishirini na tano za mpunga.

Mhe. Spika, ushauri wa kuziendeleza Karakana za Matrekta kwa Unguja na pamoja na nyongeza za mishahara tunaupokea na tutaufanyia kazi. Kutokana

na uzito wa suala hili Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliiagiza Wizara ya Kilimo na Mali asili na Ofisi ya Utumishi wa Umma kufanya mapitio ya maslahi ya wafanyakazi wa Karakana hizo pia kazi hii inaendelea.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeandaa utaratibu wa ugawaji wa pembejeo ambapo daftari maalumu la wakulima limeandaliwa ambalo wakulima husajiliwa na kupatiwa huduma za pembejeo kulingana na taarifa za usajili wao. Utaratibu huu unafanyika kwa mashirikiano baina ya wakuu wa vituo vya utoaji wa huduma na viongozi wa jumuiya za wakulima wa maeneo husika pamoja na maofisa wa kilimo wa wilaya na mabwana shamba.

Mhe. Spika, Wizara haikubaliani na hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba pembejeo za kilimo zinatolewa kwa wakubwa tu kwani baadhi ya vituo bado pembejeo hizi zipo, pamoja na kwamba msimu wa kilimo cha mpunga umeshamalizika.

Mhe. Spika, kuhusu uzalishaji wa chumvi, suala hili halimo katika usimamizi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, hivyo tunamuomba Mhe. Mwakilishi alielekeze katika Wizara ama Taasisi husika, hata hivyo kutokana na sababu za uhifadhi wa mikoko na mazingira ya ukanda wa pwani wa visiwa vya Zanzibar, Wizara ya Kilimo na Mali asili inashauri kutowepo na ongezeko la eneo lolote jipya la uzalishaji wa chumvi, na maeneo yote yasiyotumika tunashauri wananchi wayatumie kwa kupanda mikoko.

Mhe. Spika, kuhusu mradi wa Kunguru. Ni kweli kuwa mradi huu ulikuwa unasimamiwa na Idara mbili, Maofisa wa Misitu na Maofisa wa Mazingira. Kutokana na Wilaya zote 10 za Zanzibar ndio wanashiriki katika kuelimisha na kutekeleza mradi huu, hali halisi iliyokuwepo ni kwamba Idara walikuwa na fedha za SMZ na Idara ya Misitu na Mali asili zisizorejesheka ilikuwa na fedha za mchango wa washirika wa maendeleo ambao ni Ubalozi wa Finland. Hata hivyo kuanzia mwaka huu wa fedha mradi huu utasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Mali asili kupitia Idara ya Misitu na Mali asili zisizorejesheka pekee.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Ali Salum Haji, Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa katika kituo cha Kibokwa hakuna tatizo la ubovu wa *pump*, *pump* za Kibokwa zote ni nzima ila mara nyingi huwa zinatokea hitilafu katika mfumo wa umeme jambo ambalo linasababisha *pump* hizo zisitumike, hivi sasa *pump* hizo zinafanya kazi zote.

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha tathmini ya kushuka au kupanda kwa mazao ya kilimo zinapatikana kupitia tathmini ya mavumo na mazao inayofanywa kila mwaka na maafisa na wataalamu wa Wizara. Tathmini hii hufanywa kwa kuvuna eneo lenye ukubwa wa wastani wa mita 5 kwa 5 kwa zao la nafaka, na kupimwa mazao hayo kujua wingi wake, na hivyo kulinganisha na eneo lote la ukulima wa zao husika ili kupata tathmini ya kitaifa.

Mhe. Spika, kwa upande wa mazao yanayoletwa sokoni ambayo huletwa katika vifungasho tafauti kama polo, pakacha, rumbesa, tenga na vyenginevyo, Wizara inatumia viwango maalumu vinavyokubaliwa kama ifuatavyo. Mfano polo la muhogo na viazi vikuu na viazi vitamu ni kilo tisini.

Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa mitego ya kunasia nzi wa matunda bado inaendelea kupatikana katika vituo vya kilimo ikiwemo Kizimbani, kituo cha Utibabu wa Mimea kiliopo Mwanakwerekwe kwa Unguja na Machomanne kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, baada ya kutoa majibu hayo sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wawakilishi ambao wamechangia hoja hizi na wale ambao hawakuchangia, imani yangu kwamba wataipitisha bajeti yetu ili tuweze kuleta mafanikio ya kilimo, hususan ukizingatia Wizara hii kila mmoja inamhusu kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Spika, napenda tena kuchukua fursa hii kuwashukuru watendaji wangu ambao wamenipa mashirikiano makubwa baada ya kuingia katika Wizara hii nikiwa mgeni. Kwani Mhe. Spika, wanaelewa kuwa mgeni yeyote hata kama ana macho anakuwa kipofu.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru sana Katibu Mkuu wangu, Naibu Katibu Mkuu Kilimo, Naibu Katibu Mkuu Maliasili, Afisa Mdhamini Pemba pamoja na Wakurugenzi wote na watendaji wa Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nyengine ya kusimama hapa na kutoa ufafanuzi wa hapa na pale. Mhe. Spika, leo katika kuchangiwa Wizara hii tumetumia mfumo wa *supersonic*, huwezi kuamini kwamba waliochangia kwa maneno ni 18 katika kipindi kifupi na waliochangia kwa maandishi ni 9, ukiwajumlisha hao unapata kama 27. Kwa hivyo, hii ni *speed* nzuri sana na kwa kweli imesaidia sana katika kuendesha shughuli zetu hizi, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, waliochangia ni:

1. Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo)
2. Mhe. Saleh Nassor Juma
3. Mhe. Ussi Jecha Simai
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Salma Mohammed Ali
6. Mhe. Ali Salum Haji
7. Mhe. Subeit Khamis Faki
8. Mhe. Panya Ali Abdalla
9. Mhe. Asaa Othman Hamad
10. Mhe. Asha Abdu Haji
11. Mhe. Asha Bakari Makame
12. Mhe. Salim Abdalla Hamad
13. Mhe. Mussa Ali Hassan
14. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
15. Mhe. Mohammed Haji Khalid
16. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
17. Mhe. Rufai Said Rufai na
18. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Mali asili

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
2. Mhe. Nassor Salim Ali
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
5. Mhe. Omar Ali Shehe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali
7. Mhe. Marina Joel Thomas na
8. Mhe. Hija Hassan Hija

Hawa ndio waliochangia kwa maandishi, kama yuko mmoja nimemuacha atanisamehe, sikumuacha kwa makusudi ni bahati mbaya. Hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri ameshajibu hoja nyingi ambazo zinahusiana hapa na pale, kama vile hoja ya Chuo cha Kilimo Kizimbani ameshaijibu, hoja ya matatizo ya pembejeo kama ilivyotajwa katika hotuba ameshajibu na hoja ya maeneo mbali mbali Mheshimiwa ameshajibu. Mimi nitazungumza kwa muhtasari tu kwa wale ambao wamechangia mchana wa leo kama ifuatavyo:-

Mhe. Subeit Khamis anasema ingawa Zanzibar haijabahatika kuwa na wanyama pori wakubwa kwa ajili ya utalii, hata hivyo wanyama wetu tulionao ni kivutio kikubwa cha utalii. Wizara inasimamia uhifadhi wa wanyama kwa kushirikiana na wanajamii kupitia kamati za uhifadhi wa sheria na hivi sasa wanajamii wanashirikishwa na kampuni za uwekezaji wa kitalii kufanya uwindaji wa kitalii ambapo mapato yake yanagaiwa kwa wananchi na serikali. Halikadhalika wanajamii wanaozunguka misitu ya hifadhi wanashirikishwa katika kuhifadhi mali asili hizo na wanafaidika na mapato yanayopatikana.

Ni kweli kwamba tatizo la wadudu wa matunda na jitihada kubwa inachukuliwa na wizara ikiwa ni kuweka mitego ya kuwanasa wadudu hao. Hali hii inapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hili, pia wananchi ndio wanatakiwa wasaidie katika kupunguza tatizo la wadudu kwa kuzika matunda yaliyoharibiwa na wadudu.

Mhe. Spika, kazi hii ni vizuri tungeifanya na Waheshimiwa Wawakilishi. Ni kweli machungwa mengi yanaharibika na tunakula hasara sote tunao machungwa. Picha nilizoletewa sasa hivi na Mhe. Jaku Hashim kuonesha matunda yanapukutika nikimpeleka kwenye shamba langu basi ile naipiku mara mbili jinsi matunda yalivyopukutika ya machungwa. Lakini sasa dawa yake ni kuyakusanya na kuyazika pamoja na kutumia mitego, ukiacha vile vile wale wadudu wanazaliana wanaondoka chini wanakuja tena kwenye michungwa na wanashambulia machungwa, dawa yake ni kuyazika matunda yale.

Aidha, mabwana shamba wameenezwa kwa kila shehia isipokuwa idadi ya mabwana shamba hao ni ndogo, na hivyo haitoshelezi kukidhi mahitaji kwa kila shehia kuwa na bwana shamba wake. Hali hii imepelekea kwa baadhi ya maeneo bwana shamba mmoja kuhudumia zaidi ya shehia moja. Hata hivyo, kila mwaka wizara inaajiri wapya ili kuboresha huduma zaidi. Kwa mwaka huu wizara imeajiri mabwana na mabibi shamba 46, Unguja 15 na Pemba 31.

Kilimo cha mikarafuu. Mhe. Spika, kilimo cha mikarafuu kinapewa umuhimu mkubwa na serikali kwa kuwa Wizara inaelewa suala hili ndio muhimili wa uchumi wetu. Wizara imekuwa ikiotesha miche ya mikarafuu na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo. Aidha, wizara pia inatoa elimu ya uoteshaji wa mikarafuu kwa watu binafsi, na miche hiyo hununuliwa na serikali na baadae kuigawa kwa wakulima bila ya malipo. Ili kuimarisha zao hili malengo ya uzalishaji wa miche yameongezwa kutoka miche laki tano mwaka 2012 hadi milioni moja mwaka 2013.

Mhe. Spika, malalamiko haya ya kwamba miche ikipandwa inakufa yameenea sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Lakini napenda kuwaambia tu wakulima wenzangu pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi, kwamba mkarafuu ni mti harara sana, ni mti ambao lazima mzizi wake unapoupanda ukamate ardhi barabara ili ule umajimaji wa ndani ya ardhi uwezeshe ule mti kuweza kuchipua na kuendelea kuulinda. Ukipanda mti wa mkarafuu kwa kuuweka tu ndani ya shimo halafu ukafukia kama uliopanda mchicha aaa, jua likitoka udongo ule ukikauka miti ile inaachana na mkarafuu unakauka. Kwa hivyo, nafikiri ipo haja ya mche wa mkarafuu unapoupanda kuushindilia kweli kweli hasa.

Mimi nakumbuka wazee wetu walipokuwa wakipanda mikarafuu hucheza ngoma hasa pale kwenye ule mche wa mkarafuu, ili mkarafuu ule ukamatane kabisa na ule udongo uliopo pale chini.

Mhe. Panya Ali Abdalla, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha na kuendeleza jumla ya hekta 1,300 za mipira Unguja na Pemba. Madhumuni ya kuanzishwa kwa mashamba hayo ni kuongeza mazao ya biashara na kuongeza fedha za kigeni. Aidha, mashamba ya mipira hivi sasa yanakodishwa kupitia Wizara ya Fedha, Kampuni ya *AGROTEX Ltd* ya Zanzibar ndio iliyokodishwa na fedha zinaingia serikalini moja kwa moja. Jukumu la Wizara ya Kilimo na Mali asili ni kuhakikisha kwamba mipira inadumishwa na inaendelezwa vizuri.

Mhe. Spika, tatizo la viwavi jeshi linapotokea serikali inachukua hatua za dharura za kupiga dawa bila ya malipo. Suala la kunguni mgunda wakulima wanashauriwa kuweka usafi katika mashamba yao. Aidha, taaluma juu ya matumizi ya mbolea yanayotolewa katika skuli za wakulima zilizoenezwa kila wilaya, na mabwana shamba wanatoa taaluma kwa wakulima kupitia vikundi na mkulima mmoja mmoja, lakini na wakulima nao wanatakiwa wawafuate wataalamu kwa kupata ushauri. Kuna baadhi ya wakulima huwa wanawafuata wataalamu wawape ushauri.

Mhe. Spika, Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe imeweza kuhamasisha wananchi, jamii, juu ya suala zima la uhakika wa chakula na lishe nchini hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

- Uundwaji wa kamati za Wilaya na Shehia za uhakika wa chakula na lishe na kuzipatia mafunzo juu ya dhana ya uhakika wa chakula na lishe na jinsi wanavyoweza kujitosheleza na chakula na lishe.
- Jumla ya kamati 14 (Unguja 10 na Pemba 4) zimeshaundwa.
- Kamati hizi zimeshaunda Mipango kazi yao ambayo imeibua changamoto zinazopelekea kutokuwa na uhakika wa chakula na

lishe. Mipango kazi inahitaji wadau mbali mabali washiriki katika kufanikisha kukabiliana na suala la uhakika wa chakula na lishe katika maeneo yao.

- Mafunzo ya lishe yametolewa na yanaendelea kutolewa katika ngazi ya Shehia, kuwaelimisha wananchi juu ya masuala ya lishe bora na matumizi bora ya chakula kwa lishe na afya.
- Aidha, mipango ya baadae ni kuendeleza kamati za uhakika wa chakula na lishe kwa kila Shehia

Mhe. Spika, suala la kuanzisha utaratibu wa Uhakika wa Chakula ni suala la kitaalamu kweli kweli, kwa sababu unapoweka hakiba kinachowekeka hakiba Mhe. Spika, ni mpunga, huwezi kuweka hakiba mchele, mchele unaharibika, huwezi ukaweka hakiba sukari, sukari inaharibika, huwezi ukaweka hakiba unga wa ngano, unaharibika, tena kwa muda mfupi sana. Lazima vyakula hivi vinavyowekwa kama hakiba basi muda usiwe mrefu, lazima vitolewe na kuuzwa, kwa hivyo vinahitaji utaalamu wa hali ya juu sana.

Wenzetu kule Bara wanaweka hakiba ya chakula kwa kununua mazao kwa wakulima; wananunua mpunga, mahindi, ngano nzima ambavyo vinawekeka, lakini ukiweka unga wa ngano muda mfupi tu unaharibika. Kwa hivyo, ni utaalamu wa aina yake na ndio maana wanafanya utafiti katika kuona kwamba chakula kitachowekwa hakiba kikae kwa muda mrefu. Sisi tukijitizama sana tutaona labda tutataka kuweka hakiba mchele, mchele hatutoweza kuweka kwa muda mrefu. Kwa hivyo, tunachotaka kufanya ni kukiendeleza kilimo ili tuvune mazao na maganda yake tuweze kuweka katika maghala kama vile Nabii Yussuf alivyowaelekeza watu wa Misri wakati ule, kwamba wanaweza kuweka chakula kikawa ndani ya maganda yake na mashuke yake sio kuweka chakula kikaharibika mara moja hii inakuwa haifanyi kazi vizuri.

Mhe. Spika, namjibu Mhe. Asaa Othman Hamad kwamba, ni kweli kwamba kituo cha Matangatuani na vyengine vya utafiti vina matatizo mengi, hili tunakubali Mhe. Asaa, lakini serikali inahitaji kuviboresha hivi karibuni. Wizara imepeleka wataalamu wenye shahada ya pili ili waongeze nguvu, katika bajeti ya mwaka huu wizara imetenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya maabara na ununuzi wa vifaa. Mwaka huu tunataka tuiboreshe ile maabara iwe nzuri kabisa ya Matangatuani.

Sambamba na hayo Wizara inafanya mazungumzo ya kupata misaada kutoka mashirika ya ndani na nje kwa ajili ya kusaidia kituo hicho. Mikakati ya wizara ya muda mfupi na mrefu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji maji, mradi wa EXIM Bank ya Korea kwa kutayarisha hekta za kumwagilia maji ni sawa na asilimia 57 na

zinatumia uvunaji wa maji ya mvua, tukiukuza huo basi itakuwa tunapata nafasi nzuri. Hii ni kujengwa mabwawa yafuatayo:-

Kilombero nataka lijengwe bwawa la maji ya Mto Mkiwa, Kibokwa tujenge bwawa la maji ya Mto Mgambo na Kibokwa tena maji ya Mto Pweza, Chaani maji ya Mto Bwabwaja na Mlemele maji ya Mto Mlemele, Makwararani maji ya Mto Makwararani lazima tuyahifadhi maji haya tuyaweke mahala ili tuweze kuyavuna.

Mradi wa kuendeleza uimarishaji wa mbegu nao pia utaendeshwa kwa kutumia uvunaji wa maji ya mvua hasa kwenye mabonde yafuatayo:- Dobi kwa maji ya vyanzo vya Chemsa ya Renguni, Taifu na Kekewani Kisiwani.

Uendelezaji wa zao la minazi uko vipi? Zao la minazi linapewa umuhimu kama zao la mikarafuu, wakulima kupatiwa miche bora pamoja na taaluma ya upandaji na utunzaji wa miche hiyo. Wizara inawaomba wakulima kuacha kuvuna madafu yasiyokuwa ya kitamli. Uvunaji wa madafu unaudhoofisha uzazi wa minazi.

Mhe. Spika, kulikuwa na swali kwamba kwa nini maeneo ya kilimo yanavamiwa na serikali haichukui hatua? Mhe. Spika, maeneo ya kilimo yako katika hali mbili, maeneo yanayomilikiwa na watu binafsi ambayo utaratibu wa umiliki na matumizi upo kwa mmiliki mwenyewe na ya pili maeneo yanayomilikiwa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo. Wizara inachukua jitihada za makusudi za kuyapima maeneo hayo pamoja na kuyapatia hati miliki kwa mashirikiano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, katika suala hili nataka kusema jambo moja, mimi nimefurahi sana na kusikia kauli hizi kwamba tuyalinde maeneo ya kilimo hasa kwa kuwa ni Waziri ninayehusika na masuala ya ardhi, maana ninapata tabu sana. Kwa sababu unaposema unachukua hatua katika eneo ambalo la kilimo lisijengwe basi unapata tabu sana kutoka kwa watu mbali mbali, tukakae wapi, tuishi wapi, iwe vipi, maneno tele yanakuja napata tabu sana mimi, lakini kama Baraza hili litakuwa linatilia mkazo na wananchi wakasikia kwamba tutunze maeneo ya kilimo na sasa hivi yasijengwe, wizara yangu itapata nafasi ya kuzidi kuyalinda maeneo haya na ninategemea Baraza hili litaniunga mkono wakati ninapochukua hatua hizo za kuyalinda maeneo hayo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ambaye alichangia kwa maandishi kuhusu hifadhi ya chakula kuwa ni dhahiri kwamba wizara inahitaji kupanga vizuri katika kutekeleza jukumu hili. Tumeshazungumza masuala haya, hatua zilizochukuliwa na wizara nishazitaja ambapo ni uchambuzi yakinifu juu ya uhifadhi wa chakula, kazi hii

imekamilika na imeshawasilishwa serikalini. Utayarishaji wa miongozi ya kusimamia na kuendesha hifadhi ya chakula miongozo hiyo tayari imekamilika kwa kutumia. Uanzishaji wa mfumo wa ukusanyaji wa uchambuzi wa taarifa za masoko na makundi ya watu wanaoishi katika mazingira hatarishi ya ukosefu wa chakula umekamilika na mafunzo kwa watumiaji yanaendelea kutolewa.

Mhe. Spika, uanzishaji wa maghala ya akiba unahitaji kuwepo kwa mifumo na hatua tulizozitaja hapo juu. Kutokana na kukamilika taratibu hizi, wizara itaendelea na taratibu za ukarabati wa maghala kama ilivyoainishwa katika hotuba ya bajeti.

Mhe. Spika, chakula lazima tuhakikishe tunakipata hapa ndani na kama tunanunua basi tunanunua chakula kinachokubali kukaa, tusinunue chakula ambacho hakikubali kukaa kama vile unga, sukari ambavyo vitaharibika muda si mrefu.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kufafanua hoja mbali mbali nataka kuzungumzia juu ya masuala ya Mhe. Suleiman Hemed Khamis kuhusu hoja ya jambo gani linalokwaza katika utekelezaji wa kazi za Chuo.

Mhe. Spika, majukumu makuu katika utekelezaji wa kazi za Chuo kama yalivyoainishwa katika sheria nambari 5 (2007) ya kukianzisha Chuo cha Kilimo Kizimbani; ni utoaji mafunzo kufanya utafiti kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Mali asili. Chuo kinatekeleza haya kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Utekelezaji wa kazi hizi unaimarishwa siku hadi siku kwa kuwapatia walimu mafunzo na kukipatia chuo vifaa vya kisasa vya mafunzo.

Hoja ya kwamba wizara inachukua hatua gani kudhibiti maradhi ya mimea na mpunga? Wizara inatoa taaluma kwa wakulima juu ya mbinu sahihi za kukabiliana na maradhi ya mimea ikiwemo mpunga. Mbinu hizo ni pamoja na kutumia mbegu bora zenye kustahamili maradhi, kupanda kwa wakati, kutumia njia sahihi za umwagiliaji, kuhudumia mashamba yao kwa wakati, kutumia viwango sahihi vya mbolea na kutumia madawa ya kukinga na kudhibiti maradhi.

Hoja ya maeneo ya zamani mikarafu ilishamiri na uzalishaji mzuri, lakini sasa mikarafuu inaonesha imekufa. Jee wizara imepelekewa maeneo ambayo mikarafuu imekufa kutoka kwa wasimamizi.

Wizara inaelewa maeneo mengi ambayo yalikuwa na mikarafuu hivi sasa imepungua kwa sababu mbali mbali ikiwemo maradhi na uzee. Wizara inazalisha miche kila mwaka kuziba maeneo yaliyo wazi. Pia hivi karibuni mashamba yote yaliyokuweko Wizara ya Ardhi yamehamishiwa Wizara ya Kilimo, na kwa sasa wizara inahakiki mashamba hayo hali yake ikiwa ni pamoja na idadi ya mikarafuu iliyomo ili iweze kupanga hatua za kurudishia.

Mhe. Omar Ali Shehe yeye aliuliza masuala kuhusu wizara inachukua hatua gani kibajeti katika kuimarisha uwezo wa Idara ya utafiti. Wizara inaelewa umuhimu wa sekta ya utafiti, hivyo inafanya jitihada za kutoa fedha za maendeleo na za kazi za kawaida katika kuimarisha kazi za utafiti. Sambamba na hilo, wizara pia inatafuta misaada kwa waliosaidia kwa ajili wa kujenga miundombimu ya utafiti na kupata fedha za kufanya utafiti, mfano *USAID*, *IAEA*, *COSTECH* na kadhalika.

Mhe. Spika, ni kweli utafiti si kitu cha masihara; ni kitu ambacho lazima tukifanyie kazi kweli kweli. Mhe. Spika, ingawa Zanzibar haijabahatika kuwa na wanyama pori wakubwa kwa ajili ya Utalii. Hata hivyo, wanyama wetu tulionao ni kivutio kikubwa cha Utalii. Wizara ilisimamia hifadhi ya wanyama kwa ushirikiano na wanajamii kupitia kamati za hifadhi na shehia za hivi sasa wanajamii wanashirikishwa na Kampuni za wawekezaji wa kitalii kufanya uwindaji wa kitalii ambapo mapato yake yanagaiwa kwa wananchi wa serikali. Halikadhalika wanajamii wanaozunguka misitu ya hifadhi wanashirikishwa katika uhifadhi wa misitu. Ni kweli kuna tatizo la wadudu wa matunda nimeshalijibu kabisa na Mhe. Naibu Waziri amelizungumza vile vile suala hili.

Suala la kilimo cha Mikarafuu Mhe. Spika, nimeshakizungumza kwa hivyo sitaki kurejea tena hapa katika mazungumzo yangu. Uhakika wa chakula nishazungumza na nimeshafafanua sitorejea tena. Mhe. Suleiman Hemed nimeshamjibu.

Mhe. Omar Ali Shehe wizara imeona umuhimu wa utafiti, hivyo inafanya jitihada ya kutoa fedha za maendeleo na za kazi za kawaida katika kuimarisha hifadhi ya utafiti. Sambamba na hilo wizara pia inatafuta misaada kama nilivyokwishajibu awali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba Sheria ya Misitu iliyotayarishwa takriban miaka 17 iliyopita (mwaka 1996) ina mapungufu. Wizara ya Kilimo na Mali asili imeliona jambo hili na hivi sasa Sheria hiyo imeanza kufanyiwa marekebisho katika ngazi ya wizara. Kasi ya kufanya kazi hiyo imepungua kutokana na wizara kusubiri matokeo ya Sensa ya Miti (*Woody Biomass Survey*) ambayo itatoa mchango mkubwa

katika marekebisho hayo. Sensa ambayo inategemewa kukamilika mwezi Oktoba 2013.

Mhe. Spika, napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kazi ya marekebisho ya Sheria hiyo itakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mhe. Omar Ali Shehe pia anauliza suala la wizi wa mazao ni tatizo kubwa ambalo linawakabili wakulima wetu. Mhe. Spika, suala la wizi wa mazao ni tatizo kubwa ambalo linawakabili wakulima wetu hapa Zanzibar. Katika kuliona hilo wizara ilifanya uchunguzi juu ya suala hili katika wilaya zote za Zanzibar ili kujua hali halisi ya tatizo hilo pamoja na kupendekeza njia za kuweza kulipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, matokeo ya uchunguzi huo yaliwasilishwa Baraza la Mapinduzi kwa lengo la kutolewa maamuzi. Hata hivyo, Mhe. Rais wa Zanzibar alitaka ripoti hiyo iwasilishwe katika kikao maalum ambacho kitajumuisha Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Askari Polisi pamoja na Masheha wote wa Zanzibar kulizungumza kulipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Shamba la Makurunge. Wizara ya Kilimo inaendelea na hatua za kufuatilia upatikanaji wa hati miliki ya Shamba la Makurunge kwa ajili ya matumizi ya Chuo cha Kilimo Kizimbani. Hatua zilizochukuliwa ni hizi zifuatazo:-

Kufanya kikao cha pamoja kati ya Waziri wa Kilimo na Mali asili wa Zanzibar na Waziri wa Ardhi na Mipango Miji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo wenzetu walitoa pendekezo la kutoa eneo jengine. Mhe. Naibu Waziri ameshalizungumza suala hilo. Napenda kuwahakikishia Wajumbe tu kwamba, ruhusa ya kupewa hati miliki Chuo cha Kizimbani imeshatoka, na hivi sasa Chuo cha Kizimbani wanafuatilia ili hati miliki hiyo ya shamba lile la Makurunge waipate.

Mhe. Asha Abdu Haji anasema Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Programu ya Miundombinu ya masoko, kuongeza thamani na huduma za kifedha vijijini imejipanga kuwawezesha wazalishaji wa ndimu wa ukanda wote wa Mashariki ya kisiwa cha Unguja ili kuyafikia masoko kupitia mchakato wa taaluma na mnyororo wa thamani (*value of chain*). Taaluma hii itatolewa na wawezeshaji kutoka sekta binafsi kwa vikundi au Jumuiya za Wazalishaji wa ndimu.

Aidha, programu hii tayari imeshafanya mazungumzo na baadhi ya wazalishaji na kukusanya taarifa za msingi ikiwemo Jumuiya ya

JUAMIJICHWA ya Chwaka na JUWAMIUPWA ya Shehia ya Dongwe ukanda wa pwani. Haya mambo yanaendelea kufanywa sasa hivi.

Mhe. Asha Bakari Makame napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa maelezo yaliyotolewa kwenye kitabu cha bajeti kupitia idara mbali mbali zinajumuisha idara hizo kwa Unguja na Pemba, na hivyo utekelezaji wake huwa unaripotiwa kwa pamoja.

Mhe. Bi Asha hayupo lakini kwa kweli ukiisoma ile hotuba yenyewe tangu mwanzo imezungumza mambo yatakayofanywa Unguja na Pemba, halafu kule mwisho kumetajwa yale matumizi ya kawaida tu kama ilivyo katiba baadhi ya sehemu nyengine.

Mhe. Mussa Hassan. Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa mazao ya nafaka humea vizuri maeneo ya maweni na hivyo Mkoa wa Kusini Unguja una eneo linalofaa kwa kilimo hicho. Hivyo basi, Wizara ya Kilimo na Mali asili inafanya juhudi za kuzalisha mbegu za nafaka kama mahindi, mtama, kunde na chooko. Mbegu hizi huuzwa katika vituo vya kilimo. Hata hivyo, ni wakulima kidogo sana ambao wanatumia fursa hiyo, na hivyo kupelekea mbegu nyingi kuharibika bila ya kuuzwa.

Vile vile napenda kumjibu Mhe. Ashura kama ifuatavyo:-
Utaratibu unaotumika katika kumwagilia mpunga ni kutumia majaruba ambayo yana uwezo mkubwa wa kuhifadhi maji, na hivi sasa kuna teknolojia mpya inayoitwa *SRI* (*System of Rice Intensification)* ambapo maji huwekwa ardhini inapofika *field capacity* hii ni utumiaji wa maji kidogo kabisa kulingana na hali ya udongo na uwezo wa mmea kunywa maji.

Aidha, kilimo cha umwagiliaji maji kina tija kubwa na kinalipa gharama zote za uzalishaji, ambapo wastani wa uzalishaji kwa hekta ni tani sita hadi nane kulinganisha na kilimo cha kutegemea mvua, ambapo uzalishaji ni tani 0.8 kwa hekta.

Mhe. Spika, kuna suala limeulizwa hapa juu ya upandaji wa miche ya mikarafuu Unguja na Pemba, na hii kama sikosei ameuliza Mhe. Subeit Khamis Faki. Kwa hivyo, serikali imeanzisha utaratibu maalum wa ufuatiliaji wa kuanzisha buku maalum la ufuatiliaji ambapo wakulima wote wanaopatiwa miche kutoka katika kila vitalu vya serikali wanarikodiwa pamoja na taarifa zao muhimu, na baadae miche hiyo hufuatiliwa kwa kujua maendeleo ya mkulima huyo.

Mfano tathmini ya miche iliyopandwa mwaka jana Kiwilaya ni kama ifuatavyo:

Kisiwa	Wilaya	Miche iliyopandwa	Miche ilyobakia	Asilimia ya miche iliyoota
Unguja	Kaskazini A	4069	639	16
	Kaskazini B	2318	982	42
	Magharibi	9632	3299	34
	Kati	8499	3694	43
	Kusini	700	300	43
	Jumla	25218	8914	35
Pemba	Mkoani	1170	603	51
	Micheweni	3740	2076	55
	Wete	544	291	53
	Chakechake	140	56	40
	Jumla	5594	3026	51

Mhe Spika, tuna kazi ya kuwaelimisha wananchi juu ya upandaji wa mikarafuu ili iwe inamea. Hata hivyo, kwa upande wa miche ya misitu iliyopandwa, asilimia 80 ya miche hiyo imeweza kustawi. Ili kujua mikarafuu iliyopo nchini hivi sasa Wizara ya Kilimo inaendelea na SENSA YA MITI ambayo matokeo ya utafiti huo utaonesha idadi sahihi ya mikarafuu na umri wake pamoja na miti yote kiujumla.

Kufa kwa mikarafuu kunatokana na:

1. Maradhi ya *Sudden Death* na *Die back* kwa mikarafuu mikubwa,
2. Hali ya hewa iliyotokana na jua kali kwa kipindi kirefu
3. Utunzaji mbaya wa mashamba ya mikarafuu kwa baadhi ya wakulima
4. Tatizo la mdudu mchwa kwa baadhi ya maeneo wanakata mizizi ya mikarafuu midogo
5. Uingizaji wa wanyama katika mashamba ya mikarafuu nalo hili pia ni tatizo.

Mhe. Asha Abdu Haji ameuliza juu ya Msitu wa Hifadhi ya Jamii wa Kajengwa kutaka kujengwa Chuo cha Polisi.

Msitu wa Hifadhi ya Jamii wa Kajengwa ni miongoni mwa misitu 45 ya jamii ambayo ipo chini ya usimamizi wa jamii. Utaratibu wa uendeshaji wa misitu hiyo inajumuisha utengenezaji wa maeneo ya matumizi ya jamii, maeneo ya makaazi, maeneo ya hifadhi ya hali ya juu ya maeneo ya kilimo.

Kwa vile suala la ujenzi wa Chuo cha Polisi ni suala la Kitaifa na la kimaendeleo, ni vyema kutenga sehemu ya eneo hilo kwa ajili ya suala hilo muhimu la Kitaifa na eneo lililobakia kuendelea kusimamiwa na wanajamii wa Kajengwa.

Mhe. Spika, napenda kumwambia Mhe. Asha Abdu kwamba si eneo lote la Kajengwa la msitu ule linataka kujengwa Chuo cha Polisi, lakini Chuo cha Polisi kina manufaa makubwa sana katika maeneo yale, kutafunuka kule Mheshimiwa na kutakuwa wazi kabisa, angelipita *Kilwa Road* pale akaona Chuo cha Polisi kilivyokaa pale. Sasa tukiwa na Chuo chetu cha Polisi hapa itakuwa vizuri zaidi kuliko sasa hivi tunavyotumia Chuo cha pale Ziwani hatufikishi mahala popote, na hatuchukui msitu wote ule, msitu bado upo na msitu huo wanaweza kuunganisha na hiyo sehemu ambayo wanataka kuwapa hivi sasa Polisi, wanaweza wakaongeza ni eneo ambalo lina msitu mkubwa umekwenda mpaka Muyuni kule msitu ule, na wanaweza wakaendelea kuutumia na kuutanua kila siku.

Hii naomba Mhe. Spika, isiwe hoja tunapopata maendeleo kama haya tusiyapige teke. Polisi wameshasema kama watu wa Kusini hawataki tujenge tunakuombeni mtupeleke Kati, sasa kwa sababu mimi natoka Kati sitaki kutilia mkazo suala la kwenda Kati, lakini wakikataa Kusini Kati nitachukua tutajenga Chuo cha Polisi nafasi tunayo sisi. Tuna uwanda wa Umbuji pale uko wazi kabisa naweza kuwapeleka, lakini mimi siwezi kuwa msemaji mzuri katika hili ni wenyewe, Kusini wameshapata hiyo bahati mimi ningewaomba waitumie bahati hiyo, hawaitaki nitachukua Kati uamuzi ni wao.

Na la pili kule Matemwe vile vile kuna sehemu tunajenga kitu kama hicho nako pia wameshapata hiyo nafasi kule waitumie vizuri, wakikataa basi watu wengine watachukua. Halafu usije kusema kwamba kilikuwa kijengwe hapa kile lakini kiko kule wakati watu wanafaidika. Hili ndilo tatizo letu Mhe. Spika, katika masuala yetu ya maendeleo.

Mhe. Spika, Mhe. Salim Abdalla Hamad, tupande miti kwa wingi ili tuweze kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na upunguaji wa hewa ukaa. Ushauri wako kupanda miti kwa wingi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi wizara imelichukua na suala hili tutaendelea kuliendeleza kila mwaka. Aidha wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kupitia Idara ya Mazingira, ambayo ndio yenye jukumu la kuratibu suala la mabadiliko ya tabia nchi imeandaa mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Ashura Sharif Ali amezungumza juu ya Idara ya Misitu na maliasili zisizorejesheka, uchimbaji wa mchanga, mawe, kifusi umekubalika kisheria,

uchimbaji wa mali asili zisizorejesheka. Ukweli umekubalika kisheria na utaratibu wake ni kama ifuatavyo:

Muombaji anatakiwa kuwasilisha maombi kwa Shehia na Halmashauri ya Wilaya. Wilaya inawasilisha maombi haya kwa Idara ya Misitu na maliasili zisizorejesheka. Baadae taasisi hii itakuwemo Idara ya Misitu, Ardhi, Mazingira na barabara inatembelea eneo husika na kutoa muongozo nani amekubaliwa na nani amekataliwa kutokana na sababu mbali mbali. Idara kwa hivi sasa imeorodhesha watu 25 kwa Unguja na 7 kwa Pemba. Orodha hii itachukuliwa zaidi ya miaka miwili kukamilika. Idara pia inaorodhesha watu ambao hawajakaguliwa na waliokataliwa na wizara inaendelea kuratibu suala hilo, na orodha niliyoitaja iko katika ofisi yetu na inafuatwa na ziko tayari.

Mhe. Spika, utaratibu wa kupanda miti ya matunda zaidi kama mifenesi, mishokishoki, midoriani kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi. Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kushajihisha wananchi kupanda kwa wingi miti, jambo la faraja ni kwamba wananchi hivi sasa wanapanda miti mingi ya matunda hadi katika maeneo ambayo kihistoria hayakupandwa miti ikiwemo upandaji wa miembe katika maeneo ya maweni.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imetayarisha waraka maalum ambao utapelekwa Serikalini kwa muongozo wa waraka huo na mikakati madhubuti ya kuendeleza upandaji wa miti ya matunda, misitu na mikarafuu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid kwa nini utumiaji wa misumeno ya moto ni kosa na wakati inasaidia kufanya kazi kwa ufanisi. Mhe. Spika, utafiti tulioufanya unaonesha kwamba Zanzibar tuna misumeno ya moto zaidi ya 400, misumemo hii ni mingi kwa kiasi kikubwa inatumika vibaya katika nyakati mbali mbali hutumiwa wakati wa usiku na katika mazingira hatari.

Mhe. Spika, ili kunusuru nchi yetu ndogo visiwa tu hatuna budi kupiga marufuku kabisa matumizi ya misumeno ya moto, na rasimu ya kanuni mpya tayari imekamilishwa. Ushauri wa Mhe. Mwakilishi tunaupokea lakini ili kuokoa nchi yetu inabidi tupige marufuku ndio maamuzi ya Serikali.

Mhe. Spika, kuna bonde la Chaani aliendeleze kuwa bonde la umwagiliaji maji. Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kwamba wizara tayari imeshaorodhesha maeneo yote yanayofaa kumwagiliwa katika visiwa vya Unguja na Pemba katika mpango mkuu wa umwagiliaji maji.

Aidha katika kisiwa cha Pemba umwagiliaji wa maji umependekezwa ni ule unaotumia maji ya mvua kama vile bonde la Chachaani halina chanzo kizuri

cha wazi cha maji. Kwa mfano mto wa chemchem halikuingizwa katika mpango wa kuendelezwa kwa mabonde ya umwagiliaji maji. Lakini ina dhamira ya kulikumbushia bonde la Chanjaani ili maji yasambazike na waweze kujiongezea kipato.

Mhe. Spika, nimejibu haraka haraka sana na naweza nikakiri kwamba kuna watu wengi itakuwa nimewaacha kama hapa namuona Mhe. Jaku Hashim Ayoub anazungumzia juu ya habari ya msitu wa Ukongoroni na mpaka wa Ukongoroni na Kitogani.

Mhe. Spika, hapa napenda kusema kitu kimoja. Hii nchi zamani ilipimwa na mikataba ipo, zamani kulikuwa hakuna shehia ya Ukongoroni kulikuwa na Shehia moja tu ya Charawe, ila baadae ndio ikaja hiyo ya Shehia ya Ukongoroni. Mipaka ipo kiwandani kuna mpaka pale baina ya Kusini na Kati. Tutajaribu kukutana na watu wanaohusika katika maeneo hayo. Nimejaribu kutizama ramani zetu za zamani na tuoneshe mipaka iliyopo.

Jambo moja tu ninalopenda kulieleza kwamba tunapogundua kwamba eneo fulani ambalo lina rutba. Lakini kwa bahati limekwenda katika kijiji chengine wale wakulima wanaolima katika eneo lile waendelee kulima wasihamishwe. Maana wakulima wale wanaweza kutoka katika eneo jengine lakini wanalima pale waendelee kulima. Lakini mipaka wataendelea kuiheshimu, mikataba ile tuiheshimu. Na sasa hivi wizara yangu mimi Ardhi inajua kwamba wana utaratibu wa kuirejesha mipaka hii ile ya zamani, na kuionesha mle mlimopita kwa kuweka *beacon* zilizosimama sasa baada ya kuweka *beacon* zilizokuweko ardhini ambazo mpaka upekue mwitu ndio uzione. Hizi nazo zitunzwe na ziwepo.

Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub sisi tuko tayari kukutana na watu wa Ukongoroni na watu wa Kitogani tuzungumzie mipaka, na tukifikia makubaliano sisi tutayahifadhi makubaliano hayo na wao vile vile wayaheshimu makubaliano hayo na mpaka utumike ule kusiwe na tatizo lolote.

Mhe. Spika, ardhi sasa hivi mali sana na ina ugomvi mkubwa sana, haya maneno wanayoyazungumza wazee hapa juu ya maeneo yanavamiwa sijui yanajengwa, zamani kulikuwa hakuna mtu anayeuliza uwanda kabisa watu walikuwa hawaulizi. Lakini sasa hivi kila mtu anasema uwanda huu alizikwa babu yangu, huu alizikwa bibi yangu, ndio matatizo tulionayo hayo.

Lakini ardhi ni mali ya Serikali. Kwa hivyo, kama ardhi ni mali ya Serikali itaendelea kubaki kuwa ni mali ya Serikali, na mipaka hii tutaiweka na itaheshimiwa kama kawaida. Lakini wananchi wote kila wanapojisikia kulima

watalima bila ya tatizo lolote, tutajaribu kuwasihi sana wananchi wasigombanie maeneo kuwazuia watu wengine wasilime kwa sababu hii nchi ni yetu sote kabisa.

Mheshimiwa Mwakilishi uungaji wa umeme katika bonde la Machigini umepangwa kufanyika katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2013/2014. Mhe Mohammed Haji Khalid mwaka huu tumepanga kupeleka umeme katika bonde la Machigini, kwa hivyo tegemea sana kwamba utapata.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi ni kweli kuwa wanafunzi wana kawaida ya kwenda *field* kama ni sehemu ya masomo yao. Lakini maeneo hayo wanachagua wenyewe kutokana na sababu zao na huwa wanafahamu kuwa Chuo cha Kilimo hakina kasma ya kuwalipia gharama za nauli na mambo mengineyo, na vile vile aliuliza hapa Mhe. Asha Bakari Makame suala la kwamba mwanafunzi asiyelipa ada huzuiliwa kufanya mitihani. Hii ni katika tikisa ya kufanya hii ada ilipwe kwa sababu ada ndiyo inayowaendeshea masomo wale, bila ya ada masomo hayaendi vizuri. Na kama atafanya mtihani basi matokeo yake hapewi yanazuiwa kabisa mpaka amalize kulipa ada zote anazodaiwa.

Mhe. Spika, waswahili wanasemaje *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma*. Maana utapewa muda uiimbe. Lakini ndio umepewa hicho hicho kipande kimoja tu wewe sasa unakiimba pale lakini huendi mbele umesimama hapo hapo tu. Kwa hivyo *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma*.

Kwa hivyo, nimejaribu kuwajibu Waheshimiwa Wawakilishi kwa kutumia nyimbo ya kufundishwa, mnihurumie tupitishe bajeti ya Wizara hii. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa kufanya majumuisho tena kwa muda mfupi, kwa mashirikiano makubwa na Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili wanyanyue mikono.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Sasa naomba Baraza lako

tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 20 - WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Kifungu 0301 - Ofisi Kuu Pemba 400,000,000/=
Kifungu 0401 - Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilisema mapema kwamba Idara ya Mipango Sera na Utafiti nitakuwa mkaidi sana, na nikazungumza kuhusu wakulima wale wanaolima machungwa. Pamoja na Mhe. Waziri anavyojibu kwamba yeye ana machungwa yake mengi yanayopukutika kuliko hawa. Lakini nikamueleza kama sisi tumefanya ziara kwa makusudi mimi na Mhe. Hija Hassan Hija kwa kuitwa na wakulima na wakaenda kutueleza na wakatuonesha hali halisi ilivyo.

Sasa nilitaka Mhe. Waziri anieleze kama je, watu hawa machungwa yale yanayopukutika, na wakati Serikali ina mipango kabambe ya kuwahamasisha wananchi kilimo hawapati dawa wala hawaendi hata hawa mabwana shamba kukagua.

Kwa maana hiyo nilitaka kujua je, Serikali imewafikiria vipi wakulima wale wanaopata tabu na machungwa yao yanayopukutika. Wewe mwenyewe ukienda utajionea mwenyewe utaona kilio, na hizi picha tulizichukua tena kwa simu tu hizi kama ingelikuwa tuna *camera* basi kila mmoja angelikuwa anaona kilio kwa hali halisi ilivyo. Sasa nataka haya maelezo kama hawa wakulima watawasaidia vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa haya ni mapato na sio matumizi. Sijui kama unakusudia mapato haya yasikusanywe au vipi. Hii ni sehemu ya mapato lakini iko sehemu nyengine ya matumizi ambayo nadhani ndio unayokusudia kuzuia.

Kifungu 0401 -	Idara ya Mipango na Sera	2,000,000/=
Kifungu 0701 -	Idara ya Misitu na Maliasili	310,000,000/=
Kifungu 1501 -	Idara ya Kilimo	15,000,000/=
Kifungu 1701 -	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo	21,000,000
Jumla ya Fungu		**748,000,000**

Kifungu 0401 - Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza. Kwa hiyo, nataka maelezo kwa Mhe. Waziri kwa sababu maelezo nimeshaeleza na pale nilizuia sehemu ya mapato, lakini hapa sasa ndio sehemu ya matumizi. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, naifahamu vizuri hoja ya Mheshimiwa. Juu ya tatizo la nzi waharibifu katika matunda ambao wanasababisha machungwa yetu kudondoka, na hata kama ukiyakuta juu ya mti ukiutikisa ule mti basi yanapukutika.

Jitihada za Wizara ni kuhakikisha kwamba tunaongeza mitego ya nzi hawa. Hiyo ndio jitihada kubwa ambayo tunaichukua. Tunaongeza mitego ya nzi hawa na kuigawa kwa wananchi ili waiweke katika maeneo yale na pia tunataka kushirikiana na Shirika la *Atomic United National* ili itusaidie katika kuangamiza nzi hawa ili wananchi wetu wasiwe wanakula hasara katika maslahi. Kwa hiyo, jitihada hiyo tunachukua na tunayo katika mwaka huu tunaanza ili kuona kwamba suala hilo linakufa.

Sasa tunataka tuwasiliane, na watu wanaofanya *research* masuala haya kama kuna miti ya kienyeji ambayo inaweza kupunguza nzi hawa vile vile iweze kutumia dawa zile za kienyeji ili kuwapunguza nzi hawa katika kuharibu matunda yetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, namsikia sana Mhe. Waziri lakini pamoja na maelezo ya Mhe. Waziri hawa wakulima masikitiko yao ni kwamba hata hao wahusika wakuu hawajapita hata lile eneo wakaenda kuangalia ule uharibifu ulivyo wa matunda yale.

Halafu Serikali ilitakiwa iwasaidie angalau dawa, na nimezungumza kwamba kichupa kimoja cha dawa wananunua kwa shilingi elfu nane, wamenunua hivyo vichupa vya dawa, lakini hata hiyo dawa waliyoelekezwa hazijasaidia, na bahati mbaya mno hawajapita mabwana shamba hakujapita mtu hata mmoja, wataalamu wa kilimo kwenda kuwakagua wakaona hiyo hali halisi ilivyo.

Sasa labda anambie Mhe. Waziri atawasaidia vipi pamoja na kuwa mnasubiri mashirika mliyoyakusudia kuwa wawasaidie. Lakini kama Serikali yenyewe mnachukua juhudi gani kuwasaidia hawa wananchi?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kusema mitego tutaongeza ambayo mitego ndani yake mna dawa, na ile dawa kila baada ya

muda fulani inatakiwa kubadilishwa. Itabidi wakiwa na mitego wajue kwamba dawa yangu ishamaliza muda wachukue jitihada ya kwenda katika kituo kubadilisha ile dawa iliyomo mle ndani. Maana ile dawa inatumika kwa muda maalum, baada ya muda dawa ile haitumiki tena, lazima kibadilishwe.
Sasa jitihada hizi ziende pamoja baina ya Serikali na hawa wakulima wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, Maofisa wa Kilimo wanajua kuwa tatizo la wadudu limo katika maeneo yetu. Na wanajua sana kwamba hata katika baadhi ya maboga vile vile yanaharibika kwa ajili ya Mabungu hawa wanaoharibu matunda vile vile. Hiyo inajulikana vile vile, kitu muhimu ni kuchukua taaluma ya pamoja ndio kufanya kazi sote tusaidiane.

Mimi nina machungwa yangu, machungwa yanapukutika na mimi mwenyewe nitoke niende kilimo, nikasema nipeni ile mitego sasa hivi ili niende nikazuie nzi kule wananiharibia matunda yangu. Na uwahi mapema usingojee mpaka machungwa yanaiva wale wadudu wameshazaliana halafu unakwenda kuomba mitego.

Unajua kwamba hili eneo lina wadudu waharibifu. Mimi niliwahi kuchukua mitego na nikaweka kwangu na niliweka mapema tu. Lakini Mheshimiwa tena ukiwa Waziri ukienda huko mitaani tena ile mitego yote ikachukuliwa wakanambia kuwa Waziri atakwenda kutafuta mingine, machungwa yangu nikala hasara yamepukutika hii imenitokezea kabisa.

Lakini kwa kweli uchukue jitihada mwenyewe kutafuta ile mitego. Sasa ukichukua jitihada basi utafanikiwa hili ni tatizo ambalo tulishughulikie sote. Sisi tutaongeza mitego katika bajeti ya mwaka huu tumeshaanza kuzungumza na Shirika la *Atomic United National* ili litusaidie kupata dawa nyengine inayoweza kutusadia kupunguza. Hizo ndizo jitihada za Serikali katika kuona wananchi tunawasaidia.

Katika biashara Mhe. Waziri wa Biashara ana kitu kinasema kwamba ukiupakia mzigo melini na ikazama hakuna malipo si ndio. Sasa na katika mambo haya pia ipo. Ukilima ukipata hasara sawa wakati ule bila shaka ndio umeshapata hasara. Serikali ifanye jitihada ya kuzuia hasara ile isitokee mara nyengine, hilo ndilo suala muhimu ambalo tunalifanya sasa katika Wizara yetu ya Kilimo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Waziri majibu yake mazuri sana. Lakini unapokuwa unaumwa anapokuja mtu kukujuilia basi unakuwa kidogo unapata nafuu kwa yale matatizo yako yanayokukabili. Lakini sasa wizara na watendaji wote hawajapita hata kwenda kuwafariji wale watu.

Kwa maana hiyo sasa Mhe. Waziri anambie kwanza yeye na watendaji wake watakwenda lini kukagua na kuiona ile hali na kuwafariji wale watu jambo la kwanza.

Pili amesema kama yale machungwa yakipukutika ukayazike. Sasa wananchi hawajui mambo kama hayo, hawajui sasa kama wangelikuwa wanapita wangekuwa wanawaelekeza kama msingoje mpaka mkaathirika zaidi. Lakini Mhe. Waziri unakwenda unakuta mchungwa umezaa machungwa zaidi ya milioni nzima, unakuta mchungwa una machungwa mawili sasa hivi. Yamepukutika yapo chini wananchi wanalia hawajui wafanye nini? Kwa sababu wazee wengine ndio kilimo chao wanachotegemea, mtu mmoja ana mashamba mawili, matatu anategemea yale machungwa, machungwa yale yameshapukutika yote hana tena cha kujisaidia.

Sasa wao wizara hawapiti hata kwenda kuwakagua na wakati Serikali inahimiza kilimo. Sasa lini Mhe. Waziri na watendaji wake watakwenda kuwakagua wao na wawafariji wale watu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa nijitambulishe kama mimi ni mkulima vile vile. Juzi nilieleza kama mimi ni mfugaji lakini pia kilimo cha michungwa kule karibu na eneo la karibu ya Dunga na hata Makunduchi michungwa ninayo na miembe.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Wawakilishi wa eneo lile na huko anakozungumzia yeye tumeshatoa taarifa kuwa mitego ile hata kule Dunga mimi nilipewa bure sikununua hata shilingi moja, na taarifa tumewapa wakulima inatolewa bure waende pale wakachukue katika Idara inayohusika na kilimo. Hili tatizo liko kila pahala wadudu ni hawa hawa wanatoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.

Kwa hivyo, ni suala ambalo tunahitajia sisi tuzidi kutoa taaluma zaidi na maafisa wanaohusika na kilimo. Lakini sisi kama Wawakilishi tumeshawajulisha wakulima wetu kama kuna maeneo ya kilimo na mitego inatolewa bure waende watapewa bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, ninavyozungumza ni kwamba Mhe. Haroun Ali Suleiman kama anavyozungumza yeye ni Mwakilishi wa lile eneo. Lakini mimi nazungumzia watu wa Idara ya Kilimo kwa sababu ni kazi yao watakwenda lini kuwafariji wale wananchi na halafu wataona zaidi. Sasa watakwenda lini wao?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kuhusu taaluma na kuhusu namna ya kuwafariji kwa kuwatembelea ndio anachoomba pale Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa kilimo wako huko huko Kitogani na wanaishi hapo hapo Kitogani na wanazungumza, na wakulima hapo hapo Kitogani wakati wowote na hili tatizo linajulikana. Kweli wamekula hasara lakini pia na kuvuna wamepata, wamevuna kidogo.

Sasa suala la kufanya ziara hilo ni jukumu la mawaziri kufanya ziara katika maeneo hilo nalikubali. Mimi nakubali kwamba ni hasara imetokezea ya machungwa na hayakutokea Kitogani tu wala Makunduchi yametokea karibu nchi nzima. Ndio maana wizara yangu inachukuwa jitihada ya kuhakikisha kwamba inaongeza mitego kwenye msimu huu na inatolewa bure ili kuweza kurekebisha suala hili ili kusaidia kupunguza uharibifu wa nzi hawa wanaofanya katika maeneo yale.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, siwezi kutafuta jibu jengine maana yake kama kwenda kuwafariji kwa pesa hiyo ni makisio tufanye. Lakini hatuna makisio mpaka sasa hivi ya kufanya kuwafariji kwa pesa na wala siwezi kutoa ahadi kwamba kaharibikiwa na machungwa tutamlipa pesa. Siwezi kutoa ahadi katika hilo isipokuwa tunajua tu kwamba hasara imetokea, tunataka tuongeze mitego tunazungumza na Shirika la *Atomic United National* lisaidie kutafuta njia nyengine za kuwadhibiti wadudu hawa, halafu vile vile na wananchi nao kwa upande wao wasaidie katika kuzika machungwa ili kupunguza ile hasara.

Kwa sababu hata wale nzi unaowanasa katika kile kibati kile kwa sababu unaweza kuweka kibati. Sasa hivi basi ukija jioni ukaona kimejaa mpaka juu. Usiwamwage uchimbe shimo uwazike, ukiwamwaga maana yake unasababisha tatizo liendelee kuwepo tena ushawapata ndani ya kopo unatakiwa uchimbe shimo uwazike. Na machungwa yale yaliyoliwa uyazike ndio kilimo kupitia katika hatua hizi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit Khamis Faki maelezo ndio hayo juhudi za Serikali ndio hizo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, waziri mimi nnamfahamu sana anavyozungumza. Lakini nimezungumza kama yeye na watendaji wake watafanya ziara lini kwa sababu watakapokwenda wale wananchi wengine hawajui kama machungwa yanazikwa yakishakuwa yana matatizo. Lakini watakapokwenda ndio watatoa elimu zaidi na hiyo mitego anayozungumza Mhe. Waziri kama iko mitego watu wanaitafuta, haipo, kwa sababu yeye Mhe. Waziri anasema mitego anataka iongezwe, kwa sababu haitoshi.

Sasa hilo watakapokwenda watendaji watazidi kuwaelekeza watu na kuwapa maelekezo na wao wenyewe watajisikia raha kama watendaji wamekuja, na kama wapo watendaji Kitogani hawajaenda hata siku moja huko. Sisi tumekwenda jana na Mhe. Hija Hassan Hija tumerudi hawajaenda hata mmoja. Wapo kweli huko Kitogani lakini hawajaenda.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri nitoe maelekezo tu kama anavyosema yeye mwenyewe Mhe. Waziri kwamba taaluma izidishwe mabwana na mabibi shamba watembelee kwa karibu zaidi na viongozi wengine hata Waziri mwenyewe. Naibu Waziri wanaweza wakatembelea maeneo haya hilo ndio la msingi. Na nafikiri katika hili Mhe. Waziri unakubali mashauri hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, bila ya kufanya hivyo maana yake hatufanyi kazi, lazima twende mimi nakubaliana kabisa ni ziara ya kawaida ambayo inafanywa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri ameshakubali atakwenda basi atakwenda kujionea yeye kwa macho yake na atawapa maarifa zaidi. Nakubali tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, alipojibu Mhe. Waziri wala usije kufikiria kama sipo mimi nilikuwa nipo ofisini kwa bi Moza na nimefahamu sana Mhe. Waziri.

Hoja yangu hivi sasa watu wa Ukongoroni tayari wameshafyeka ile miti na iko kwa Sheha, na hii hali tukiiachia malumbano yatazidi na wote jamii moja watu wa Ukongoroni na Kitogani wote ni wamoja, ni ndugu. Alisema tutakaa tukakwenda na huku wakati wa Ramadhani sijui tutakaa lini.

Nataka anambie lini tutakaa ili twende, lakini tukiiachia hii hali tutakuja kupigana mapanga pale Mungu asijekujaalia ikafikia hatua hiyo na watu wa Ukongoroni inaonekana hii sijui kama ni tabia au vipi, maana yake juzi juzi ilikuwa kesi na Marumbi leo wameshaingia eneo la Kitogani Uwandani. Mhe. Waziri kwa unyenyekevu kabisa nahitaji maelezo yako.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri lini mtakaa ili kutatua hayo matatizo ya mipaka.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni kwamba suala hili si suala la Kilimo peke yake. Wizara ya

Kilimo pamoja na Wizara ya Ardhi twende pamoja tukakae kitako tuoneshane mipaka. Hilo tutakwenda lakini kwa siku tisa hizi zilizobakia za Ramadhani ambazo zina mambo mengi, kuna mialiko ya futari, kuna wengine tunafutarisha, siku hizi lazima zimalizike. Kwa hivyo, baada ya sikukuu tukijaaliwa hapa Mwenyezi Mungu akipenda tutakwenda sisi Ukongoroni hatusemi kama tutakwenda kesho.

Mhe. Naibu Waziri hodari sana kutembelea akisikia kuna matatizo. Kwa kweli kazi kaipata *late* tu, lakini kama angesikia mapema angelikuwa keshakwenda zamani maana alisikia kuna mgogoro wa mchanga Kaskazini huko kaenda upesi upesi kwenda kuliona hasa tatizo liko vipi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sisi tukishamaliza mwezi wa Ramadhani tunaomba kwanza wastahamili tumalize mwezi huu, hili suala tutakwenda, tutazungumza. Lakini tunachotaka makubaliano tutakayofikia yaheshimiwe na yakubaliwe. Nina hakika tutafikia makubaliano, makubaliano tutakayofikia yaheshimiwe na yakubaliwe, nina hakika tutafikia makubaliano hakuna kisichozungumzika Mhe. Mwenyekiti, tutazungumza na tutafikia makubaliano.

Jambo moja tu hatutounga mkono kuwafukuza watu wanaolima; wanapata chakula chao tuwafukuze hilo litakuwa tatizo kidogo, kwa hiyo wazee kule watukubalie kwamba mtu anapolima analima anapata chakula chake ardhi yetu ndio hii hii, watu lazima wapate chakula katika maeneo haya haya, lakini mpaka tutaoneshana huu hapa mpaka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti narudia tena kwa sauti ya chini kabisa, hapa mpaka Kitogani hapafiki hata dakika 25 Mungu akitujaalia, muda aliouweka ni mbali na hali inazidi kuwa tete. Mimi ningelimuomba kwa heshima na taadhima tungefanya kama itawezekana japo kesho au Jumamosi wakati hakuna kazi tukaenda, lakini hali mbaya baada ya kutoka nje tu mimi Mhe. Mwenyekiti, nimepokea simu karibu tatu, hali hairidhishi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, usiniharibie kikao changu kwa kuondoka baadhi ya Wajumbe, tunakuja na utaratibu hapo baadae mpaka Jumamosi tutatumia. Sasa nadhani ukubaliane na kile alichokisema kwamba mara baada ya mfungo huu wa mwezi mtukufu wa Ramadhani wewe mwenyewe binafsi Mhe. Jaku Hashim, fanya juhudi mkakumbushane mpange siku ya kwenda huko, lakini katika kipindi hiki cha kuanzia leo hii mpaka tarehe 6 aah! Hapo sitaki kiingie kitu kingine. Maana kikiingia mambo mengine hapo mtanipunguzia *quorum*, na kwa kweli shughuli zetu zinaweza zikaenda vibaya. kwa hiyo chukua juhudi uwasiliane na Wizara ili mupange siku baada ya mwezi mtukufu wa Ramadhan. Hilo kila mmoja anajua

umuhimu na jinsi tulivyokuwa tuna shughuli nyingi katika kipindi hiki, kwa kweli si vyema kuingiliana na masuala mengine. Nadhani baada ya maelekezo hayo Mhe. Jaku ukubali tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi sina tatizo Mhe. Mwenyekiti, kwa vile umezungumza mtu mzima na nitakuwa sina adabu kama sijakuheshimu wewe Mhe. Mwenyekiti, lakini tu anambie tunapokwenda tunakwenda na yeye na Wizara gani maana ikifike siku ile tatizo hili tulijue maana yake, anitajie tu baada yeye kama ni Waziri wa Ardhi na vile vile anakaimu Waziri wa Kilimo itakuwa kheri pamoja jiwe moja tutapiga ndege wawili. Sasa aniambie tu atakwenda yeye kwa niaba ya Wizara zote mbili au kuna Wizara nyengine itaongezwa katika mjadala huu.

Mhe. Mwenyekiti: kama ulimsikia sawa sawa shughuli hii alisema kwamba si tu kwa Wizara ya Kilimo bahati nzuri kumbe ni yeye vile vile ni Waziri wa Ardhi, sasa kiutaratibu utafika kwa Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo na wewe mwenyewe Mheshimiwa ili muende huko mukaifanye hiyo kazi, sasa nani atakwenda hiyo mtapanga pamoja huko tusipange hapa ndani ya Baraza.

Kifungu 0401

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu kilimo cha ndimu Dongwe. Kilimo cha ndimu Dongwe hawana soko, ndimu zile ningeomba Wizara kwamba iwapatie angalau kiwanda kidogo japo kuwa cha kusarifu tu zile ndimu angalau na wao wajipatie mahitaji yao.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi pale kwamba sasa tuna *pilot project*, tunajenga kiwanda kwa kushirikiana na *UNIDO* pamoja na wananchi wa Chwaka na natarajia mwaka huu kitamalizika na kitaanza, na kikianza kazi tutaangalia ule mradi utakavyokuwa, kikiwa na mafanikio basi *pilot project* zile zitaendelea katika maeneo mengine kwamba wanatoa ndimu nyingi hazina soko. Kwa hiyo atuvumilie kidogo hichi kiwanda wakati wowote kinaweza kikaanza kazi.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera 449,549,000/=
Kifungu 0402

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nimemueleza Mhe. Waziri kwamba kuna tatizo la upandaji wa miembe katika Bonde la Mpunga la Mbuzini pamoja na lile la Mtwangeni pale. Katika majibu yake aliyojibu alimjibu mtu ambaye alizungumzia mjengo wa nyumba

katika maeneo ya kilimo, lakini mimi nilikuwa nazungumza zaidi katika masuala ya upandaji wa miembe katika mabonde ya mpunga. Sasa nilikuwa nataka tu anieleze pengine haya mabonde ya Mbuzini pamoja na Mtwangeni ni miongoni mwa mabonde ambayo yanamilikiwa na wananchi ama vipi, hilo nataka nijue. Lakini kama itakuwa bado mabonde haya yanamilikiwa na Serikali sijui kama Wizara yake sasa imetoa ruhusa ya wananchi kubadilisha kilimo hicho cha mpunga na kulima miembe ama na minazi tena kule kwa sasa ama vipi. Mheshimiwa naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unakusudia kwenye Chuo hichi cha Kilimo maana hapa tunazungumzia Chuo sasa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Samahani hii ripoti itakuwa nimeitoa kwengine, samahani naomba niweke sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Haya nimekusamehe.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, katika Chuo cha Kilimo Kizimbani nilichangia mambo mengi tu lakini ninamshukuru Mhe. Waziri, amenipa ufafanuzi. Ila katika suala la vifaa vya kufundishia pale Chuoni nilizungumza zaidi kuhusu suala la trekta; nilimwambia Mhe. Waziri, kwamba kwa masomo wanayofundishwa chuoni pale yanahitaji kusomwa kwa vitendo, kwa hiyo kwa mfano somo *agri-merchanisation* linahitaji hasa kwamba wanafunzi wale liwekwe trekta la kuwafundishia wanafunzi ili waweze kusoma kwa vitendo, lakini pia watu wale watakapoajiriwa kama mabwana shamba basi waweze angalau kuwasaidia wakulima wengine wadogo wadogo katika yale maeneo ambayo wanakwenda. Lakini Mhe. Waziri katika majibu yake hapa alisema kwamba kuna *semi trailer* mbili zitapelekwa pale. Tunachotaka sisi hapa trekta kwa sababu wanasoma kwa vitendo na hawawezi kuwasaidia watu wengine ambao watakuwa na matrekta katika yale maeneo, hilo la kwanza.

La pili, kuna suala la malimbikizo ya mishahara pamoja ya miezi kama mitano hivi ya wafanyakazi wa Chuo kile, wafanyakazi wa kawaida pamoja na walimu. Suala hili bado sijapata ufafanuzi wake, kwa sababu suala la kudai haki ni suala zito na watu hawa tunawategemea watusaidie kwa wanafunzi wetu, ambao baadae wawe wataalamu, suala hili sikupata ufafanuzi kwamba lini watu hawa watafanyiwa marekebisho ya hayo madai wanayoyataka.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika Chuo hiki hiki kwa haraka, keshokutwa Mhe. Rais wa Zanzibar atakuwa mgeni rasmi katika sherehe za nane nane kule. Kwa hivyo nilitaka kujua hapa kwamba hii wizara imejipanga

vipi na pengine chuo kitawapeleka watu wangapi ambao watashiriki. Vile vile nataka nijue chuo cha kilimo wanalo banda lao kule kwa mwaka huu.

Suala la mwisho Mhe. Mwenyekiti, ni suala la kisima, tulizungumza kuwa kuna tatizo la maji na Mhe. Waziri alisema kwamba tayari ameipa Mamlaka ya Maji kuchimba kisima hiki. Lakini Mhe. Spika, ukweli uliopo kwamba Mamlaka ya maji waliwatafuta watu wengine na watu hawa wanachimba kisima kwa kutumia mikono yao. Sasa kuna siku Mhe. Waziri huyu nilipomuuliza suala la uchimbaji kisima katika Jimbo langu aliniambia magari hayapo kwa wakati ule, lakini kumbe Mamlaka ya maji hivi sasa inachimba visima kwa kutumia mikono, pengine na mimi angenisaidia. Lakini hapa zaidi nataka atuhakikishie je huo uchimbaji wa kisima cha taasisi ya serikali kitakachochimbwa kwa kutumia mikono, atatuhakikishia vipi usalama wa kisima hicho, lakini pia upatikanaji wa maji na ubora wa hicho kisima. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kwa hoja zangu hizi hapa nne.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, katika jibu nilizungumzia suala la upungufu wa vifaa, nilisema kwamba wizara imechukua hatua ya kukiimarisha Chuo hicho kwa kutenga na kutoa fedha za ruzuku pamoja na kuwasiliana na washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Mfano mzuri ni uimarishaji wa maktaba ya Chuo kwa kupatikana vitabu vya kufundishia na ujenzi wa dakhalia pamoja na vifaa vya kufundishia, vikiwemo kompyuta. Pia Chuo kinategemea kupokea matrekta madogo manne hivi karibuni, ili kuhakikisha vifaa vyote muhimu vinapatikana. Hili Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu alilijibu swali hili.

Kwenye suala la kisima alichosema kinachimbwa kwa mikono. Mhe. Mwenyekiti, ZAWA wanapokuwa na dharura mahala, huwa tunatumia *manual* kabla ya kupata ile gari ya kuja kuchimba kisima. Hii *manual* kama mahala maji yako karibu unafika na unayapata na wanakwenda chini mpaka mita 60 au 70 wanashuka chini kwa kutumia mikono. Hawa wakichimba mkiteremsha pampu ile ndogo kwa matumizi ya ile *campus* yenu pale tu yanawatosheni. Visima hivi viko hata katika majumba ya watu mbali mbali wanatumia ambavyo vimechimbwa kwa *manual*, wakati huo mnafanya mpango wa kutengeneza kisima kikubwa ambacho kitasaidia kuhudumia pamoja na umwagiliaji na mambo mengineyo. Kwa hivyo, asishangae kwamba kuna baadhi ya visima vinachimbwa kwa mkono na kuna baadhi ya visima vinachimbwa kwa mashine, inategemea mahala gani, ikiwa pale mahala kidogo maji yapo karibu ukichimba kwa mkono unapata maji ya kutosha na unatumia bila ya tatizo lolote kwa ile *campus* iliopo pale na maji hayakosekani. Unaweka *over head tank* lile ya lita kama 5,000 na unasambaza mifereji katika maeneo kama mawili au matatu kupunguza tatizo la maji

katika maeneo yale. Hii ni hatua ya dharura sio ya kawaida, kwa hivyo asiwe na wasi wasi nayo sana.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee

Kifungu 0402 Chuo cha Kilimo Kizimbani

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri michango yangu huwa sana haitaki na hii sio mara ya kwanza kutonijibu maswali yangu ninapomuuliza. Sisi ni Wawakilishi wa wananchi ambao tunawawakilisha wananchi wetu na wapiga kura wetu, ili kusikia kile tunachokiuliza na wao wapate kusikia na kuelewa. Lakini Mhe. Waziri hii ni mara ya pili katika wizara yake hakunijibu na wizara hii nyengine pia hajanijibu hata swali moja.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri asipende sana kuwadharau Waheshimiwa, kwa sababu na wao huwa wananchi kule wanawasubiri kwa masuala yao wanayowapa.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema kwamba pamoja na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 49 wa Chuo cha Kizimbani hicho cha diploma, lakini bado kuna haja na ni muhimu kwa diploma kupewa kipaumbele zaidi ya kuboreshwa, lakini Mhe. Waziri hakunijibu. Pia kuboreshwa elimu hiyo iwe sawa angalau na Tanzania Bara kwa kile kiwango cha taaluma.

Je, Mhe. Waziri swali hili ulinijibu? Kwa hivyo naomba unijibu na ikiwa hukunijibu bado sijakubaliana na wewe na nitazidi kunyanyuka kupiga buti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mwenyezi Mungu aniondoshee tabia ya kuwadharau Waheshimiwa wenzangu nisiwe nayo kabisa, maana kama nitawadharau Waheshimiwa wenzangu maana yake siwezi kufanya kazi na wenzangu. Tatizo ni kwamba maswali yako mengi na muda wenyewe ni mfupi na alipojibu Mhe. Naibu Waziri kuna baadhi ya mambo aliyagusia, nikaona madamu yameshagusiwa tena mimi sina haja ya kurejea tena ili kuokoa ule muda, kama unavyotaka Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, asifikiri kwamba sijamjibu kwa sababu ya kumdharau hapana, siwezi nikamdharau hata siku moja. Siwezi kumdharau mtu aliyeteuliwa yuko hapa kwa sababu ya kuwakilisha wananchi. Nakubaliana na wazo lake la kwamba diploma iboreshwe na sio diploma iboreshwe tu, lakini Chuo cha Kizimbani kitakuwa ni kitivo cha Chuo Kikuu baadae, katika jitihada zetu

tunazoendelea nazo za kukuza maabara na mengine, kwamba itakuwa ni kitivo cha Chuo Kikuu baadae.

Halafu ni kweli kwamba kuna suala la ajira za wanafunzi katika Chuo cha Kizimbani, ambapo wenyewe watu wa kilimo wanasema wakimaliza pale wanawaajiri na mwaka huu wameshasema kwamba wataongeza baadhi ya wanafunzi wanaomaliza Chuo pale kuwaajiri. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, asinifikirie kwamba mimi nayadharau maswali yake hapana, ni kwa sababu tu maswali yanakuwa mengi na muda wenyewe ni mfupi hautoshi. Mwenyezi Mungu aniondoshee tabia ya kuwadharau Waheshimiwa wenzangu. Mimi naomba dua kila siku nikilala na nikiamka, niwaheshimu maana ni Waheshimiwa hawa, ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nampa hongera Mhe. Waziri kwa suala nililomuambia la kudharau, pia sitomlaumu. Lakini vile vile nasema kuwa nakiri kwamba nimekosea na nasema Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu yake tuendelee ahsante.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia katika eneo hili la Chuo nilimuomba Mhe. Waziri baada ya kazi nzuri inayofanywa na chuo pale, lakini wanafunzi wanaohitimu kuna mipango ipi ya serikali kuwawezesha vijana hawa kuweza kujitegemea kutokana na taaluma wanayoipata badala ya kusubiri ajira kutoka serikalini. Suala hii sikupata kumsikia Mhe. Waziri anasema nini.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, mipango hasa kwa maana ya kuwawezesha vijana wale kujitegemea napenda niseme hatujaiandaa. Isipokuwa lazima tufanye mpango mpaka tupate *incubator*, *incubator* ni fedha ambazo zinasaidia unapowaazimisha watu wanapomaliza unawakopesha wanakwenda zao kujiendeleza katika maeneo mengine. Hawa ni wakulima, wengine ni wafugaji, wengine watakuja kuwa wavuvi baadae, kinachotakiwa kufanywa hapa ni kwamba hawa tuwapatie fedha kwa ajili ya kwenda kuendeleza kilimo katika maeneo yao, kuendeleza ufugaji katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Kilimo suala hilo hatujalipanga, lakini Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika hilo suala analifanyia kazi, la mifugo na mambo mengineyo. Kwa hivyo, wakishamaliza hapa kama wanahitaji kujitegemea na ni vizuri hasa na ni wazo zuri sana alilozungumza Mhe. Asaa Othman, wakienda katika Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika wakaweza kupata mikopo pale kuweza kujiendeleza katika maeneo mbali mbali ambayo

wamesomea pale, hili ni suala muhimu kabisa. Sisi hatujawa na *incubator* ya kuweza kusaidia mambo hayo. Wenzetu Cho cha Amali wana *incubator*, wanafunzi waliomaliza pale wanawakopesha pesa wanawasaidia wanakwenda kununua patasi, landa na mambo mengineyo. Sisi mfuko huo hatujawa nao, lakini tunashauri kwamba mfuko wa uwezeshaji upo, waende pale watasaidiwa.

Kuna wizara ya vijana hapa vile vile nayo ina mikopo maalum inatoa na huku pia kuna mifuko ipo waende wakajiendeleze, hilo ndio suala muhimu kabisa. Kutokana na ukuaji wetu wa elimu, kwa kweli hivi sasa vijana wanatakiwa wahamasike katika njia hiyo, wahakikishe kwamba wanapomaliza skuli wanafikiria zaidi kujitegemea na kujiajiri kuliko kuajiriwa. Mhe. Mwenyekiti, ajira katika serikali imeshakuwa haiyayuki tena, hakuna imeshajaza sasa, serikali imeshavimbiwa katika uajiri. Kwa hivyo, suala la kujitegemea ni suala muhimu kweli, ndio maana hata tumeyaruhusu mashirika binafsi waanzishe vituo mbali mbali waweze kuwaajiri watu hawa na sehemu nyengine mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri, ila kwa kuwa kamtaja Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika, pengine tungepata kumsikia kuna lipi angalau katika hili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili kwa maelezo yake sahihi. Sio wale wahitimu wa Chuo cha Kilimo tu Mhe. Mwenyekiti, hata wahitimu wa vyuo vikuu wengine wengi wako. Pale kuna kituo maalum kwanza cha kujiorodhesha wale wote ambao wanataka kuwezeshwa na kupata ajira. Sasa vitu hivi viwili vilivyoongezeka pale kupitia idara ya uwezeshaji, lakini kuna kituo cha kujiorodhesha pale kwa wale wahitimu wote. Kama wanahitajia msaada wa taaluma, kuna mtaalamu tumemleta pale kutoka India nilisema wakati nawasilisha bajeti yangu wataelekezwa zaidi ili waweze kuwa wajasiri amali wazuri waweze kujiendesha kimaisha yao.

Kwa hivyo, hili suala lipo na tuna programu katika zile programu ambazo serikali imetenga shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuwaendeleza wananchi au pengine vijana wa aina hii.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0402	Chuo cha Kilimo Kizimbani	500,000,000

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambaye katika historia yangu mimi sikumbuki kuwa na majibu mabaya sana, ni mtu mwenye maneno mazuri yenye murua na ndio maana akafika mpaka leo kuwa Waziri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee hivyo hivyo.

Sasa aliniambia kwamba sheria kweli amekubali kuwa ina mapungufu, lakini msitu wangu wa Kiwengwa nataka kumwambia unazidi kuyoyoma na unazidi kupotea. Namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na kukubali kwamba mapungufu yapo, lakini hakuniambia ni lini sheria hiyo itakuwa na harakati sana na hasa kiangazi kama hiki msitu unalia kule.

Nimesema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu *fine* hasa zinazotolewa ni ndogo, haihalisi na ndio maana watu wakawa hawaogopi wanaendelea kukata tu Mhe. Mwenyekiti. Naogopa tu kuja kupigwa kanuni na kusema kuwa magari mengine yanayohusiana na sisi, sisi nani sijamtafsiri mtu na ndio maana naomba Mhe. Mwenyekiti, kuwa atuletee sheria haraka sana ili akina sisi tusije tukaingia hatiani. Naomba suala hili Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, namjibu Mhe. Mwakilishi suala lake zuri na jitihada yake ni kutaka kutuhimiza kwamba sheria ifike upesi katika Baraza la Wawakilishi ili ifanyiwe marekebisho, kweli ile sheria ni ya zamani, na ni kweli inafanya mambo yaliyokuwa hayaendani na wakati sasa hivi na ana masikitiko makubwa kuwa msitu wake wa Kiwengwa unapotea.

Mhe. Mwenyekiti, hata kama sheria hazijaja. Kuna mambo kama tutayafanya katika maeneo yetu yatasaidia kupunguza uharibifu wa misitu yetu. Suala la kutoa cheti cha makaa, kutoa cheti cha kuni viko katika maeneo yetu kwa masheha wetu, nadhani ni vizuri tupunguze utoaji wa vyeti vya makaa na kuni, tukipunguza na tukishirikiana, basi ikiwa mtu akiwepo pale Kiwengwa hapati cheti cha makaa na hapati cheti cha kuni, basi anajua hana pahala pa kwenda kukata. Walioko Upenja, maana anaweza kutoka kule Kiwengwa akasema anakwenda kukata cheti cha makaa Upenja. Huko nako wakizuia wasikate cheti cha makaa na kuni mpaka kwa sababu maalum na wakawasiliana na masheha, basi nina hakika misitu haitoharibiwa. Lakini ikiwa tunaendelea kutoa vyeti vya makaa na kuni, ambavyo tunavitoa sisi wenyewe katika maeneo yetu, basi bado misitu yetu itaendelea kuangamia. Suala hili ni muhimu kabisa kwa sababu linahitaji umoja wa watu wote katika maeneo yetu, tufanye kazi sote kwa pamoja, tuwaelimishe watu wetu wasiharibu misitu.

Mhe. Mwenyekiti, zamani ukienda kwa sheha ukitaka cheti kuna maswali mengi anakuuliza, ukimjibu ndio anakupa cheti na ukishindwa kumjibu anakwambia cheti sitoi, hiyo ndio hali halisi. Tukishirikiana katika hili basi huu msitu hautoharibika, hii sheria tutaileta itafanyiwa marekebisho mbali mbali, lakini sheria peke yake haitofanya kazi ikiwa bado tunatoa ovyo vyeti vya kuni, vyeti vya makaa basi sheria itakuwa haina maana yoyote. Maana mtu akipita polisi pale ana cheti rasmi cha sheha, akipita kwengine ana cheti rasmi cha kuni na cha mkaa bila shaka itakuwa hakuna tatizo tena, maana watu wa Misitu wamewaweka watu njiani kuangalia ile ruhusa na mambo mengineyo. Sasa tujitahidi katika hili sote kwa pamoja kuwaelimisha wananchi kulinda misitu, ulinzi wa misitu na mazingira yetu ni wetu sote wananchi, sio wa serikali peke yake, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, naamini kweli Mhe. Waziri hana tabia ya kuringa anajibu vizuri. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mkurugenzi wangu shujaa kwa kunisaidia kulinda msitu huu na yeye anasikia na atajitahidi kumsaidia Waziri kuleta sheria haraka sana iwezekanavyo, ili kipande kilichobakia kisimalizike. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Nilipochangia Idara hii ya Misitu na Maliasili nilizungumzia kuhusu wanyama wale waliomo ambao wanaweza kuisaidia serikali kupata fedha, na nikazungumzia kuhusu hawa Kimapunju, nikazungumzia kuhusu popo ambao wanapatikana katika visiwa vyetu tu. Sasa nikauliza je, hawa wanaingiza mapato ya kiasi gani katika nchi yetu kusaidia suala la utalii.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka nijue tu kwamba kuna mipango gani mizuri ambayo imepangwa ya kuweza kuingiza fedha kwa vitu hivi vya maliasili katika nchi yetu na kuwasaidia wale watalii, ikawa serikali inapata kipato zaidi. Kwa sababu mtu huiga lile jambo ambalo ni zuri. Kwa hivyo, wenzetu tunawaona maliasili zao hizi zinawaingizia fedha kwa serikali kwa kupitia watalii na watu wanaokwenda kufanya maonesho.

Kwa hivyo, aniambie Mhe. Waziri wamejipanga vipi au wana mipango gani mizuri, kwa maliasili zetu kuhusu hao ndege yaani hao Kimapunju wanaingiza mapato zaidi. je, wamejipanga vipi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu nilisema kwamba katika kuhakikisha kwamba maliasili zilizomo kwenye misitu tunazifanya pamoja kwa kushirikiana na jamii. Ndio maana hapa Jozani kuna ule ushirika unaitwa, jina lake limenitoka lakini unajulikana. Ushirika wa Jozani pale,

ushirika ule wa Jozani unashughulikia masuala ya ulinzi wa ule msitu pamoja na haya masuala ya hizi biashara za wageni wanaokuja kutembelea pale na mambo mengineyo yanakusanyika pale yanafanywa. Sasa kama kuna msitu mwengine huko haujawa na ushirika mwengine wa Micheweni huko ni jukumu la wale wananchi wa eneo lile wafanye ushirika vile vile na kuna mapato inapata serikali na wanapata wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa mgeni rasmi katika kugawa mapato yaliyopatikana katika msitu ule wa Jozani, wananchi wa pale walipewa mapato fulani yaliyotokana na mazao yaliyopatikana ya wale wanyama waliokuwa pale katika msitu ule wa Jozani. Sasa kama na Micheweni tatizo hilo lipo, basi ni vizuri wakakaa pamoja wakaunda hiyo jumuiya na wao watafaidika, kwa hivyo serikali itapata na wao watapata. Maeneo tunatumia kwa pamoja katika masuala mazima ya utalii.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Waziri. Lakini namuomba sasa Mhe. Waziri yeye kwa kupitia wizara yake wawashajihishe wale watu, halafu wakishawashajihisha wawe wao kama wizara ni wapiga debe wao kuwapata hao watalii kwenda kuangalia halafu kuingiza mapato ili yaingie kwenye serikali. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu misitu, nilisema kwamba hifadhi ya misitu Kajengwa wana kiwanja chao ambacho kinataka kujengwa kituo cha polisi. Lakini kituo kile wameambiwa kwamba watapewa kiwanja mbadala, lakini hawakitaki na ni lazima wapewe kile ni kwa sababu gani?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, polisi hawajasema kuwa ni lazima kile kabisa. Ndio maana nikasema mimi walikuja ofisini kwangu na wameniambia kwamba kama Jambiani hawataki basi tupeni msitu wa Umbuji, kaja Kamishna mwenyewe kaniambia suala hilo, kwa sababu hawajasema kuwa ni lazima kiwanja kile. Lakini Serikali za Wilaya na Serikali za Mikoa zinafanya kazi kwa faida ya wananchi. Kwa hivyo wameona faida ya pale iendelee kupatikana pale Makunduchi na Jambiani, ndio maana wakasema tutajenga hapa, mnasemaje. Sasa wenyewe wakasema aah! tujenge hapa na wala sio suala la Afisa Tawala, ni suala la kuwa Serikali ya Wilaya imekubaliana kwamba wajenge pale kituo na nimewaambia watu wangu waende wakapime ili patengenezwe na hautatumiwa msitu wote. Watu wa sehemu ile ya Kajengwa wameshafaidika na msitu ule inajulikana kabisa, na bado wanaweza kuukuza msitu ule kwa kuuendeleza mbele zaidi. Sio lazima pale kabisa, hiyo haijatokea kwamba ni lazima pale. Kama hawapataki kupatoa basi polisi watatafuta pengine, hilo nimeshasema kabisa, polisi

watatafuta pengine watajenga. Lakini ukitizama pale mahala ni *strategically*, kwa sababu kuna suala la utalii katika ukanda ule.

Mhe. Mwenyekiti, tukiwa na askari walinzi karibu pale itakuwa ni *strategic* nzuri kabisa ambayo tutayalinda maeneo yale. Sasa wao sijui wanataka kuwaondoa pale polisi wawapeleke wapi. Nadhani waliwahi kuoneshwa hao polisi mahala ambapo ni ndani sana mwituni huko. Sasa huko mwituni si ndio kwa kukuza msitu. Sasa kama pale wananchi hawataki Kamishna keshasema basi wako tayari wapewe pengine. Lakini Serikali ya Wilaya inajua kuwa kuna faida gani katika kituo kile kwa faida ya wananchi wa eneo lile, ndio maana wanasema tujenge hapa, tena wanashauriana tujenge hapa, sio Afisa Tawala peke yake.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ushauri wangu ningeomba wizara ingekwenda kwa wananchi ili kuwaelimisha waelimike, maana yake bado hawajaelimika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, hilo shauri zuri. Tumeshakwenda na tumeshaanza kuzungumza na wananchi. Unapozungumza nao wanaitikia vizuri, lakini ukiondoka ukenda kule unapata matatizo kidogo. Tumewahi kuzungumza nao wanaitikia vizuri, lakini ukienda kule unapata matatizo. Hujui kama anatokea kidudu mtu anaingia kwa nyuma huko yanatokea matatizo mengine. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni suala la maendeleo na ndio maana wilaya inasema pajengwe pale ni maendeleo ya Wilaya ya Kusini.

Mhe. Mwenyekiti: Basi Mhe. Waziri atakwenda kutoa taaluma, tunaendelea.

Kifungu 0701	Idara ya Misitu na Maliasili	1,299,318,000

Kifungu 1102 Idara ya Umwagiliaji Maji

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii na pia nimshukuru Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yao.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la kadhia ya wakulima wa Bumbwisudi, ambao wamelalamika kuchangishwa fedha za kuchangia umeme. Sasa katika maelezo yake Mhe. Naibu Waziri amekiri ingawa amesema kwamba takwimu nilizotoa si sahihi, na mimi nataka nimuwekee sawa hapa, kwamba mimi sikutoa takwimu, isipokuwa nilitoa makisio.

Kwa hivyo, nilisema kulingana na vile viji-*plot* viliomo mule ndani kama unataka kufanya makisio ndio utafikia kiwango kile, kwa sababu kwa vyovyote vile wakulima wale wasingeweza kujua kwa ujumla wake zimekusanywa kiasi gani. Lakini nashukuru kwamba yeye mwenyewe amekiri kwamba wamechangishwa shilingi 20,000/= na jumla zilikuwa kama shilingi milioni 6,000,000/= kwa ujumla wao.

Sasa kwenye mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba wakulima hawa hoja yao ya msingi ni kwamba kwa nini wamechangishwa wao tu, mbona kwenye mabonde mengine hawakuchangishwa? Kwa hivyo, je kuna uhalali gani wa kuchangishwa suala hili na badala yake wakapata hasara na matokeo yake wakapata hasara mara mbili, kwamba kile kilimo chenyewe hakikua na huku wametakiwa kila mmoja; wakulima, wananchi wanyonge, masikini kila mmoja atoe shilingi 20,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuelezwa kwamba baada ya hivyo walivyoliona. Kwanza nataka nithibitishiwe kwamba walichangishwa mabonde yote au Bonde la Bumbwisudi tu? Pili ikiwa ni bonde hili kwa nini iwe bonde hili tu? Tatu wanachukua hatua gani, ili kuwarejeshea haki zao wakulima wale wa Bumbwisudi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikimjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu nilieleza kwamba katika kuchangishwa wakulima ni mabonde yote na sio Bonde la Bumbwisudi tu. Wakulima wa umwagiliaji wanapaswa kuchangia katika sehemu zote za umwagiliaji suala la umeme na sio kama Bonde la Bumbwisudi peke yao. Kwa kweli hili ni suala la umeme kila kwenye *irrigation* hivyo mkulima anatakiwa achangie shilingi 20,000/=.

Vile vile kuhusu kujereshewa fedha zao, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikijibu suala hili baadhi ya fedha nyengine nilisema kwamba katika mchango huo waliochanga wakulima hawa ulikuwa hautoshi, na wizara nao walichangia kwenye mchango huo. Kwanza suala hili Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyingi kulikuwa na mita za zamani, sasa baada ya kutolewa mita zile zikatiwa mita za TUKUZA na kulikuwa na madeni mengi, ambapo wizara madeni yote yale imeyabeba.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakuna fedha ambazo zilizozidi kwa wakulima hawa katika kuchangia umeme, pia kama nilivyosema kwamba fedha walizochangia zilikuwa hazitoshi, na wizara ilipiga kifua kujaliza fedha hizo za umeme.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba suala hili kwangu mimi limeletwa na wenyewe wakiwemo hawa kama kwenye majibu yake Mhe. Naibu Waziri wakati alipokuwa akifanya majumuisho, aliposema kwamba fedha hizi hazikukusanywa, na huyu niliyemtaja ndugu Kadir akasema kwamba zimekusanywa na wenyewe viongozi wa Kamati hizi za Mabonde, lakini hao viongozi wenyewe miongoni mwao ndio ambao wameniletea suala hili.

Sasa mimi nadhani mambo mawili, ili tuendelee moja ikiwa kuna usahihi wa taarifa ambazo Mhe. Waziri amepewa na watendaji wake, basi taarifa hizi zifikishwe kwa wakulima wenyewe. Kwa kweli moja nililizungumza Mhe. Mwenyekiti hapa, kwamba waliomba hawa kama ikiwa wizara suala hili limeidhinisha basi wapewe angalau barua ya kuthibitisha kwamba Katibu Mkuu ameagiza suala lile, na kwamba serikali kupitia wizara itatoa bakaa iliyobakia kile ambacho wametakiwa wakichangie.

Mhe. Mwenyekiti, inaonekana wakulima wenyewe hawajaridhika na wanahisi hakuna uwazi katika suala hili zima. Kwa hivyo, ili tuendelee nadhani angalau Mhe. Naibu Waziri aniambie kwamba atakwenda kukaa na wakulima wa Bumbwisudi akutane na uongozi pamoja na kamati zao zile, kwa ajili ya kuelewana na suala hili walijue ukweli wake uko vipi.

Vile vile kama ni suala ambalo linahusu utaratibu basi waeleweshwe, na mimi nina hakika kwamba wananchi wa Zanzibar ni waelewa na kwamba wakieleweshwa na wakaona mantiki ya hoja yao basi wataelewa tu, basi ninataka anieleze hivyo tu na nitaruhusu tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, namhakikishia Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba nitakwenda kukaa na wakulima wa Bumbwisudi, ili kuona suala hili pamoja na kuwaelimisha, kwa sababu suala hili ni jambo ambalo liko katika maeneo mengi na masuala yanayohusu wananchi wetu mimi napenda sana kuyafuatilia, ili kujua ukweli wake uko vipi.

Kwa hivyo, ninamuhakikishia Mhe. Mjumbe, kwamba suala hili tutalifuatilia kwa ajili ya kuona liko vipi na kuona haki iko wapi na tuweze kukaa pamoja na kuendeleza kilimo chetu hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na wakati nilipokuwa nikichangia kwenye eneo la umwagiliaji maji nilisema kwamba Mhe. Waziri anayehusika na wizara ya maji alituambia kwamba tunalo tatizo

linalotukabili la uhaba mkubwa wa maji chini ya ardhi visiwani Zanzibar. Sasa kuna muendelezo wa uchimbaji wa visima kwa ajili ya umwagiliaji wa mazao je, tutafika na swali langu liko hapo?

Lakini nikakumbusha kwamba kuna suala la uvunaji wa maji ya mvua limefikia wapi hili badala ya kuendelea kuchimba visima ambavyo tayari tuna tishio hilo la uhaba wa maji ardhini na tukizingatia ongezeko la mahitaji, yaani *population* ya watu pamoja na vyote tunavyopanda mimea na kadhalika, Mhe. Mwenyekiti hapa sikupata majibu sahihi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alisema hilo na kwenye majibu yangu nakumbuka nilitoa, na nikataja baadhi ya mabonde ambayo maji yake yatahifadhiwa kwa ajili ya umwagiliaji. Wakati nilipokuwa nikijibu suala hili na pengine Mhe. Mjumbe alikuwa amekwenda kusali sala ya Adhuhuri ndio pengine hakuweza kunipata.

Lakini nilisema kwamba mkazo hivi sasa tunaoendelea nao ni kuweka umwagiliaji kwa kutumia maji ya mvua, yaani uvunaji wa maji ya mvua. Mhe. Mwenyekiti, pia nilisema kwamba kwa Kilombero tunataka tuyakusanye maji ya Mto Mkiwa, kwa Kibokwa tunataka tukusanye maji ya Mto Mgambo na Kibokwa tena maji ya Mto Pweza, Chaani maji ya Mto Bwabwaja, Mlemele maji ya Mto Mlemele, hali kadhalika Dobi kwa maji ya vyanzo vya Kensa na Renguni Taifu na Ukewani Kisiwani; na hayo ni maeneo ambayo tunataka kuanza kufundisha watu kutumia maji ya mvua.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba tusibweteke katika suala la mabadiliko ya tabia nchi tupande miti kwa wingi, na tukipanda miti kwa wingi basi tunahakikisha kwamba maji yatakuwa yanapatikana kwa wingi katika nchi yetu, kwa sababu mvua zitakuwa zinapatikana na hakuna sehemu ambayo ilikuwa ina ukavu zamani kuliko Dodoma, yaani kulikuwa na ukame mkubwa sana.

Lakini baada ya jitihada ya kupanda miti maeneo yaliyozunguka Dodoma, basi hivi sasa utashangaa kwamba Dodoma wanapata mafuriko ni kwa sababu ya ile miti imepandwa pale. Kwa hivyo, nakubaliana kwamba tukuze suala la kiwango cha maji ardhini kwa kupanda miti pamoja na kufanya hili zoezi la kukusanya haya maji ya mvua katika maeneo mbali mbali ya *irrigation* na nilizungumza.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na majibu ya Mhe. Waziri, isipokuwa kwa sababu tunalima, na ili tulime ni lazima kilimo cha uhakika na matumizi ya maji. Sasa suala la kuvuna maji ya

mvua ni hadithi ya muda mrefu nakumbuka waliopita wote hata marehemu Adam Mwakanjuki ilikuwa ipo hii. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ipi mikakati ya muda mfupi, ya kati na mirefu maana tunataka twende sambamba na haya mambo, tukisema tutavuna na huku kuna *story* ya kuchimba visima na mimi nimeiona ni tishio ndio nikakumbusha serikali kwamba mbona tuna suala hili, na hili lisitajwe tu angalau ile mikakati ya muda mfupi ni ipi tuelewe hivyo, kati ni ipi na pamoja tena zuri kabisa ambalo alomalizia ni kwamba tutaendeleza masuala ya miti kuipanda na mimi nilikumbusha hilo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba tuwatumieni masheha na wala tusiwatumie kwa mambo mengine tu na haya ya uhai wa watu ni muhimu na miti ipandwe Mhe. Mwenyekiti ni hilo tu. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aligusia eneo la Kilombero. Lakini mimi wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu nilisema kwamba kulikuwa na *study* ya mwanzo; nakumbuka walikuja wataalamu wa kutaka kutuwezesha, ili tupate mpunga wa kumwagilia maji na wakasema Kilombero, Pangeni, Upenja maji yapo ya kutosha.

Lakini *study* ya pili sikupata *briefing* yoyote kwamba wamefikia wapi na walikubali wamepasisha kabisa wataalamu hao kuwa bonde lile linawezekana likafanyiwa *system* hiyo ya umwagiliaji maji mpunga, na hili sikupata kusikia jibu Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aniridhishe, ili nisimpotezee wakati wake na wananchi wamsikie lini wategemee kuweza kulima mpunga wa kumwagilia maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kutekeleza miradi ya maendeleo ni hatua kwa hatua na nilisema kwamba Benki ya *Exim* inaanza na masuala haya katika Bonde la Kibokwa, na bila ya shaka si kama wataishia hapo, isipokuwa watakuwepo Kibokwa, Cheju, Kilombero, lakini hivi sasa mtazamo mkubwa wanaanza kwa Kibokwa kwa ajili ya umwagiliaji maji.

Sasa ni utaratibu wao ni kwamba watakwenda katika eneo jengine na Cheju pia watakwenda, kwa ajili ya umwagiliaji maji, na nia yetu hasa ile tuliyoizungumza kwamba tujitosheleze kwa wali hapa ipo pale pale. Kwa hivyo, ndio maana tunaomba misaada kutoka benki tofauti na bila ya shaka tutakwenda hatua kwa hatua na wala hatuwezi tukafanya (*buu baa!*) wakati mmoja, tukatengeneza visima au *irrigation* katika nchi nzima si rahisi kusema

kweli, isipokuwa tunakwenda kidogo kidogo. Kwa mfano, Kibokwa kule yanaweza kukaa maji ya mvua na Kilombero pia yanaweza kuja maji ya mvua.

Mhe. Mwenyekiti, maji ya mvua unaweza kuyatumia kwa muda mrefu ni *sustainable*, kwa sababu Mwera hakuna kisima pale na *irrigation* ipo kila siku na watu wanalima na Mtwango *irrigation* ipo, na kila siku watu wanalima, kwa sababu kupungua kwa maji ya Mto Mwera hivi sasa ndio maana Mwera wanaanza kuchimba visima, kwa sababu ile hali ya maji ya Mto Mwera imeshuka sana kutokana na tabia nchi.

Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe namuomba asubiri tu tunakwenda kidogo kidogo na tutafika kama alivyoniuliza Mhe. Asaa Othman Hamad je tutafika, basi *inshaallah* akipenda Mwenyezi Mungu tutafika na jambo la msingi ni mshikamano tu katika utekelezaji wa miradi yetu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mwanzo Mhe. Waziri alisema kwa kuwa wizara hii si yake kuna mambo mengine yatampenya nakubaliana naye, kwa sababu mimi nilikuwemo siku hiyo walipokuja Wamarekani na kuweza kupasisha suala hilo pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti tuendelee kwa kuwa wizara hii si yake, na mambo mengine amekiri kwamba yatampenya na mimi nakubali kwamba yatampenya na wala si kwa jeuri tu, isipokuwa kwa nia nzuri tu. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 1101	Idara ya Umwagiliaji Maji	607,066,000/=
Kifungu 1301	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, sipendi kumkwaza Mhe. Waziri, lakini kwenye majumuisho yake sikupata jibu hata moja alilonijibu na nilisema jibu nalijua nitakapolipata. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nilipochangia nilisema kwamba kuna wanafunzi ambao wanasoma kwa vitendo na wanafunzi hawa huwa hawalipwi na wala hawapati usafiri, na nilimuuliza Mhe. Waziri na wengine huwa wamepangiwa shughuli zao mbali. *(Makofi)*

Kwa mfano, wengine wanakuweko Pemba, wengine wanakuweko vijijini na wengine wanakuweko shamba katika mji huu wa Zanzibar, lakini hawana nauli na wengi wao ni masikini hawana uwezo wa kulipia gari. Je, Mhe.

Waziri wizara yako imejipanga vipi kuhusu suala hilo na ninamuomba Mhe. Waziri anipatie jibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Mjumbe amenisaidia sana kujua kwamba kumbe hili swali nimelijibu, lakini sikujua ninamjibu nani na kumbe ninamjibu yeye.

Kwa hivyo, nilijibu kwamba wanafunzi wanaofanya mafunzo ya vitendo huchagua wenyewe maeneo ya kwenda, kwa sababu ya kurahisisha kuyafanya yale mafunzo ya vitendo na huwa wanasema, kwamba mimi nitakwenda mahala fulani na huko ndio wanaruhusiwa kwenda kwa ajili ya kufanya mafunzo ya vitendo, kwa sababu yeye anajua Chuo kile hakina uwezo wa kuwalipa masuala ya nauli na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo wanakuwa wanachagua wenyewe kwa ufupi, na nilijibu wakati nilipokuwa nikifanya majumuisho ya Wizara hii na wala sikujua ninamjibu nani na kumbe hili moja nilipata na kwamba Mhe. Mjumbe nilimjibu.

Sasa nashukuru sana *Alhamdulillah*, kwamba wale wanachagua wenyewe maeneo ya kwenda na wanapochagua huwa wanasema mimi nitakwenda Kengeja, mwengine anasema nitakwenda Kisima Mchanga, pia wengine wanasema nitakwenda Muyuni na maeneo tofauti, yaani wanakwenda maeneo yale kwa kuchagua wenyewe, na wanapochagua maeneo yale wanajua wenyewe wameshajifikiria watafanya vipi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba ni kweli wanafunzi huwa wanachagua wenyewe. Lakini wengine tuseme wanakaa hapa mjini anapangiwa Muyuni na huko hataki usafiri wa kwenda Muyuni. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anijibu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, anapochagua Muyuni anajua atakuwa na mwenyeji Mhe. Jaku Hashim Ayoub na hilo ndio tatizo, kwa sababu kule Muyuni anakuwa amechagua yeye mwenyewe na sio kama amepangiwa, isipokuwa anakuwa amechagua yeye mwenyewe kwamba mimi nitakwenda Muyuni na ilihali yeye yupo hapa Mjini. Kwa hivyo, nadhani ni vyema angechagua Mwera ambapo nauli ya daladala ni ndogo, lakini anachagua Muyuni au maeneo mengine ya mbali na wala hachagui Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali langu ni kwamba wanafunzi wa vitendo hata walioko katika vyuo vya Tanzania Bara wanachagua wenyewe watakwenda wapi labda kujae huku. Kwa mfano mimi ninao wanafunzi tayari wameshakuja wanasoma Bara, lakini wameamua kuja kufanya mafunzo ya vitendo hapa na wamechagua wenyewe na tunao majumbani mwetu tunakaa nao.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, sawa Mhe. Waziri amenijibu lakini bado sijaridhika. Kwa hivyo, niseme kwamba katika hizo safari zao hakuna utaratibu wa kulipiwa nauli.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, maana ya kuwaambia wachague wenyewe ni kwa sababu hiyo bajeti yetu tuliyonayo haitoshi kukidhi yote na ndio maana tunawaambia wachague wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tuendelee.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Vicheko/Makofi)*

Kifungu 1301

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tunazungumzia Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo inajumuisha takriban shughuli zote za wizara nimeona nisimame hapa hapa juu ya suala langu hasa kwa uzito wake.

Mhe. Mwenyekiti, sentensi yake ya mwisho Mhe. Waziri wakati alipokuwa akifanya majumuisho alisema kwamba nyimbo ya kufundisha au kufundishwa haikeshi ngoma, naam! Mimi nataka nithibitishe kwamba *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma*. Mhe. Mwenyekiti, hasa limethibitika hilo wakati alipokuwa akijibu hoja za Wajumbe mbali mbali nikiwemo na mimi kuhusu suala la hifadhi ya chakula. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Waziri kutokana na hoja yangu na za Wajumbe wengine nafikiri akinijibu mimi labda itakuwa pengine ameshasaidia na wengine atapunguza buti katika idara inayofuata ya Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Kwa kweli alisema kwamba inakuwa vigumu kuweka hifadhi kwa sababu ya chakula ambacho tunatumia hapa, akatoa mfano wa mchele, sukari na unga kwamba vinaharibika, hivyo akasema kunahitajika utaalamu wa hali ya juu.

Suala hili Mhe. Mwenyekiti limenisikitisha, kwa sababu na ndio maana alihusisha na ile nyimbo ya kufundishwa, kwani Waziri mwenyewe alipokuwa akitoa mswada huu mwaka juzi nafikiri alikuwa Mhe. Mansoor Yussuf Himidi. Kwa hivyo, tuliambiwa hapa kwamba utaratibu wake kwa sababu chakula kisiharibike huwa kinahifadhiwa, na halafu ikionekana hakikuhitajika mpaka muda wa kuharibika usije ukafika huwa kinatolewa. Kwa hiyo inakuwa ni *rotation* ya kuhifadhi chakula na tuliambiwa hapa katika majumuisho ya mswada ule wa Sheria ya Hifadhi ya Chakula na Lishe.

Sasa leo inapokuja serikali ikatujibu kwamba inashindwa kuanzisha hivyo kwa sababu chakula kinaharibika kuna utaalamu, huo utaalamu wakati walipotuletea mswada ule hawakuutafakari. Mhe. Mwenyekiti, hii ni hoja muhimu tena ni nzito, kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Kusimamia Hifadhi ya Chakula na Lishe ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, wanapokuwa hawaifanyii kazi au hawaitekelezi, basi wanamuangusha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie maelezo yangu na nipate maelezo ya Mhe. Waziri kugongomelea msumari kwenye hoja yangu. Kwa kweli inasikitisha Mhe. Mwenyekiti, na tumesema katika hili Waheshimiwa Mawaziri wasituvungevunge, Mhe. Mwenyekiti kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 50 kuna maelezo kuhusu *Program* ya Uhakika wa Chakula na Lishe, na wala sitaki kuyasoma yote maana itachukua muda mrefu sana, lakini fedha ambazo ziliombwa zinashindwa kupatikana, na fedha zilizopatikana ni shilingi milioni 30,000,000/= kutoka SMZ na milioni 55,294,720/= kutoka Serikali ya Ujerumani. Sasa tukitizama jumla ya shughuli zilizofanyika, na kama nilivyosema kwamba sitaki kupoteza muda, hazionekani kabisa kwamba zinaakisi hata hizi milioni 85 ambazo zimepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, ninachouliza ni kwamba wao wenyewe kwenye kitabu chao cha *Program* wanatuambia viashiria vya kufanikiwa ni kuwa na maghala na tani za vyakula vilivyohifadhiwa. Kwa hivyo, watuambie na tumeshachoka na maneno ya kila siku ya semina na mafunzo, yaani ile shughuli yenyewe; na kila siku huwa napiga kelele Mhe. Mwenyekiti, kwamba tatizo letu tunatenga fedha lakini *output* haipatikani, yaani ile tija ya shughuli tunayoifanya haionekani na inaishia kwenye semina, mafunzo, kamati na tunaishia hapo hapo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niambiwe kwamba hili kwa nini tuidhinishe fedha hizi za kwenda kushughulikia hifadhi ya chakula ikiwa shughuli ya milioni 85 ni hii ambayo wameiorodhesha kwenye ukurasa wao wa 50 wa kitabu hichi. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, si kama katika suala la Hifadhi ya Chakula hakuna kitu kilichofanyika. Kwa kweli yapo mambo mengi yameshafanyika katika mwaka uliopita na mimi nimeyazungumza.

Kwanza kuna kamati nne za uhakika wa Chakula na Lishe zimeanzishwa Wilaya ya Kati, Shehia ya Marumbi na Umbuji, Wilaya ya Kaskazini 'A' Shehia ya Mwembeshauri na Tumbatu Gomani na jumla ya wanajamii 48 walishiriki katika kazi hizi, ili mafunzo juu ya utekelezaji wa mipango kazi, tathmini ya ufuatiliaji wa uhamasishaji wa rasilimali za utekelezaji wa mipango kazi ya uhakika wa chakula na lishe yametolewa kwa Wajumbe wa kamati hizi.

Vile vile Repoti ya *Food Balance Sheet* imetayarishwa na kusambazwa kwa wadau, mafunzo juu ya Elimu ya Lishe yametolewa kwa Shehia za Mbuzini na Pujini, Tumbe Mashariki na Magharibi na Pemba na Shehia ya Kijini, Kilimani, Kidoti na Tazari jumla ya wanajamii 120 wamepatiwa mafunzo. Kwa hivyo, haya ni baadhi ya mambo ambayo yamefanyika kwa hizo ambazo nimezitaja hapo juu fedha zilizotolewa na zilikuwa ziwe milioni 300,000,000/=, lakini tumepata milioni 30,000,000/= katika suala hili na wametumia kwa ajili ya kazi kufanyia kazi mbali mbali ambazo nimezieleza hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo ukiyasoma kwenye hotuba yamefanyika na ni kweli, kwa sababu hivi sasa kwa sababu haya mambo yameshafanyika, na sasa Uhifadhi wa Chakula wanaendelea na utengenezaji wa ghala kwa ajili ya kuweka chakula. Sasa pale niliposema suala la unga na mchele nilikuwa nataka wenzangu wafahamu, kwamba katika uwekaji wa chakula mchele huwezi kuweka muda mrefu ni lazima kila baada ya muda ubadilishwe, na sawa kama alivyosema na mimi nilisema hivyo, kwamba baada ya muda mfupi mchele, unga wa ngano ubadilishwe.

Lakini ni vizuri kupata vyakula vikiwa kwenye maganda yake, kwa sababu vyakula vikiwa kwenye maganda yake vinakaa muda mrefu, kwa mfano wenzetu Bara kule wananunua mipunga katika maeneo mbali mbali kwa kuweka kwa ajili ya hifadhi ya chakula na huko ndiko tunakolenga na sisi. Kwa hiyo, pamoja na kuwa *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma*, lakini unajua kwamba chakula kwenye maganda yake kinakaa muda mrefu zaidi na badala ya kuwa mchele unakuwa mpunga, na hilo ni suala muhimu kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, pia masuala ya mafunzo ya lishe yenyewe ambapo nimesema kwamba yameshafanyika katika ukurasa huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama ulikuwa ukiniona ninacheka wakati Mhe. Waziri akisoma yale maelezo ndio nikasema narejea tena *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma* na ametuambia mwenyewe Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Kwa kweli, Mhe. Mwenyekiti hayo maelezo nimeyasoma, na mimi kawaida yangu huwa sinyanyuki nikaripuka nimeshasoma, ndio nikajiuliza kwamba hivyo kuanzisha kamati nne za shehia nne na kutayarisha Ripoti ya *Food Balance Sheet* ndio milioni 85. Mhe. Mwenyekiti, tukitizama hizi ni shughuli za kiutawala kimsingi, ambazo katika bajeti ya Idara hii ya Uhakika wa Chakula na Lishe, na sikuzuia kule nimezuia katika fungu la Utumishi na Uendeshaji kwa sababu inahusu na wizara nzima.

Katika fungu la Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi, hasa, *actual* wamepewa milioni 140,400,000/=, mwaka jana makisio kwa sababu haikufika mwisho wa mwaka ni milioni 329,760,000/= shughuli za uendeshaji za idara na mwaka huu inaombewa milioni 172,188,000/= na hizi zilipangwa ziende katika shughuli ambazo zinazalisha tija. Kwa hivyo, tija yake ni kuundwa kamati hizi za shehia nne na Ripoti ya *Food Balance Sheet*.

Mhe. Mwenyekiti, tusidanganyane kwa sababu msingi wa kuletwa Sheria ya Hifadhi ya Chakula na hatimaye kuanzisha idara ya Hifadhi ya Chakula na Lishe katika wizara hii msingi wake ni kuwa na hifadhi ya chakula na sio maneno Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa kweli, mara nyingi Mhe. Mwenyekiti unatushauri hapa tuchunge fedha za walipa kodi, na sisi mara nyengine mijadala hii inachukua muda Mhe. Mwenyekiti kwa sababu ya mambo kama haya. Kwa mfano, unapokwenda katika nchi nyengine Mhe. Mwenyekiti zinawezekana mambo 90 yanakwenda sawa na 10 hayaendi sawa ndio unachukua muda mfupi kujadili, lakini hapa kwetu 10 ndio yanakwenda sawa na 90 hayaendi sawa tutachukua kila siku, kwamba siku 3 kwa ajili ya kujadili wizara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kwa nini tuendelee kuidhinisha na katika fungu la maendeleo nilihoji na bado kuna fedha katika suala la hifadhi ya chakula, na wala hatutaki kuona vikao na mambo haya yasiyokwisha, isipokuwa nielezwe hifadhi ya chakula itaanzishwa lini. *(Makofi)*

Hata hivyo, hoja zake zote Mhe. Waziri hazina msingi, kwa sababu kama nilivyosema walipotuletea mswada walijua kama tunakula mchele, sukari na unga, na walijua kama vinaharibika na wakatujibu wao hapa kwamba kutakuwa na utaratibu wake vyakula hivi vinafanyiwa *rotation*, yaani vinazungushwa, ili visifike pahala pa kuharibika.

Vile vile naomba niambiwe kwamba hii kamati tangu tumeiunda mwaka juzi kwa sheria imeshakutana mara ngapi tangu mwaka juzi, hilo na hifadhi ya chakula itaanzishwa lini. Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidiwe maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Mjumbe anachokitaka ni kuona kwamba ghala iko tayari na chakula kimo ndani na hilo ndilo analotaka kulisikia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunamuambia kwamba hivi sasa tunafanya matengenezo ya ghala ambazo baadhi ya fedha zitatumika katika matengenezo ya ghala hivi sasa, na tumepanga mipango yetu kwamba tutakamilisha Kanuni za Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe, kutayarisha miongozo juu ya usambazaji wa chakula cha dharura, tutafanya ukarabati wa ghala moja la uhifadhi wa chakula liliopo Unguja, kutoa mafunzo ya lishe kwa ngazi ya akinamama na wajawazito pia tumeeleza kwenye hotuba yetu.

Mhe. Mwenyekiti, najua kwamba hamu na kiu yake Mhe. Mjumbe kuona kwamba chakula kimo ndani ya ghala, na chakula kitakuwemo ndani ya ghala muda si mrefu ujao *inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda na jitihada ndio zinaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, bado nimeuliza hii kamati chini ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais (*muadhwamu*) imekutana mara ngapi tokea mwaka juzi tulipopitisha sheria hii na ikasainiwa na Mhe. Rais na hilo moja.

Pili naendelea kurejea yale yale hii sheria imeanza kazi tokea mwaka juzi Mhe. Mwenyekiti, kama ilikuwa mwaka mmoja wa kuweka misingi ya utawala wameweka, na mwaka jana wameunda kamati za shehia nne na kutayarisha *Food Balance Sheet*.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu ndio haya ametusomea kwamba *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma*, anatusomea kwenye kitabu ambacho na mimi ninacho na humu bado hamna hifadhi ya chakula, isipokuwa inazungumziwa

kuanzishwa kanuni za sheria, kutayarisha miongozi juu ya suala hili na haya ni mambo ya shughuli za kila siku za kiofisi.

Kwa kweli inasikitisha sana kwamba *program* hizi zinaingizwa kwenye *program* za maendeleo na ndipo tunapohoji kwamba hizi fedha za utawala zinafanya kazi gani, kama ikiwa kutungwa kanuni kunaingizwa kwenye fedha za maendeleo, kutayarisha miongozo juu ya usambazaji unaingizwa kwenye fedha za maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, haya si matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi, wananchi masikini, wanyonge wa nchi hii ambao tunawaambia mambo mengi waendelee kuchangia kila siku, lakini fedha huku zinatumika katika mambo kama haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bado naomba maelezo kwamba hifadhi itapatikana lini, na kikao au vikao mara ngapi imekaa kamati hii tangu tumepitsha mswada mwaka juzi? Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kwamba Mhe. Mjumbe anataka kuniuliza swali kwamba vikao vimeshakutana mara ngapi. Hilo swali mimi siwezi kulijibu kwamba vikao vimekutana mara ngapi.

Mimi ninachojua kwamba watu wa chakula na lishe wanajitahidi kuona kwamba lengo la sheria ile wanalifikia na wanalitekeleza. Hicho ndicho ninachokijua mimi. Nimeshazungumza nao kama mara mbili au tatu, wananambia kwamba jitihada wanaifanya na ndio maana sasa wanaelekea kwenye utengenezaji wa ghala ili waanze kuweka hicho chakula. Hivyo ndivyo ninavyojua mimi mpaka sasa hivi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kitabu cha mwaka jana haya haya yanarejea rejea ya kutengeneza ghala isiyomalizika. Lakini sitaki kwenda huko. Mimi nasema tena kuna mambo mawili ili shughuli zifanyike kwanza hiyo kamati. Kwa sababu umuhimu wa suala hili Mheshimiwa mimi katika uzoefu wangu mfupi tangu nimekuja hapa nimeziona tume mbili zikipewa viongozi wazito. Kwenye dawa za kulevya nimeona kwamba Makamu wa Kwanza wa Rais kafanywa Mwenyekiti ya Tume ya kupambana na dawa za kulevya. Tulihoji wakati wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza, kwa sababu sisi hatuchagui Mheshimiwa. Na katika hili kwa uzito wake akawekwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwa Mwenyekiti.

Sasa kama yeye hawezi kulijibu ndiyo hiyo inathibitisha hoja yangu jana hapa wakati nachangia kwamba wizara hii Mhe. Rais aione. Kuendelea kuazimwa Mawaziri kila siku utendaji utashuka. Sasa nataka Mwenyekiti wa Kamati yupo hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, bahati nzuri kwa kofia yake yeye

ndiye kiongozi wa shughuli za serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi atwambie yeye basi.

Na nasikitika maana si jambo la kumnyanyua yeye lakini tunapokuwa na Mawaziri namna hii itabidi twende huko. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atusaidie wamekutana mara ngapi na wanachukua hatua gani katika suala hili?

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi naielewa sana *concern* ya Mhe. Ismail Jussa, lakini nimuhakikishie kwamba tangu sheria hii ipitishwe na Kamati hii kuundwa imekaa kikao chake hivi karibuni, sikumbuki wakati gani. Na kikao hichi kinakaa kwa mujibu wa sheria. Kuna idadi ya vikao kwa kila muda fulani. Lakini kikao cha kwanza kimeshakaa tayari, tumejadili mambo haya na maamuzi yapo. Akitaka Mhe. Jussa tunaweza kumpatia hayo maamuzi yaliyofikiwa katika kikao cha mwanzo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Kwanza namshukuru nitakuwa mtovu wa shukurani kama sikumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kunipa taarifa hizo. Nashukuru kwa sababu siku ilipozinduliwa tulitangaziwa, tuliona hasa katika vyombo vya habari. Mimi ninachokiomba sitaki kuendeleza mjadala madhali kanyanyuka Kiongozi Mkubwa katika nchi hii.

Ninachokiomba hili naliomba wizara kwa sababu Mhe. Makamu wa Pili yeye ni kiongozi wa wizara zote lakini kwa hili kapewa jukumu la kisheria kuongoza, lakini watendaji wake *secretariat* yote kama mnakumbuka katika sheria *secretariat* ya kamati hii ni Idara ya Chakula na Lishe. Ninachoomba Mheshimiwa asimamie hili kwa sababu taswira za viongozi wetu hatupendi zichafuliwechafuliwe na uongozi wa wizara na Mhe. Rais atusikie sasa atupe Waziri wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba suala hili lifanyiwe kazi, tija ya mambo haya yasionekane kwa kuunda kamati nne za shehia na kuweka *food balanceship*. Yaonekane kwa kuwa na hifadhi ya chakula kwamba likitokea lolote la kutokea wananchi wa Zanzibar wana angalau usalama kwamba wanajua. Kwa mfano wa miezi kadhaa au miaka kadhaa tuna hifadhi ya chakula ambayo ipo ndani ya nchi kama ulivyokuwa ule msingi wa sheria.

Tukumbuke Mhe. Mwenyekiti, tulipoletewa Mswada ule tulikuwa tuna maelezo mengi moja ilikuwa kuna *crisis* katika dunia juu ya bei ya vyakula kutokana na mahitaji kuwa makubwa kuliko uzalishaji, tukasema kila nchi imejipanga kuweka hifadhi yake. Tuambiwe hilo kwamba Wizara itakwenda kujipanga ione kwamba hili sasa linafanyiwa kazi, tumechoka na maneno tu. Mhe. Mwenyekiti, sijaridhika lakini kwa indhari hiyo kwamba serikali

italifanyia kazi mwakani tusije tukapata tena hadithi hizi za nahau na nyimbo za kufundishwa ambazo hazikeshi ngoma katika Baraza hili. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea haya yafanyiwe kazi.

Kifungu 1301 Idara ya Uendeshaji na Utumishi 1,130,634,000
Kifungu 1401 Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe

Mhe. Panya Ali Abdalla: Nilipokuwa nikichangia idara hii nilimuomba Mhe. Waziri anieleze amewashajihisha vipi wakulima wetu kuhusu kupanda mbegu zile zinazoweza kuvumilia ukame. Hasa ukizingatia hali hii ya mabadiliko ya tabia nchi. Lakini pia vipi amewashajihisha wakulima kuweza kujiwekea hakiba ya chakula kwa sababu ya kuweza kuwa na uhakika wa chakula. Mheshimiwa jibu sikulisikia au sijui kwamba *echo* zetu humu ndani. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri anipatie maelezo, kwa sababu ni lazima tuwe na uhakika wa chakula.

Zile siku za nyuma mimi nilikuwa nakumbuka kwamba wizara hii hata kabla ya kuwa tunataka kujiwekea utaratibu huu wa chakula, lakini ilikuwa ina utaratibu kwa wakulima pale tunapomaliza tu kuvuna kilimo cha mpunga basi tulikuwa tunawashajihisha wakulima kwa kuwapatia mbegu za kunde. Lakini pia tulikuwa tunapatiwa mbegu za mahindi ili tulime mahindi hayo kwa kujiongezea chakula.

Basi nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri vipi amejiandaa ingawa amesema yeye *nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma*. Lakini kwa umuhimu wa suala hili tumuomba Mheshimiwa atupatie majibu ili tuweze kuwa na uhakika wa chakula na lishe.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Nakumbuka nimemsikia Mheshimiwa Mjumbe alipokuwa akizungumza suala hili la kuwaelimisha watu wetu juu ya kujua namna ya kulima chakula na kujiwekea hakiba wao wenyewe. Ni wazo zuri na nalikubali kabisa.

Halafu vile vile kuna suala la mbegu za mpunga ambazo ni za kustahamili ukame. Mheshimiwa hili Wizara ya Kilimo inawaelimisha wakulima kupanda mbegu au mazao yanayoweza kustahamili ukame. Tatizo tunalolipata katika kazi hii ni mazoea ya wakulima wetu. Wakulima wetu wameshazoea kulima mbegu zao za zamani, kwa hivyo hata ukiwapelekea hizi mbegu za kisasa mara nyingi wanakuwa wanazikataa. Lakini bado wizara itaendelea

kuwaelimisha wakulima wetu kuhakikisha kwamba wanalima mbegu za kustahamili ukame na zinachanua kwa muda mfupi.

Kutokana na hali ya hewa yetu tuliyonayo hivi sasa, kuna baadhi ya mbegu ukipanda leo huivuni, haitochanua kwa sababu ya hali ya mvua inavyokuja. Aidha itakuja nyingi kupindukia au zitakuja kwa upungufu, ndio tatizo tunalolipata kusema kweli. Kwa hivyo nakubaliana na mawazo yake juu ya suala hilo.

Ni kweli lazima tufanye jitihada ya kuwaelimisha wananchi wetu kuweka hakiba ya chakula na kulima vyakula vinavyostahamili ukame na wawe na hakiba za kutosha. Wakianza kujiwekea wenyewe katika majumba yao basi tatizo litapungua. Halafu tena ukija uwekaji wa serikali litakuwa tatizo linapungua zaidi na linaondoka kabisa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pia nimuombe aongeze jitihada kwa sababu mimi nimeshuhudia kwa sasa mahindi tunayolima yanaishia katika kuchomwa na kuuzwa sana. Hii inakatisha tamaa kuona kweli ikitokea dharura ya ghafla tutatishindwa sisi kujikimu na chakula.

Namuomba sana Mhe. Waziri tushirikiane kwa pamoja kuona wakulima wetu hawa tunawapatia elimu hii ya kujiwekea hakiba ya chakula na tusiendelee kuyauza mahindi mabichi. Zamani mahindi mabichi tulikuwa tunavuna kidogo tu kiasi ya kuonja tu mahindi yale ya kuchoma. Lakini sasa hivi imekuwa ndio mradi mkubwa, yote yanavunwa majichi. Nilikuwa nasisitiza hilo tu Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Spika: Jitihada izidishwe tunaendelea.

Kifungu 1401

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili la Idara ya Chakula na Kuweka Chakula cha Hakiba, nilipokuwa natoa maoni yangu na kutoa michango yangu kwenye wizara hii niliomba kutoa maelekezo na Mhe. Waziri ametoa maelekezo pamoja na ndugu yangu Ismail Jussa ameelezea kwa kirefu sana.

Ninachokiomba katika Idara hii ya Chakula la Lishe, pamoja na mambo yote yanaliyokuwepo naomba kitengo hichi ukiongezee nguvu ili kiweze kufikia malengo yanayokusudiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri ushauri.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nimeupokea.

Kifungu 1401	Idara ya Chakula na Lishe	172,188,000
Kifungu 1501	Idara ya Kilimo	

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Nimebahatika kuchangia katika njia zote mbili nimeruhusiwa, nilipochangia kwa maandishi hii Idara ya Kilimo nimegusia juu ya madereva wa matrekta wengi wao ni wale wenye elimu za chini na wameajiriwa zamani na maslahi yao ni madogo mno. Nilitaka kujua kuna mpango gani wizara iliyopanga kuwasaidia wafanyakazi hawa hasa ukilinganisha kwa wengine wapo ukingoni na kustaafu na bado maslahi yao ni madogo.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, wizara inalipa mishahara kwa mujibu wa matoleo ya Utumishi mbali mbali yanayotolewa kutoka Idara Kuu ya Utumishi Serikalini. Sisi tukipata ruhusa ya kuongeza maslahi yao bila shaka tutawaongezea na wala hatutokuwa wakaidi kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, anaposema maslahi madogo sijui kama ni mshahara au kiinua mgongo au mambo gani. Lakini kusema kweli mishahara yote inatoka kwa mujibu wa mfumo unaotolewa na Idara ya Utumishi Serikalini, yaani Idara Kuu ya Utumishi Serikalini ambayo ni Idara ya Utumishi wa Umma.

Mimi nakubaliana na hoja yake kwamba mishahara midogo, na ni kweli pesa haitoshi hata ukimpa mtu kiasi gani pesa haimtoshi bado ataendelea kusema ndogo. Mimi nakubaliana kwamba wanaweza wakalalamika kwamba mishahara midogo lakini tujue kwamba tunafuata utaratibu wa Idara Kuu ya Utumishi Serikalini katika kulipa mishahara yetu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini pamoja na kuwa najua kuwa Wizara ya Utumishi ndiyo inayopanga maslahi ya wafanyakazi wote, lakini kina wizara inawaangalia watumishi wake. Watu hawa Mhe. Spika, wameitumikia serikali kwa muda mrefu na maslahi yao ni duni.

Labda niirudishe kwa Utumishi Serikalini madereva hawa wa matrekta wataangaliwa vipi maslahi yao, mtu aliyeajiriwa miaka 30 nyuma au 25 ikawa ndio takriban mshahara wake mdogo mno, sijui tunawafikiria vipi watumishi wetu hawa. Kama Mheshimiwa anayehusika na Utumishi ningeomba utumishi serikalini iwasaidie hawa kuwafanyia *scheme* ili wakitoka wajisikie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mohammed Haji Khalid kwa suali lake hili ambalo amekuwa akilizungumzia nakumbuka hii ni Wizara ya tatu analizungumzia suala hili. Lakini ieleweke kwamba serikali ikishatoa *statement* maana yake *statement* ile inahusu kwa serikali nzima. Sasa tukihitaji kwamba kila Wizara au kila idara tutoe *statement* yake haiwezekani, maana *statement* ni ile ile moja.

Nilipokuwa nikiwasilisha bajeti yangu nilisema serikali katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 ina mpango wa kuwaongezea mishahara wafanyakazi ambao hawana sifa za kielimu lakini wameitumikia nchi hii katika kipindi cha muda mrefu. Na juzi wakati nilipokuwa nikisaidia majibu kwenye Wizara ya Habari nilisema kwamba serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuwaongezea mishahara hao wafanyakazi ambao hawana sifa za elimu lakini wameitumikia nchi hii katika kipindi cha muda mrefu.

Mimi nitawaomba Waheshimiwa kwenye suala lolote linalowahusu wafanyakazi ambao hawana sifa za kielimu, serikali tayari imeshatoa maelezo kwenye wizara zaidi ya tatu. Nafikiri Mhe. Mohammed awe anafikiria na zile kumbukumbu za bajeti nyengine tunazozipitisha hapa na *statement* ambazo tunazitoa. Mhe. Ismail Jussa huwa anasisitiza hapa, kwamba tusisahau yale maelezo ambayo huwa tunayatoa hapa, mimi nimeshasimama zaidi ya mara tatu au mara nne kulizungumzia jambo hiko. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Mhe. Waziri wa Utumishi kwa maelezo yake yaliyoonesha msisitizo. Kwa kuwa mara hii serikali imeamua kuwaongezea wafanyakazi ambao hawana sifa maalum, naomba tuendelee.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa kuwa kazi tuliyonayo ya kujadili hoja ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili bado haijamalizika na ni muhimu tuimalize hii leo. Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu litenge kando kanuni ya mda mpaka tutakapomaliza kupitisha vifungu hivi katika Kamati ya Matumizi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kazi iliyobaki sio kubwa kwa wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kabla sijaomba ufafanuzi kwanza nitoe shukurani kuwa Mhe. Waziri kanijibu kwa vyote vile nilivyochangia, hoja zangu kanambia zitachukuliwa na kufanyiwa kazi. Lakini kuna mambo hapa hayakukaa vizuri naomba nipate ufafanuzi.

Nilichangia kutaka kujua kuhusu kilimo cha mpunga. Kwa mujibu wa taarifa ya kitabu kinasema kuwa hali ya uzalishaji ilipungua kwa mpunga kutoka tani 23,702 mwaka 2011 hadi tani 6,372. 1 mwaka 2012. Kitabu kimeeleza kuwa sababu ni upungufu wa eneo lililolimwa kwa vile lilivamiwa kwa kulimwa mananasi pamoja na mboga mboga. Pia upungufu wa mvua uliosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa, maradhi na wadudu waharibifu wa mazao na upungufu wa rutuba katika maeneo ya kilimo.

Ukurasa wa 5 umesema kuwa taarifa ya hali ya hewa kwa kipindi hichi hichi cha mwaka 2012/2013 ni za kutia moyo hasa kwa kilimo cha mpunga, kutokana na hali hiyo kwa msimu wa mwaka 2012/2013, mavuno yanakadiriwa kufikia zaidi ya tani 30,000 za mpunga. Huku imesema tani 30,000 kwa mwaka huu, na huku zilizovunwa ni tani 6 na kidogo kama ilivyoelezwa. Kwa hivyo nataka nijue kwanza iliyo sahihi ni ipi? Ni hii huku iliyowekwa pamoja na mazao mengine au ni hii iliyofuatiwa baadaye?

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, sina hakika anakusudia paragrafu gani angelinisaidia nikaiona hiyo paragrafu yenyewe nikapata kuitolea jibu. Nisaidie Mheshimiwa hiyo paragarafu uliyoizungumza.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Taarifa ya mwanzo iko ukurasa wa 4 kuanzia kifungu 112 - 114 hii inachukua mazao mengi lakini hapa mimi nazungumzia mpunga ndipo ilipoeleza kuwa mwaka 2011 mazao ya mpunga yalivunwa tani 23,702 na mwaka 2012 ni tani 6,372.1 kaeleza kuwa kilimo kilipungua.

Halafu kifungu cha 114 ukurasa wa 4 ndio kaeleza hizo sababu tatu ambayo inamalizikia ukurasa wa 5.

- "Upungufu wa eneo lililolimwa kwa mazao ya muhogo, migomba na viazi vitamu kwa mwaka 2012/2013 kutokana na uvamizi wa maeneo ya kilimo na wakulima kujikita zaidi katika kuzalisha mazao ya mananasi na mboga mboga."

Yaani eneo lilitumiwa kwa mazao mengine. Halafu akatoa sababu ya pili ukurasa wa 4 chini kabisa ni:

- "Upungufu wa mvua uliosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa."

Sababu ya tatu ya kushuka kwa kilimo ni

- "Maradhi, wadudu waharibifu wa mazao na upungufu wa rutuba katika maeneo ya kilimo."

Kifungu nambari 1.16 ukurasa wa 5 ndio ulioeleza taarifa nyengine kabisa naomba niisome kwa ruhusa yako kama ilivyo.

"Mheshimiwa Spika, taarifa za hali ya hewa katika kipindi cha miaka 2012/2013 ni za kutia moyo hasa kwa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua. Takwimu zinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la mvua za masika mwaka 2012/2013 ambazo zimenyesha zaidi ya wastani wa kila mwaka. Hali hii imeimarisha kwa kiasi kikubwa ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua ambapo sehemu kubwa ya kilimo hicho kimeimarika vizuri na kuleta matumaini ya kupata mavuno mazuri. Kutokana na hali hiyo, kwa msimu wa mwaka 2012/2013 mavuno yanakadiriwa kufika zaidi ya tani 30,000 za mpunga."

Sasa maelezo ya huku na huku ni tofauti, na hichi kitabu kimetungwa kitaalamu. Kwa hivyo tunaomba tujue tufuate wapi.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mheshimiwa napata tabu kweli kulifahamu swali lake. Isipokuwa tulichokieleza ni kwamba msimu uliopita mpunga hatukuupata kwa wingi kutokana na sababu hizo ambazo zimeelezwa. Lakini msimu unaovunwa hivi sasa watu wapo mabondeni wanavuna. Msimu huu tunategemea kwamba mpunga utafika kwenye tani 30000, tafauti na zile tulizozitaja katika msimu uliopita, ndicho tulichokusudia. Sasa kama tarehe zimekosewa atatusamehe katika hilo, lakini tunakusudia kwamba msimu uliopita mpunga haukupatikana kwa wingi, lakini msimu huu unaovunwa sasa hivi mpunga utapatikana unategemewa tani 30000.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri sana lakini sisi tunaangalia kile kilichoandikwa na kimeandikwa na wataalamu. Hakuna humu msimu uliopita wa mwaka 2012 wala msimu ujao wa mwaka 2013 tunaangalia ile *consent* ilivyo ndio tukauliza. Sasa ikiwa ni hivyo kakubali kuwa kimeandikwa kimakosa ili tuendelee.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nimesema kabisa nakubaliana na hoja yake kama kuna tarehe ambayo imeandikwa imekosewa, lakini tulichokikusudia hasa ni msimu uliopita hatukupata mpunga mwingi kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa. Msimu huu hali ya hewa imekuwa nzuri ambapo bado hatujamaliza kuvuna hatujajua tumepata kiasi gani, lakini tunategemea kufika 30,000. Sasa kama kuna kosa hilo nakubali kwamba lile kosa la kibinaadamu litakuwa limefanyika kimaandishi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, namaliza lakini namalizia hivi, hivi hizi mvua za masika zina misimu mingapi? Naona kitabu hichi kinatungwa mwezi huu ni wa Julai, masika yaliyopita ni mamoja tu, kuna masika mangapi?

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri anachokusudia msimu wa mvua za masika, mavuno yake ndiyo haya yanayovunwa yake ndiyo haya yanayovunwa hivi sasa. Na mategemeo ndio hizo tani 30,000.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, angelisema mfumo wa masika wa 2011/2012 mazao yalikuwa haya mvua haikunyesha, huu wa safari hii 2012/2013 ingelikuwa ni sahihi, na hiyo nayo pia ingelikwenda kinyume na maelezo ya kifungu cha mwanzo. Kwa hivyo kwa vyovyote akubali kuwa kuna makosa na wataalamu hawakumsaidia, ili tuendelee.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nimesema kama kuna tatizo la kuandika hizi tarehe nimelikubali tangu mwanzo. Lakini desturi ya mpunga unavunwa katika kipindi hichi cha baridi, na ndio maana zamani tulivyokuwa wadogo tunaita makapu kwa mpunga mpya, ndio huu unaovunwa sasa hivi. Ndio nilichosema hicho, kwa hivyo kama kuna tatizo limekosewa nakubali hilo kosa kwamba pamekosewa ni makosa ya kibinaadamu, nakubali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa kwa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri anieleze kuwa wenzetu wa JKT msimu uliopita walitukopesha matrekta yao. Je mpaka sasa hivi wizara yake imeshalipa kiasi gani ili na msimu wa ujao twende tukakope kwa wingi ili tusichelewe kuwalimia wananchi kwa wakati unaofaa. Naomba jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nadhani katika swali la nyongeza pia nililijibu. Alisema kwamba tuna upungufu wa matrekta na tumekopeshwa je, tutaweza kulipa matrekta hayo katika msimu huu ili tuweze kuja kukopa mengine tupate ongezeko la matrekta.

Mhe. Spika, nilimueleza kwamba tunategemea tutakapoipata bajeti yetu vizuri basi tutapunguza deni la matrekta. Kwa sababu hayo matrekta hayatutoshi, kila tukipata kukopa tukipata kwa wingi tutapata kufanikiwa kulima kwa vizuri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Mhe. Jussa alitoa dua nzuri sana akasema kuwa Mhe. Waziri basi atafutwe mtu apewe Uwaziri naipokea, *inshaallah* dua hiyo inikute mimi nipate Uwaziri wa Kilimo. Lakini nakubaliana naye Mhe. Naibu wangu waziri kwa suala hilo kuwa yuko tayari kuwalipa ndugu zetu wa JKT kwa kweli ni suala ambalo linatia moyo na *inshaallah* ajitahidi na bajeti hii tutaipitisha sasa hivi hatupigi tena buti ili zipatikane fedha za kununua trekta.

Lakini la mwisho nimshukuru sana Naibu Katibu amenileta ki-*memo* hapa kuwa suala la Kilombero na Pangeni masuala yameisha na sasa hivi wakati wowote pesa zitapatikana kwa kujenga miundombinu ya kufikisha maji kwa kumwagilia. Ahsante sana ninamshukuru sana.

Kifungu 1501 Idara ya Kilimo 5,649,736,000
Kifungu 1701 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nilipochangia nilisema kwamba nifafanuliwe vizuri sasa hivi ni miaka 49 kituo cha utafiti Pemba hakiko kitajengwa lini? Na kama kipo kimefikia wapi? Wakati kule nako kuna mazao nayo muhimu, ni kisiwa vile vile kina *green island and fertile island.* Sasa nataka ufafanuzi sasa hivi miaka 49 keshokutwa tunatimia miaka 50, hivyo kweli tunakipa kipaumbele tukasema kilimo ni uti wa mgongo na dhamira ya Rais ni nzuri ndio maana akabagua Wizara hii, naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi hapa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikijibu masuala haya nilitoa ufafanuzi juu ya kituo cha utafiti cha Matangatuani. Lakini nakubaliana kwamba sasa tuko miaka 49 katika utawala nilikuwa napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi tu ni kwamba tunaye muda mrefu katika serikali anajua wakati gani hali ilikuwa nzuri na wakati gani hali ilikuwa mbaya maana yake yumo katika serikali kwa muda mrefu kabisa, kama kumpita labda nimempita kidogo tu, lakini ni mtu ambaye yumo muda mrefu katika serikali.

Kituo cha Utafiti Matangatuani kilikuwa ni kituo kizuri sana wakati ule hali ya uchumi ni nzuri, na kilikuwa kinafanya utafiti wa aina mbali mbali pale Matangatuani, na kilikuwa kina sifa katika Afrika nzima kituo cha

Matangatuani kama kilivyokuwa kina sifa kituo cha Kizimbani. Hapa katikati tulipoanguka kwenye masuala ya kiuchumi, sio kituo cha Matangatuani kilichoathirika lakini hata cha Kizimbani nacho kiliathirika. Hivi sasa tumechukua hatua ya kukifufua kituo cha Kizimbani na sasa hivi kidogo kinakaribia kufika katika hali yake pamoja na kuanzisha chuo pale. Na nimesema katika majibu yangu kwamba hivi sasa tunafanya jitihada ya kukifufua Kituo cha Matangatuani na tumepeleka watu wawili pale wenye ujuzi mkubwa wa kilimo kwa ajili ya kusaidia kukifufua Kituo kile cha Matangatuani ili kiweze kufanya kazi nzuri kama kilivyokuwa kikifanya kazi nzuri hizo siku za nyuma. Hicho ndio nilichokusudia kukisema na nimesema katika masuala yangu, na pia tunazungumza mashirika mbali mbali ya maendeleo kwamba walitusaidia muda mrefu katika kituo cha Kizimbani na sasa hivi tunataka waje kutusaidia pia katika Kituo cha Matangatuani.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasimama sijaridhika na majibu ya Mhe. Waziri, ninajua na mimi pia ni wa muda mrefu katika serikali hii, na katika mambo ambayo tunafuatilia tunafuatilia, lakini si vyema kwa kweli na nitoe pongezi za dhati kabisa katika kituo hichi, jinsi kuna vitu viwili ambavyo wanavifanya ndio maana nikasema kitafanyiwa ukarabati lini sasa hivi miaka 49? Lini angalau basi anidanganye anambie katika kipindi cha mwaka huu lakini lini Mheshimiwa na hiki kituo ni muhimu ambayo yeye mwenyewe kasema kwamba huko nyuma sisi kituo kimetusaidia, sasa ni lini?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nilisahau kwamba hivi sasa tuko katika zoezi la kukifanyia ukarabati kituo cha Matangatuani na ndio maana juzi tu tumepeleka wataalamu wawili wa kilimo watusaidie kutupa ushauri lipi na lipi na lipi tulirejeshe katika kituo cha Matangatuani, hivi sasa tunaendelea na kazi hiyo. Nilisema wakati nilipokuwa niki-*wind up* hiyo kazi inaendelea hivi sasa hivi na kwenye bajeti ya mwaka huu tutafanya marekebisho makubwa katika kituo cha Matangatuani nacho kirudi kama kilivyorudi kituo cha Kizimbani.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, tukimaliza bajeti, tukishamaliza kula na sikukuu Mungu akitujaalia uhai na uzima tufuatane twende Pemba niende nikakione Kituo cha Matangatuani ili nihakikishe maana ya kuambiwa tutafanya, tutafanya hivi, tuko tayari, tuko tayari naona hayamaliziki kila siku tutadanganywa namna hiyo Mhe. Mwenyekiti. Akikubaliana na mimi hapo ninakubali, hakubali ninazuia.

Mhe. Mwenyekiti: Ninaamini Waziri hakatai hilo ila mnavutiana kwa sababu, Mhe. Jaku yuko wapi, na yeye anataka hivyo hivyo pia ndio

alivyoahidi kwamba mara baada ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, kwa hivyo msivutiane mkaja mkamuumiza lakini naamini hilo hakatai.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti mimi si mkaidi kwa Bi Asha kabisa, bila shaka kama tutakwenda kesho au kesho kutwa tutakuta hatua hazijafikia hizo anazotaka kuziona yeye. Maana anataka kituo kile kiwe kizuri na kirudi katika ile hadhi iliyokuwepo zamani, nasema ni kituo ambacho kilikuwa na sifa. Sasa mimi si mkaidi hata kidogo kwenda, lakini sasa hivi kidogo itakuwa kumaliza suala hili kumaliza sikukuu. Mimi niko tayari kufuatana na yeye kabisa twende Matangatuani hapana tatizo lolote, mimi niko tayari twende na maofisa tayari wapo pale tumeshawaweka wawili, na wao sasa wapo katika *working paper* ya kutengeneza kipelekwe nini na nini ili kituo kirudi katika hali yake. Tunatekeleza sera yetu ya Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilikuwa sijui kama Mhe. Rama hana ukaidi na Mhe. Asha.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti kwa sababu Mhe. Rama lazima nimstahi alikuwa Waziri wangu basi ninamkubalia, tukishamaliza mambo yetu haya yote ya kupitisha bajeti na sikukuu,basi tutafuatana na wataalam tutakwenda, mimi sina matatizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Laiti ingelikuwa Mhe. Mwenyekiti katiba inaruhusu kuwa Waziri mmoja kuongoza Wizara mbili basi ningemuomba Mhe. Rais huyu bwana anayejibu masuali leo ampe yeye hii Wizara hii amuongezee hii Wizara Mheshimiwa. Baada ya dibaji hiyo Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Mwenyekiti wakati ninachangia nilieleza masikitiko yangu sana na nika-*declare interest* kwamba mimi ni mkulima. Nilieleza masikitiko yangu sana kwamba hili zao la karafuu liliingizwa hapa tangu karne ya 17 na bwana mmoja anaitwa Saleh Buhareren huyu mfanyabiashara wa Ki-Oman. Na la kusikitisha ni kwamba sasa mikarafuu ile imekuwa mikubwa sana na wachumaji wa karufuu Mhe. Mwenyekiti katika maeneo yetu wengi ni akinamama, hawawezi sasa kuupanda huu mkarafuu ulioletwa na Saleh Buhareren tangu karne ya 17 kuupanda juu na wakazichuma karafuu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nauliza swali langu (a) kwamba mimi nina *knowledge* kidogo ya *plant anatomy and physiology* sasa nyie wataalam wetu hamuwezi kutusaidia mkatoa chotara wa mikarafuu ambayo itakuwa ni *affordable* kwa hawa akina mama kuweza kuipanda na kushuka? Kwa sababu sisi katika awamu ya pili sisi hapa tulipokuwa madarakani tuliweza kuondosha hii minazi mrefu *East African Tall* tukaleta minazi chotara, je

nyinyi wataalam wetu wa siku hizi mtashindwa kutuletea mikarafuu chotara watakayo-*afford* hawa. *That is* (a) Mhe. Mwenyekiti.

(b) Mimi ni mkulima wa tungule katika kijiji cha Vitongoji Mhe. Mwenyekiti, na nilisikitika sana kwamba katika kipindi cha mavuno tunalazimika kuuza zile tungule zetu kwa bei ya kutupwa jambo ambalo ile dhana ya SMZ ya kupunguza umasikini na kuongeza kipato inakosekana kwa sababu tunalazimika kuuza kwa bei ndogo sana.

Sasa Mheshimiwa, wataalam wetu hawa watatuletea utaratibu upi ambao utatuwezesha ku-*store* aidha hizi tungule zetu zikasubiri soko au kuushawishi ulimwengu wakaweka *Canning Industry* kuwauzia hao wawekezaji vile viwanda vya kushindika tungule watatufanyia tafiti hizi kiasi gani.

(c) Nimalizie kwa nerica kwamba ukiipanda katika ukanda wa magharibi inakuwa vizuri na ni *productive,* lakini ukiipanda katika ukanda wa Mashariki kuanzia Muwambe mpaka kwetu huku Mheshimiwa mpunga ule hauzai sana unakuwa tatizo. Je, nyinyi wataalam hamuwezi kuzalisha nerika mbili yaani nerika 1(a) ikawa ni *special* katika *loamy soil* na nerica 1(b) ikawa huku kwenye *acidic soil* huku kwetu ukanda wa maweni hamuwezi kutufanyia hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti Mhe. Saleh Nassor mkwe wangu, kuhusu suala la nerica kwa upande wa mashariki wakati nilipokuwa nikijibu suala lake kwamba suala la mashariki Pemba kwamba utafiti umefanyika kuhusu upandaji wa mbegu ya nerica ndio maana katika mabonde ambayo niliyokuwa nimeyataja katika sehemu ya mabonde Tovuni Kiungoni, Gombeume, Mchangamdogo, Mfubaha, Vitongoji na Chanjaani, na Chambani huku kumeonesha kwamba matokeo yaliyoonekana katika mbegu hii ni matokeo mazuri. Bila shaka wataalamu wamefanya utafiti huu ndio ikaonekana kuwa upande huu mashariki mbegu ya nerica imeimarika vizuri. Kwa hivyo Mhe. Saleh naomba uwaamini watafiti wetu kwamba utafiti huu wameufanya na matokeo ambayo hiyo sehemu iliyotajwa zimeonesha matokeo mazuri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili):
Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh anaposema anatumia sauti kali kiasi ambacho *echo* ya hili jengo letu inatufanya sisi hata tukisogeza sikio letu hapa hatumpati vizuri, ninajua kauliza suali la karafuu na utafiti wa karafuu lakini kakusudia nini sikumpata vizuri, namuomba radhi kama atarejea kunieleza ili niweze kumjibu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mikarafuu waliitaja kuna mikarafuu mengine ni mirefu mno kwamba akina mama ambao ndio wachumaji wakubwa inakuwa tabu sana kuipanda. Sasa watafiti wetu je hawawezi kufanya utafiti wa kupata mikarafuu ambayo itakuwa labda imetandawaa mifupi kidogo hivi, ikawa rahisi kuweza kuchuma. Nadhani ndio alilokusudia hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili):
Mhe. Mwenyekiti nataka kumjibu tu Mhe. Mwakilishi kwamba suala la utafiti wa mazao kama mikarafuu kusema kweli inachukua muda mrefu mpaka ukaweza kupata hiyo aina unayotaka wewe ya mkarafuu mdogo. Lakini Mheshimiwa kama tunataka karafuu kwa wingi basi ni vizuri kuwa na mikarafuu hii mikubwa ambayo ina uzazi mkubwa sana. Mikarafuu midogo mara nyingi haitoi karafuu nyingi sana, inakuwa mikarafuu yenyewe ni kama ninavyosema tunayo mikarafuu inapoanza kuzaa watu wanachuma kwa ngazi tu wanaweka ngazi halafu wanapanda wanachuma, inapokuwa midogo tunafanya kitu namna kama hicho lakini uchumaji unakuwa si mkubwa. Kwa hivyo ni vizuri kupata mikarafuu yetu tuliyonayo, hii mikarafuu yetu inatoa karafuu nyingi zaidi kuliko mikarafuu midogo midogo anayoitaka.

Lakini hata hivyo utafiti unaendelea kuweza kupata mikarafuu ambayo anaitaka lakini mikarafuu yetu nayo sasa hivi inatoa karafuu nyingi sana na mikubwa, maana yake unajua wewe ukikaa katika tawi moja unajaza gunia. Lakini mkarafuu mdogo utauchuma wote bado hujajaza gunia. Kwa hivyo ninalikubali wazo lake anataka kinamama nao wapate mikarafuu midogo midogo ya kuchuma. Ukiendeleza kupanda mikarafuu katika hali hii tuliyoendelea nayo tunaweza tukafika katika kiwango hicho.

Mikarafuu mifupi itakuwa na mavuno madogo sana na sisi tunahitaji mavuno mengi zaidi, tunaendelea na utafiti wa kuongeza mavuno na kuongeza ubora wa karafuu, programu ipo ya kusarifu mazao na kutoa fedha vijijini, Mhe. Mwakilishi awahamasishe tu wananchi ili wajiunge katika vikundi na utafika mradi eneo lake wataje mahitaji yao ili wasaidiwe namna ya kuongeza thamani bidhaa za tungule au nyengine. Hili suala la tungule limejibiwa pamoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti mikarafuu iliyopo inazaa sana kweli, lakini sasa uchumaji wake kwa sababu wanawake hawaiwezi inabidi karafuu zianguke na badala yake hiyo thamani ambayo tunaitegemea kuipata kutokana na karafuu zile zikidondoka chini zinakuwa mpeta na zinakosa soko katika soko la ulimwengu zinakosa thamani. Sasa je, kuvuna zilizokuwa sio nyingi lakini zina *quality* na kuziokota hizi zenye mpeta hazina *quality* sijui

ipi ni nzuri zaidi, kwamba tunauza kidogo lakini kwa bei kubwa. Lakini tunauza nyingi hazina bei kwa sababu zimekuwa mpeta ipi nzuri zaidi?

Na halafu lile suali langu hakulijibu lile la tungule sasa anambie kwamba ni bora tuuze nyingi lakini zimepoteza sifa au tuuze kidogo zenye sifa nataka anipe jibu hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mheshimiwa hiyo nadhani isingekuwa hoja, anachosema Mhe. Waziri mikarafuu hii iliyopo mikubwa, inatoa mazao mengi, hata hivyo utafiti unafanyika hicho ulichokiomba hicho kinafanyika utafiti huo, lakini ni utafiti ambao unachukua muda mrefu, sasa miji nadhani tena hapo uachie. Kwanza nilikustahmilia sana naona hili nikwambie hizi hoja umechukua nyingi wakati tayari tumeshamaliza. Tuendelee zimekwisha hoja.

Kifungu 1701 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo 967,498,000
Kifungu 1702 Idara ya Mipango Sera na Utafiti Pemba

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti wakati ninachangia nilizungumzia kilimo cha chumvi na katika majibu ya Mhe. Waziri alinambia kwamba kilimo cha chumvi hakimo katika Wizara yake na Mhe. Mwenyekiti mimi mchango wangu niliutoa kwa kusema sikuutoa kwa maandishi, kwa hivyo chumvi haiko katika Wizara ya Kilimo ilikuwa Waziri muhusika anijibu masuala yangu. Na suala langu niliulizia kwanza hii chumvi iko Wizara gani na pia niliomba anambie huyu muhusika wa chumvi kule ambaye ni mtaalamu jina lake ni nani na anawasaidia vipi wakulima wa chumvi. Lakini Mhe. Mwenyekiti sikupata jawabu kwa hivyo naomba nipate jawabu ya suali hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, suala la mazao ya baharini moja kati ya chumvi ni zao la baharini, lakini nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kuwa suala lake tumelisikia na tunalichukua mimi nitafanya ziara kwenda kuwaona wananchi wale ili tujue tatizo linalowakabili, ili serikali basi iweze kuwasaidia na iwe karibu sana na wakulima wa chumvi. Nilitaka asiwe na wasiwasi na suala hilo tutalichukua kwa karibu zaidi.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti kwanza naomba kabla ya kuendelea na hoja nieleze kidogo maneno ya msanii mmoja aliyezungumza kuhusu chumvi. Msanii huyo Mhe. Mwenyekiti alisema:-

"Chumvi ninaipa pole hakika inaonewa, sijasikia milele chumvi pongezi kupewa, chumvi tangu hapo kale katu haijasifiwa." Mhe. Mwenyekiti msanii huyo pia aliendelea kwa kusema "Chumvi ni kitu muhimu hapana asiyejua,

haifanyiki karamu bila ya kununuliwa, pilau haiwi tamu bila ya chumvi kutiwa".

Mhe. Mwenyekiti nina masikitiko makubwa kwa sababu Wizara ya Mifugo na Uvuvi tayari imeshapita na katika kitabu chake hatukuona hata pahala pamoja ilipozungumzia suala la chumvi. Na wananchi wa Pemba wengi wanazalisha chumvi na wanahitaji elimu, na vile vile nilizungumzia kuhusu kusaidiwa kutafuta soko na ninaamini kwamba mwani uko katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi lakini ukishazalishwa wanaoshughulika ni Wizara ya Bishara, na ikiwa chumvi iko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ikishazalishwa hiyo chumvi anayehusika ni Waziri wa Biashara kwa sababu ndiye mtu wa masoko. Na vile vile chumvi Mhe. Mwenyekiti huwa ina athari. Kwa hivyo pia Wizara ya Afya hapa ina haki ya kusaidia wakulima wa chumvi kuwapa elimu. Na Waziri wa Uwezeshaji ana haki ya kuwawezesha wakulima wa chumvi, lakini Mhe. Mwenyekiti Wizara karibu zote hizo zishapita hatukuisikia chumvi kutajwa na Mawaziri wapo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti naomba Waheshimiwa Mawaziri wanipe maelezo kuhusu chumvi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kunipa fursa hii na mimi kueleza machache tu kuhusu chumvi. Kwanza nampongeza sana Mwakilishi kwa kuwa mtetezi wa chumvi. Mhe. Mwenyekiti Wizara ya Biashara inashughulikia masoko ya chumvi, kule Pemba tumewasiliana na NGO's nyingi sana ambazo kwamba zinazalisha chumvi. Wanamiliki kiwanda kimoja pale Wawi ambacho kinasaga chumvi na kutia *iodine* ambayo walipewa msaada na Unicef karibu gunia laki tatu, kwa bahati mbaya chumvi yao waliyotoa inarishai haiko *dry*, kwa hivyo wanakosa *drier*. Kwa hivyo sisi tumeajiri Shirika la Tildo kutoka Tanzania tumewalipa karibu milioni thalathini kwenda kufanya utafiti wa kiwanda kizima cha chumvi kuanzia mashine ya kwanza mpaka ya mwisho ili tuwasaidie kuwapatia *system* nzima na mafunzo maalum ambayo kwamba yatasaidia kutoa chumvi ambayo itakuwa na viwango. Chumvi hiyo itakuwa na viwango itakayokuwa na muhuri wa ZBS *Zanzibar Bureau of Standard*, na itakuwa na madini ya *iodine*, kwa hivyo katika mkakati wetu wa mwaka huu kuona kwamba kiwanda hiki kinafufuka na chumvi kutoka Pemba inauzwa. Inatuuma sana kuona Zanzibar kunauzwa chumvi ya Tanga na chumvi ya Mombasa wakati visiwa hivi vimezungukwa na chumvi. Ninakupongeza sana na tutafanya kazi pamoja ili chumvi ya Zanzibar iuzwe Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti mimi sina nia ya kung'ang'ania hapa lakini pia katika taarifa niliyoipata ni kuwa Wizara ya Kilimo ndio inayotoa kibali kwa wakulima wa chumvi. Sasa hapa nataka

nijue hao Wizara ya Kilimo wanawasaidia nini wale wakulima wa chumvi wakati wanatoa kibali na wao kibali hawapewi bure wanalipia. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti naomba nisaidiwe pia.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti wasiwasi wangu isije kuwa Mheshimiwa anazungumza wakati Wizara ya Kilimo imekuwa imekusanya yote ya bahari na kilimo, nilikuwa nazungumza hilo na kuna wakati Wizara ya Kilimo ilikuwa imekusanya yote ya bahari pamoja na uvuvi na mambo mengineyo isijekuwa anazungumza wakati huo. Lakini wenyewe wameshakiri kabisa kwamba wao wanahusika na masuala ya chumvi.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri Mhe. Salma kwanza tukupongeze kama walivyokupongeza Waheshimiwa Mawaziri juu ya suala hili na Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi tayari ametoa ahadi kufuatilia jambo hili, sasa ukubali ahadi hiyo ingefaa tu ukafuatilia ni namna gani utaweza kuifanya shughuli hiyo pamoja na kutimiza hiyo ahadi ambayo Mhe. Naibu Waziri ameitoa hapa. Nafikiri ungefikia hapo tukakubaliana na kuendelea.

Lakini pia kuhusu habari ya jina la yule mtaalamu nadhani hiyo isiwe hoja ya kutuzuia, maana ulisema lakini haikuwahi kutoka majibu, muendelee kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu Waziri kufuatilia suala hilo la chumvi kwa ujumla wake na pale ambapo Mhe. Waziri wa Kazi yeye ni mtu wa kazi basi na yeye pia mnaweza mkampa taarifa baadae, hasa kwa vikundi mbali mali hivyo ambavyo vinahitaji kupata msaada kutoka Wizara hiyo ya kazi. Nadhani turuhusu tuendelee.

Kifungu 1702

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi nilipochangia Mhe. Mwenyekiti nilisema kama katika mapinduzi ya kilimo hayakuja kwa ajili ya kilimo cha mpunga tu lakini hata sehemu nyengine tu wanahitaji kuona mapinduzi ya kilimo. Sasa nikatoa mfano kama kule kwetu Micheweni, pia nilitaja Makunduchi kama ndizi zikimwagiliwa maji zinakubali kwa wingi sana, na nikazungumza kwamba Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Kwanza wa Rais walikuja Micheweni na wakakagua eneo kwa ajili ya kufanya kilimo cha mfano cha kumwagilia maji kwa ajili ya kupata migomba. Sasa nilikuwa nataka kujua tu suala lile naona lilifia lakini nataka kujua watu wa Micheweni karibu mwaka wa tatu wanalima mtama lakini hawavuni, inakuwa mpaka imeshafika katikati inagonjwa haipatikani kitu chochote, sasa nilikuwa nataka kujua tu katika utafiti wao wanaoufanya watu wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti wamefanya utafiti gani na kuona kama katika kanda zile za maweni

mashariki, wanajipanga vipi kuona kwamba watawapa elimu watu wa maweni kuona kama wanalima vilimo ambavyo vinaweza vikawasaidia baadae kuliko kulima vilimo ikawa hawapati chochote.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara kazi yetu kutoa taaluma kwa wakulima, na kazi hii Wizara inafanya kutoa taaluma hii kwa wakulima na kujua kwa kufanya utafiti ili kujua watu wa Micheweni ni kilimo gani ambacho kitawasaidia. Mimi nina imani Mhe. Mwakilishi, atuachie kazi hii, bado tunaifanya na tutaendelea kuifanya hasa kwa Jimbo lake la Micheweni.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia sana Mhe. Naibu Waziri na nia yangu si kuzuia fungu wala kuzuia kifungu, lakini nia yangu ni kuwakumbusha pamoja na kuwa najua kama wanakumbuka kwa sababu ni wajibu wao, lakini ninaomba hili suala walipe kipaumbele waone kama kuna haja na hizi kanda za mashariki maweni humu basi wanahitaji nao kufikiwa na elimu hiyo, na hao mabwana shamba wakafika wakaenda wakafanya kazi ikiwa wapo, kwa sababu sisi tunasikia tu kama mabwana shamba wapo lakini hatujawahi kuwaona. Kwa hiyo kama wapo basi wafike ili wawasaidie wakulima, na kama hawapo basi tunahitaji na sisi kuletewa hao mabwana shamba ili kuwasaidia watu katika vilimo vyao, hasa ukiangalia kama vilimo vya Micheweni na kanda ya mashariki ni vilimo vya msimu maalum, kwa sababu ni sehemu ambayo ni ya ukame, mvua zake ni mvua maalumu. Kwa hiyo ule wakati zinapokuwa mvua zinanyesha basi wawasaidie wananchi ili waweze kuvuna wasiwe wanatoa jasho lao bure.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia na kutokana na umuhimu wa Wizara hii nilisema kuwa tumekabiliwa na athari ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo inasababisha ongezeko la joto, inasababisha mvua zisizo na uhakika zisizotabirika, upepo mkali, bahari kupanda juu na ongezeko kubwa ya hewa mkaa, yote haya yataathiri katika kilimo. Na kwa sababu kuna Taasisi hii ya Utafiti nilitaka nijibiwe imejipanga vipi katika kutafuta mbegu ambazo zitaweza kustahamili vishindo vyote hivi vya tabia nchi ili binaadamu wasije wakafa kwa njaa.

Mhe. Mwenyekiti, kule kwa wenzetu Tanzania Bara panapotokea mambo kama haya wanapewa tahadhari na wanapewa mbegu maalum wakulima, ambazo zitaweza kustahamili katika hali zote, lakini huku ni kimya na hasa tumeona katika mbegu zilizogaiwa safari hii na Serikali, kuna mahala zimewekwa sana na kuna mwahala hazikuwepo kabisa, kwa sababu kila mahala pana aina yake ya mbegu. Kwa hivyo Wizara hii katika kutumia hii *section* yake ya utafiti ya kilimo imejipanga vipi kwa kuweka mbegu ambazo

kwa vile tumo katika janga hili zitoweza kustahamili matatizo haya na binaadamu waweze kuishi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati :(Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikisoma hotuba yangu nilitaja malengo kwa mwaka 2012/13, na nikataja kwamba mazao yote ambayo yanafanyiwa utafiti ili kuweza kunusuru mazao, sasa utafiti sio mazao kuzagaa lakini pamoja na kustahamili hali ya hewa iliyopo na mabadiliko ya tabia nchi. Nilisema kwamba utafiti wa zao la mpunga limejumuisha mbegu 76 kutoka vituo vya utafiti vya ndani na nje ya nchi ikiwemo IRRI, African Rice, Vietnam zinajaribiwa katika mabonde ya Mtwango, Kizimbani, Tungamaa na Mwera. Matokeo ya awali inaonesha miongoni mwa mbegu 76 zilizofanyiwa utafiti mbegu za aina tano zimeonekana kufanya vizuri, na utafiti kwa mbegu zilizobakia bado unaendelea. Ina maana katika mpunga tushapata mbegu tano zinazostahamili hali ya hewa yetu ya Zanzibar na kufanya vizuri kati ya zote zile zilizofanyiwa utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, halafu Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na programu ya *feed the future* imewapatia mafunzo wakulima 400 juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mpunga. Kuanza kutayarisha ardhi mpaka hatua za uvunaji katika mabonde ya Bumbwisudi, Kilombero na Kipange. Utafiti wa kupata mbegu za muhogo vile vile ambao nao pia unastahamili ukame, zinazostahamili maradhi na zitakazokuwa na uzazi mkubwa umefanyika katika vituo vya utafiti vya Kizimbani na Matangatuani. Utafiti maana yake unatizama lile zao lenyewe pamoja na ustahamili wake wa hali ya hewa na utafiti katika Idara ya Utafiti. Na ndio maana watu wetu wa Kilimo wanapopita katika maeneo wanasema hapa bora panda mbegu fulani kuliko kupanda mbegu fulani, kama nilivyosema mwanzo ukipanda mbegu zote za zamani haziwezi kupatikana kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, hii kazi inafanywa na Idara ya Utafiti na nimezungumza katika hotuba yangu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana, sana kweli kweli kwa maneno ya Mhe. Waziri, lakini ningeliomba kusema hivi Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi niliposisitiza kwenye utafiti si kwa kuwa sikufahamu anavyozungumza, lakini siku zote unapoleta mbegu mpya kuna mawili hutokea, kama utafiti wako haukuwa mzuri inaweza ikawa mwaka wa kwanza mwaka wa pili ikawa tena haiendelei na hilo limewakumbuka hata nchi zilizoendelea katika utafiti wa mambo haya kwenye kilimo na kwenye mifugo. Yeye anasema atatafuta mbegu inayostahamili hapa, atafuta mbegu inayostahimili hapa, anatilia maanani kuwa tunataka hizi ziwe endelevu na endelevu na endelevu, isije ikawa kama wenzetu wa mifugo na uvuvi, tokea 1984 tumo katika mpango wa machotara

mpaka leo hatujapata lolote, kwa sababu kizazi kama hukufanya utafiti wa kutosha hakiwezi kuwa endelevu. Tunataka kitu ambacho kitaweza kuwa endelevu pia wawe wanatilia maanani haya, wao wanataka kuweka mbegu halafu zije zifeli tuingie katika matatizo, janga la njaa hatuliwezi wala hatuna pesa za kuagizia chakula.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati :(Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na mawazo yake na kweli hii inatokea, lakini Idara ya Utafiti pia inatizama utafiti aina ya udongo na mbegu gani inaweza kuota katika udongo fulani. Na nilisema vile vile kwamba kuna mapitio ya ramani ya aina ya udongo wa Unguja na Pemba kwa kutumia mfumo wa *digital* ambao utafiti huo unaendelea hivi sasa juu ya udongo gani unaotesha mazao gani na udongo gani unaotesha mazao gani, hiyo jitihada tunaifanya, tunajitahidi sana katika sehemu ya utafiti.

Kifungu 1702	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Pemba	25,080,000/=
Kifungu 1703	Idara ya Misitu na Maliasili Pemba	88,760,000/=
Kifungu 1704	Idara ya Umwagiliaji Maji Pemba	36,480,000/=
Kifungu 1705	Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba	1,556,052,000/=
Kifungu1706	Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe Pemba	18,240,000/=
Kifungu 1707	Idara ya Kilimo Pemba	41,040,000/=
Kifungu 1708	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Pemba	

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia kama Wizara ya Kilimo ifanye utafiti kwanza ndio iwape wakulima mbegu. Kwa taarifa niliyoipata katika kipindi cha Mawio. Mhe. Mwenyekiti, katika majibu Mhe. Naibu Waziri alisema kama taarifa hiyo hata yeye aliisikia, lakini mbegu ile haikuchanua kwa sababu ya ubovu, bali haikuchanua kwa sababu ilitiwa si muda. Sasa namuomba Mhe. Waziri, hapa anifahamishe ilikuwaje kuwapa wakulima mbegu ambayo si kipindi chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mwakilishi, alichangia kuhusu mbegu ambayo ilitolewa katika bonde la Dobi na Kinyakuzi. Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo yanatokea ni mambo si ya kukusudia. Hata nyumbani Mhe. Mwenyekiti, unaweza na hilo tatizo limeshatokea unaweza ukaweka mafuta ya taa na mafuta ya petroli lakini wakati wa kunyanyua ukanyanyua petroli ukatia kwenye kibatari hatimae ukawasha ikakukuta athari. Kwa hiyo jambo lililotokezea hapa ni kwamba mbegu iliyokuwa imekusudiwa ipandwe pale ni mbegu sio iliyokusudiwa, lakini wakati wa kuwekwa mbegu ile kwa bahati mbaya si kwa makusudi, kulikuwa kuna sehemu mbili; sehemu moja kuna magunia ambayo

yamewekwa mbegu *bican super* ambayo yalikuwa yako pamoja, na nyengine ikawekwa super india, *super india* ni mbegu ambayo huwezi ukapanda wakati wa vuli.

Mhe. Mwenyekiti, kilichotokea pale ni kwamba wakati wa kutiwa lebo ndio hapo ilipokuja kutokea mtihani na mtihani huo unamtokea binaadamu yoyote. Wakati wa kutiwa lebo kwa bahati mbaya mbegu ya *dicen super* ikaja ikawa lebo *ya super* india, na ile ya *super india* ikawekwa lebo *dicen super*. Wakati wa kuja kupelekwa mabondeni unachukua ile una uhakika kwamba mbegu hii wakati lebo yake ishasomwa nje, hii ni mbegu ya *bican super* hupelekwa mabondeni, tizama, na kilichotokea mtihani wa Mwenyezi Mungu hata wakati wanapanda wakulima mbegu yoyote ukiikamata mkononi bila ya shaka utajua, hii rinda, hii moshi lakini hata yeye mwenyewe mkulima hakuweza kutambua kwamba hii ninayoipanda ni mbegu gani, kwa sababu mbegu ukiikamata mkononi wataalamu wetu wanajua hata wakulima wetu, hata na mimi nilikuwa na utaalamu huo nikiikamata najua nakwambia hii ni mbegu ya *super*. Lakini wakulima wale hawakuweza kujua mpaka wanaipanda, kilichokuja kutokea wakati wa kuchanua mpunga ule unachanua unakwenda juu tu, ndio maana tukasema kwamba mbegu ile si mbovu, ingelikuwa mbovu mbegu ile isingeota, kitu chochote hakioti, lakini kutokana na mbegu iliyopandwa pale kwa bahati mbaya ni mbegu ambayo haihimili wakati wa vuli, hicho ndicho kilichotokea kwa bahati mbaya kubadilishika magunia.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimeyasikia majibu ya Mhe. Naibu Waziri, na bahati mbaya ni hakika inatokea popote hata mie ni mpishi siku nyengine chungu baada ya kutia sukari hutia chumvi, hivyo mambo haya yanatokea. Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala la kilimo ni jambo kubwa, wananchi wanatumia nguvu nyingi, na hapa lililotokezea anasema ni mbegu kubandikwa lebo iliyokuwa siyo. Sasa hapa ninamuomba Mhe.Naibu Waziri au Waziri anieleze ni hatua gani zilizochukuliwa za wale wataalamu waliobandika mbegu iliyokuwa siyo na kuwatia hasara wakulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kitu chochote kilichotokea kwa bahati mbaya huwezi ukamchukulia mtendaji hatua, ni kitu ambacho utakwenda kinyume hata katika sheria ya dini, kitu kikitokea kwa bahati mbaya nadhani Mhe. Mwakilishi anajua inapotokea athari njiani mtoto wako kapigwa na gari kwa bahati mbaya huwezi ukamchukulia hatua. Kwa hivyo hii hatukuchukua hatua, kwa sababu ni kitu ambacho hakukusudia Mtendaji, lakini baada ya kilichotokea hapo nilimueleza katika majibu yangu kwamba wakulima wale walioathirika wote tumewalipa fidia.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linasema kutojua sheria sio sababu ya kufanya kosa, kwa hiyo hapa namuomba Mhe. Waziri, yeye sina haja ya kubishana naye sana, lakini wataalamu wetu ni lazima wawe makini, kwa sababu pale zinatumika nguvu nyingi na hatimaye hasara ni kubwa inayopatikana. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1708	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Pemba	27,360,000/=
Jumla ya Fungu		**12,569,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 20 WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Kifungu 0401

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa tena. Wakati nilipokuwa nikichangia nilitaka maelezo juu ya tija ya miradi hii ya maendeleo yote ambayo iko katika Wizara hii ya Kilimo, tuje Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika majihu niliyopewa niliambiwa kwamba miradi imetolewa maelezo katika kitabu cha hotuba ya bajeti. Mhe. Mwenyekiti, mimi kitabu cha hotuba ya bajeti nimekisoma, lakini ninaomba nimsaidie Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwanza kwamba miradi iliyoorodheshwa hapa katika hili buku la makadirio ni miradi 14, miradi iliyotolewa maelezo katika kitabu cha Mhe. Waziri, katika viambatanisho ni miradi 9, lakini sitaki kulizuia Baraza kwa maelezo marefu, maana nikiamua kwenda moja moja kwanza zitazidi hoja tatu, na nadhani itakuwa narefusha muda bila ya sababu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa mfano mmoja tu kuhusu hoja yangu. Wakati nilipochangia nilisema hoja yangu kwamba moja ya matatizo makubwa tunayoyaona katika Serikali ni kuwa na miradi mingi inayotumia fedha nyingi za maendeleo lakini halafu ile *end product* inakuwa haionekani. Na nikasema Mhe. Mwenyekiti, kwamba bahati mbaya sana tusije tukachukulia kwamba fedha hizi ni fedha labda za misaada, kwa sababu ukiangalia katika ukurasa wa 459 kwenye jumla ya fungu utaona kwamba jumla ya fedha hizi ni 17,751,998,000/= katika hizo mikopo ni 14,023,596,000/=, sehemu kubwa sana ya fedha hizi ni fedha za mikopo, hoja yangu ikawa ni kwamba hizi fedha ni gharama inayotokana na walipa kodi wanyonge wananchi wa Zanzibar; ambapo zitaendelea kubakia kuwa deni kwao la taifa kwa miaka mingi likilipwa na kodi zao, sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti ni kwamba tija yake iko wapi?

Mhe. Mwenyekiti, nilipoambiwa nifanye *reference* au nifanye marejeo katika kitabu cha Mhe. Waziri, ndio nilipopata *shock*. Sasa kwa sababu sitaki kuyazungumza yote naomba nitoe mfano mmoja tu Mhe. Mwenyekiti. Naomba tuangalie kijifungu cha 610017 programu ya miundombinu ya soko, kuongeza thamani za bidhaa na misaada ya kifedha vijijini, *marketing infrastructure, value edition and rural financial support program.* Nataka Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mbona hatuoni na miradi hii ya kusarifu mazao na kuongeza thamani inajirejea katika miradi mengine vile vile, sasa nikasema mbona katika uhalisia hatuoni hizo shughuli zikifanyika Mhe. Mwenyekiti, kwamba tunaona bidhaa ambazo zinatengenezwa Zanzibar zikiwa zimetokana na kuongezea thamani au inatokana na usarifu wa mazao.

Mhe. Mwenyekiti, tukikiangalia kitabu hichi, nimalizie hoja yangu. Mradi huu una fedha nyingi sana tukisoma ukurasa wa 47 ya hotuba ya Mhe. Waziri, programu inatarajia kupata 60,000,000/= kutoka SMZ na zile za mikopo ya misaada ni 9,348,560/=, lakini ukitizama malengo yake ndio yanayotia mashaka. Sasa nilikuwa nataka nisaidiwe kuna suala humu la kutengeneza au kukarabati kuna mita mia za barabara za mashambani; ambapo mwaka jana lilikuwemo kwa mujibu wa maelezo yao ya utekelezaji halikutekelezwa linahamishiwa mwaka huu. Mradi Mhe. Mwenyekiti, ambayo ukiyatizama hayaendi sambamba na thamani halisi iliyowekwa na mradi wenyewe, kwa hiyo nimeliuliza kwa mfano huu, lakini nimeliuliza kwa pamoja kwamba fedha hizi nyingi 17,000,000,000/= za fedha za maendeleo, tija yake kwa ujumla wake katika mafungu mbali mbali yaliyoelezwa hayaonekani, ndio narudi kule kule kama nilivyotoa mfano kwenye uhakika wa chakula na lishe kwamba fedha nyingi zinaishia katika miradi ya kuunda kamati, kutoa mafunzo, lakini tija ya mwisho iliyokusudiwa katika miradi ya maendeleo haionekani, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati :(Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine huwezi kuyajibu ghafla hapa mpaka ukaione hiyo miradi yenyewe namna ilivyotekelezwa, na najua mimi kwamba kuna masomo tayari yameshajengwa na barabara baadhi ya mabonde tayari zimeanza na baadhi ya mabonde barabara nyengine zinategemewa kuendelea, hata tulipofanya ziara ya Rais lilichomoza hilo kwamba kuna maeneo barabara zinatoka katika mabonde ya mpunga kwa kurahisisha wakulima katika mabonde yote. Sasa hapa mimi labda nimwambie tu Mhe. Mwakilishi, ili apate ushahidi mzuri zaidi ashirikiane na Wizara ya Kilimo na aombe aoneshwe hizo barabara zilizojengwa pamoja na hayo masoko yaliyokwisha kutengenezwa katika maeneo mbali mbali, labda atapata jibu lililo zuri zaidi kuliko kumueleza hapa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe, Mwenyekiti, labda ndio ile '*nyimbo ya kufundishwa haikeshi ngoma'*. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 47 kwa maelezo tuliyopewa inapingana na maelezo aliyonambia Mhe. Waziri sasa hivi, anatuambia barabara zimeanza naomba nisome Mheshimiwa.

"Malengo 2012/13 kukarabati barabara za mashambani kilomita 50 na ununuzi na ufungaji wa mitambo miwili ya kuzalisha barafu kiutekelezaji, ukarabati wa barabara na ununuzi wa mitambo ya kuzalisha barafu haukufanyika, kutokana na mabadiliko ya mpango wa manunuzi wa AfDB na badala yake umepangiwa kufanyika mwaka wa fedha 2013/14" .

Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano wa pili nipate kumaliza hoja yangu, vifungu vitatu vimewekwa kwa pamoja vilikuwemo mwaka jana hivi.

'Kuwajengea uwezo na kuwaunganisha na masoko wazalishaji wadogo wadogo, kuwapatia mafunzo ya uzalishaji juu ya uhifadhi na usarifu wa mazao, na kuandaa ziara za kimasomo kwa vikundi kwenye masoko na kuona usindikaji wa mazao"

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji huo, kitabu chao hicho kinasema hivi:

"Kazi hizi zilitegemea watoa huduma kutoka sekta binafsi ambapo mchakato wa kupatikana watoa huduma umefikia hatua ya majadiliano", mwaka mzima Mheshimiwa huo, na unangojea baraka za Mfadhili no objection na kufungiana mikataba

Mhe. Mwenyekiti, haya yanajirejea sitaki kurejea kila pahala kwa sababu ni miradi mingi. Mimi katika hili kwa sababu najua mara nyengine Mhe.Mwenyekiti tunapotoa mifano hii tunajua hapa hatupati maelezo kwa sababu maelezo yenyewe hayapo, kwa hiyo haina haja ya kuzuia fungu hapa tukaendelea kupigishana kelele Ramadhani hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba hili nimuombe Mhe.Mwenyekiti wa Kamati yako Mhe. Salmin Awadh ambaye ni mzoefu na anaiongoza Kamati hii kwa muda mrefu, haya katika katika kazi zao na bahati nzuri anasaidiwa na Kamanda mzuri Makamo Mwenyekiti wake Kamanda Hija Hassan Hija, basi niwaombe hii na Wajumbe wao kwa pamoja lakini na baadaye na PAC watizame hili katika fedha za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi wasi wasi wangu mkubwa pia nitaendelea kusema hivi kwamba miradi hii inapokuja kuunganishwa na Wizara ya Fedha tutakuja kuona tukifika huko, tunaona kuwa miradi haiendi mbele ni kwamba Wizara ya Fedha imeng'ang'ania miradi yote hasa ikiwa mikubwa ikiwa na fedha nyingi kama hizo halafu tija yake haionekani. Kwa hivyo hili mimi niombe tu

kwamba Kamati yetu ilifuatilie kwa kina fedha hizi za miradi ya maendeleo yote iliyoorodheshwa hapa, waone tija yake inapatikana au ndio tunaishia katika kuunda kamati nne za sheria zile na ndio inakuwa mwisho wa hadithi. Tumechoka na hadithi hizi tunataka kuona matokeo ya fedha hizi za walipa kodi zinavyoidhinishwa na Baraza zinatumika kuleta tija iliyokusudiwa sio kuishia katika matumbo ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naiomba Kamati ichukue shughuli hii tukikubaliana hapo nasema tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri ni kazi ya kawaida, unawasaidia kamati tu ili wajue moja ya sehemu ya kazi ambayo wanapaswa kuifanya ni hiyo, nadhani Mhe. Salmin, Mwenyekiti na makatibu watakuwa wanajua hilo kupitia *hansard* ili kupanga ratiba ya shughuli zao, una maelezo kidogo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati :(Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, Mhe.Jussa anaposoma hizo taarifa yanayofanyika hayasomi, husoma yale yaliyokuwa hayakufanyika. Kwa hivyo ni vizuri hilo pendekezo alilolitoa mimi nalikubali, na kamati iende ishirikiane na Wizara ya Kilimo katika kufuatilia masuala hayo. Kwa sababu na mimi pia nataka utakelezaji wa Wizara ya Kilimo ufanyike vile vile kwa ajili ya wananchi kwa sababu ni sehemu ya walipa kodi, hivyo nakubaliana na wazo lake kwamba Kamati iende ikashirikiane na Wizara ya Kilimo na ataoneshwa kipi kimefanyika na kipi hakijafanyika, nakubaliana na wazo lake kabisa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sina nia ya kunyanyuka lakini sitaki yakae maelezo ya Mhe. Waziri, yakarikodiwa bila ya *challenge*. Mhe. Mwenyekiti, nimesema nikisema yote hapa tutaendelea kupoteza muda wa Baraza, lakini nataka nisome vifungu viwili vinavyosema kwamba ni kutoa mafunzo ya upangaji, utekelezaji na utunzaji wa miradi ya miundombinu, mafunzo yaliyotolewa kwa miradi kumi na tatu yakiwa saba kutoka katika Idara ya utengenezaji wa barabara na Ofisi ya Mazingira wilaya tano na Mhandisi mmoja Idara ya Umwagiliaji ndio *component* pekee hiyo.

Tuje ya mwisho sasa, kuwapatia mafunzo ya kujenga uwezo wafanyakazi wa Idara ya Ushirika, SACCOS pamoja na Wajumbe wa Bodi za SACCOS, tizama ilivyotokezea Mhe. Mwenyekiti, programu imelipia mafunzo kwa maofisa watano wa Idara ya Ushirika kwa ngazi ya cheti na *diploma* katika fani ya huduma za kifedha vijijini na uhasibu wanaotumia teknohama imeishia katika utawala katika Wizara. Hawa wahusika hasa kwenye SACCOS hakuna maelezo hapa, kwa hivyo ndio wanaposema utekelezaji ni huu kwamba fedha zinamalizikia kunufaisha watendaji wa Wizara tu, lakini

walengwa narejea kusema tena walengwa ambao ni wananchi, na hapa ilikuwa walengwa ni hizi SACCOS ambazo wameziandika wao wenyewe lakini katika utekelezaji huzioni zimeishia ku-*sponsor* wanafunzi, watendaji wa Wizara kwenda kusoma diploma na cheti lakini wajumbe wa bodi za SACCOS, SACCOS zenyewe hazimo kwenye utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo asitunukuu vibaya, tukiamua kusoma kila kimoja tukakihakiki tutafika kesho, kwa kifupi Mhe. Mwenyekiti, bado kuna tatizo kubwa sana la fedha hizo za miradi ya maendeleo na utekelezaji, hili Serikali ikitaka isitake inaonekana katika ripoti zao wanazotuletea wao wenyewe humu ndani. Ahsante naomba tuendelee.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa nilisema kwamba wapo wajasiri amali waliojikusanya katika kijiji cha Pangani Kukuu ambao wanajishughulisha na uatikaji wa miche ya mikarafuu, lakini kwa bahati wakaenda Wizara ya Kilimo kwenda pale kununua miche ile, lakini hadi hii leo bado wananchi wale hawajalipwa fedha zao. Je, Mhe. Waziri, nilimuuliza ni lini atakwenda kule kuwalipa fedha zao wananchi wale.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuna watu ambao walichukuliwa miche yao hawajalipwa, lakini tunaahidi Mhe. Mwakilishi kabla ya sikukuu fedha zao ambao hawajalipwa watalipwa wote.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	17,751,998,000/=
Jumla ya Fungu		**17,751,998,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati :(Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imekaa na kupitisha makadirio ya fedha za Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: sasa niwahoji wale wanaokubaliana ha hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda (Makofi).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nirudie tena kuwashukuru kwa sababu shughuli hii tuliianza jana tena kipindi cha wakati wa dhiki kidogo, muda ulikwishakuwa mkubwa lakini leo tumemudu kuimaliza. Nafikiri kwa hali yetu na hotuba zilizobaki tukienda kwa utaratibu huu nadhani tutafika pahala pazuri na kumaliza kwa wakati. Sasa Wajumbe kuna tangazo moja dogo, Waheshimiwa Wajumbe mara baada ya kuondoka humu ndani kutakuwa na kikao kifupi sana cha *caucus* zote mbili; moja ya Wajumbe wa upande wa CCM na nyengine ya Wajumbe wa upande CUF. Taarifa niliyoletewa hapa ni kwamba wajumbe wa cocus ya CCM watakutana pale juu, na wajumbewa cocus ya CUF watabakia humu ndani baada ya hawa Wajumbe wengine kuondoka. Kikao hicho nataka nithibitishe ni kifupi sana chenye mnasaba wa shughuli zetu kuzifanya kwa ufanisi mkubwa.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe nirudie kuwashukuru kwa mashirikiano makubwa na sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 31/7/2013, saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 9.04 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 31/07/2013 saa 3.00 za asubuhi)